

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Kumi – Tarehe 21 Aprili, 2008**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Spika Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ILIYOWASILISHWA MEZANI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MUUNGANO) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa Mwaka 2006/2007 (*The Annual Report and Accounts of the National Environment Management Council (NEMC) for the year ended 2006/2007*)

**MASWALI NA MAJIBU**

Na.119

**Wananchi Kuchangia Shughuli za Maendeleo**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE (K.n.y. MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) aliuliza:-**

Kwa kuwa ushirikishwaji wa wananchi katika miradi ya maendeleo ni jambo la kiungwana na kizalendo; na kwa kuwa katika kufanya hivyo Serikali za Mitaa zimekuwa na utaratibu wa kuwachangisha wananchi kwa nguvu, fedha na vitu mbali mbali:-

- (a) Je, Serikali inayo taarifa ya uchangiaji huo unaofanywa kiholela huko vijijini na kusababisha usumbu na kuwanyima raha wananchi?

- (b) Je, Serikali iko tayari sasa kuandaa mfumo rasmi wa uchangiaji kwa nchi nzima utakaozingatia pato la mwananchi wa kati unaofaa kuchagiana kulingana na hali halisi ya uwezo wa mwananchi husika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba ushirikishwaji wa wananchi katika miradi ya maendeleo ni jambo la kiungwana na la kizalendo. Aidha, ushirikishwaji huo unaongeza nguvu katika juhudhi za Serikali za kuwezesha kuwepo kwa maendeleo ya wananchi kijamii na kiuchumi. Vile vile unafanya kuwepo kwa maendeleo endelevu. Kama yapo maeneo ambayo michango hii inafanyika kiholela, ni wajibu wa Serikali za Vijiji na Mitaa kuhakikisha kuwa michango inayotolewa na wananchi ni ile ambayo wananchi wa maeneo husika wamekaa ana kukubaliana katika kuchangia miradi ya maendeleo yao wenyewe.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu mfumo rasmi wa kuchangia, tunafahamu kuwa ipo mifano mingi ya michango, baadhi ni ile inayotokana na sheria ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa mfano, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa upo mchango wa Mfuko wa Elimu ambao umewekwa kuititia sheria hizo. Sheria inatamka kuwa kila mkazi mwenye uwezo wa kufanya kazi atachangia kiasi cha shilingi 5,000/= kwa mwaka. Aidha, sheria ndogo hizi hutungwa na Serikali za Vijiji na kuidhinishwa na Halmashauri ya Wilaya husika.

Mheshimiwa Spika, iko baadhi ya miradi ya kitaifa na ya wafadhili ambayo inaambatana na michango ili wafadhili waweze kutoa fedha, wananchi wanatakiwa kuchangia. Kwa mfano; Mradi wa *TASAF* wananchi wanatakiwa kuchangia asilimia 20 ikiwa ni pamoja na fedha taslimu pamoja na nguvu kazi.

Kadhalika Miradi ya MMEM, MMES, *PADEP* na miradi mingine. Miradi ya Maji Vijijini sharti wananchi wachangie asilimia 5 ya thamani ya fedha zote za mradi. Miradi yote hiyo wananchi huelimishwa kwanza kabla ya kuchangishwa. Na wananchi walio wengi, wakishaelimishwa, huchangia bila matatizo yoyote. Mchakato mzima wa kuchangia shughuli za maendeleo unamilikiwa na wananchi wenyewe katika maeneo husika.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali ya nyongeza. Kwanza, niwapongeze wananchi kwa kufanya kazi nzuri ya kujenga shule za sekondari na shule za msingi. Sasa swalii, kwa kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya kukamilisha majengo hayo hasa shule zetu za sekondari kwenye kata ni kidogo sana. Je, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana

nami kwamba pamoja na nguvu za wananchi, Serikali itakuwa tayari katika bajeti ya 2008/2009 kupanga fedha za kutosha ili kusaidiana na nguvu za wananchi hasa katika ujenzi wa shule za sekondari za kata?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA:** Mheshimiwa Spika, Serikali kazi yake ni kutafuta fedha kutoka kwenye vyanzo vyetu wenyewe na pia kutoka kwa wafadhili na kuzipeleka katika Halmashauri husika. Katika ujenzi wa sekondari, si fedha za MMES peke yake ambazo zinatengwa kwa ajili ya kazi hiyo, pia ziko fedha mbali mbali ambazo Serikali imepeleka. Kwa mfano; fedha za *Local Government Capital Development Grants* ambazo ahazina masharti yoyote. Halmashauri husika ndiyo inayopanga kwa ajili ya shughuli mbalia mbali. Kwa hiyo, fedha zinapopelekwa kwenye Halmashauri ni Halmashauri husika ambayo inapanga ni kipi kipaumbele katika kutekeleza miradi ya maendeleo. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha zikipelekwa huko, zipangwe kulingana na vipaumbele na sisi kama Serikali tutakuwa tunatafuta fedha ili kuhakikisha kwamba shule za sekondari zinajengwa na miradi mingine pia inaendelea.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini naomba niulize swali hili moja. Itokeapo wananchi wameamua kuchanga na wapo wengine wakaja wakawaambia msichange kwa sababu maendeleo ni jukumu la Serikali, wao wanapinga michango. Je, Serikali inasema nini juu ya watu hao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna malalamiko mengi kwenye baadhi ya maeneo kwamba kuna watu wanapita wanawashawishi wananchi wasichangie shughuli za maendeleo. Lakini, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, mjenga nchi ni mwananchi na mbomoa nchi ni mwananchi. Kwa hiyo, hao amba wanapita ili kubomoa nchi, sisi kama Serikali tutawachukulia hatua.

Mchango kwa ajili ya maendeleo ni jukumu la mwananchi na siyo hiari, ni lazima achangie kwenye shughuli za maendeleo. Sisi kama Serikali hatuwezi tukafanya kila kitu. Kwa hiyo, tunapotoa fedha kidogo, inabidi wananchi wachangie ili kuleta maendeleo yao. Mimi niseme tu kwa wale wenzetu wanaopita pita kufanya kampeni kwa ajili ya kuwarubuni watu wasichange michango, kwamba Serikali tutawashughulikia watu hao ili wale wachache wanaochanga wasije wakavunjika moyo.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nataka kuuliza kama ifuatavyo:- Kwa kuwa michango hii hasa MMES kuchangia nyumba za walimu na madarasa imeonyesha mafanikio. Lakini kwa kuwa kuna dosari kidogo, uchangiaji wake unapokuwa katika utaratibu wa msako na unapofanyika katika miezi ambayo wananchi hawana hela – Desemba hadi Machi, ambapo hawana chakula, hawana pesa, hawana hela ya kununua pembejo za kilimo; Je, Serikali itakuabaliana na ushauri wangu kwamba michango hiyo ifanyike wakati wa msimu wa mavuno kwa mfano;

kuanzia mwezi Juni – Oktoba ili kuondoa kero hiyo kama Waziri Mkuu ambavyo amewahi kusema?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba watendaji wetu wakati mwingine wanatumia excessive power na hawaangalii wakati muafaka. Naomba nikubaliane kwamba ni kweli michango itolewe wakati muafaka hasa wakati wa mavuno ambapo wananchi wanavuna na wanaauza mazao yao. Siyo vizuri kwa mwananchi kuchangishwa wakati wa kilimo au wakati wa njaa. Ni sawa na kwenda kuomba jamvi wakati wa msiba. Kwa hiyo, naomba nikubaliane na hilo ndilo alilolisema Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye ziara yake kule Rukwa kwamba tuangalie muda muafaka wa kufanya michango hiyo. (*Makofî*) Na. 120

### **Uboreshaji wa Zahanati na Vituo vya Afya**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza :-

Kwa kuwa, Serikali imakusudia kwanza kuboresha zahanati na vituo vya afya vilivyopo kabla ya kuanza ujenzi wa zahanati na vituo vya afya vilivyopo, hatua ambayo naiunga mkono na kuipongeza:-

- (a) Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya kupanua kituo cha afya cha Izigo na kile cha Kamachumu?
- (b) Je, Serikali imechukua hatua gani za kushirikiana na wananchi wa Kata ya Bulyakashaju katika kujenga zahanati ya Kata katika kijiji cha Lugando?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla ya sijajibu swali la Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamiii inatekeleza Mpango wa Maboresho ya Sekta ya Afya. Moja ya malengo muhimu ni utoaji wa huduma za afya katika mazingira bora na majengo mazuri. Serikali kwa kushirikiana na wahisani inatoa fedha za ukarabati wa vituo vya kutolea huduma ya afya ya msingi (zahanati na vituo vya afya) katika mamlaka za Serikali za Mitaa. Chini ya mpango huu wa ukarabati, jukumu la Serikali ni kutafuta na kupeleka fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Majukumu ya Halmashauri ni kufanya uteuzi wa vituo kwa kuzingatia ubovu wa zahanati au kituo cha afya, kutoa ushauri wa kitaalam kwa kamati za afya za vituo, kufuutilia na kufanya tathmini ya utekelezaji. Jukumu la wananchi kuititia kamati zao za afya za vituo ni kuandaa mipango ya ukarabati na ujenzi, kuteua wazabuni, kusimamia

kazi za kila siku, kuidhinisha malipo kwa kazi zilizofanyika. Ushirikishwaji wa wananchi katika shughuli za maendeleo ni jukumu la msingi la Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, mwaka 2005/2006, Serikali ilipeleka jumla ya shilingi 198,800,000/= kati ya shilingi 284,000,000/= zilizotengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Muleba kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya afya vya Kaigara na Izigo na zahanati za Kyamyorwa, Ruhanga, Mubunda, Kimwani, Kibanga, Bumbire, Kishanda, Kagoma, Omurunazi, Karambi, Bukekyo, Kabare, Buganguzi, Ilemera na Nyakabango. Halmashauri ya Muleba iliona kwamba vituo hivi ndivyo vilivyokuwa vibovu kuliko vingine.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) inaendelea kuandaa mchakato utakaowezesha ujenzi wa zahanati kila kijiji na vituo vya afya kwa kila kata na katika mpango huu zahanati ya kijiji cha Lugando na kituo cha afya katika kata ya Bulyakashaju vitapewa kipaumbele.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, nakushuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Pamoja na ukweli kwamba Halmashauri za Wilaya ndio huteua vituo vya kufutilia na kufanya utekelezaji katika ukarabati wa vituo au zahanati katika maeneo yao; Mheshimiwa Waziri anakubalina kwamba milioni 198.8 alizozipeleka kwa zaidi ya vituo kumi, ni kidogo mno kwa kuweza kukarabati zahanati hizo alizozitaja hapa pamoja na kituo kile cha Izigo? Izigo kweanza, ni kituo cha afya na Bulyakashaju ni zahanati mpya, pesa hizi alizozisema ni za ukarabati, anakubaliana na mimi kwamba pesa hizo hazilengi kujenga wala hazilengi kupanua maeneo. Kwa hali hiyo nataka kumwomba, anaishauri vipi Serikali yake iweze kujenga pesa za ujenzi na za kupanua maeneo, si kukarabati?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA:** Mheshimiwa Spika, kama alivyosema mwenyewe, amesema kwamba shilingi milioni 198 ni ndogo, lakini lengo la Serikali ni kukarabati angalau asilimia 25 ya zahanati na vituo vya afya katika nchi nzima. Kwa hiyo, fedha hizi zimetawanywa katika Halmashauri mbali mbali ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Muleba. Lakini niseme kwamba, kwa zahanati kukarabati kwa shilingi milioni 14 pamoja na nguvu za wananchi, mimi nina uhakika kwamba fedha hizo zinaweza kutosha kwa ukarabati wa zahanati. Na kwa upande wa vituo vya afya, zinatengwa shilingi milioni 52 kwa kila kituo cha afya.

Kama kweli Halmashauri imedhamiria kufanya upanuzi pamoja na ukarabati, inaweza kufanya hivyo, kwa sababu kuna baadhi ya Halmashauri pamoja na kwamba tumewaambia kwamba wakarabati, lakini kwa jitihada zao wenyewe na kwa nguvu za wananchi, wamepanua pamoja na kufanya ukarabati. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge angalie vizuri kwenye Halmashauri na watu ili waweze kufanya upanuzi pamoja na ukarabati katika vituo hivyo. Fedha hizi milioni 52 kwa kituo cha afya, zikisimamiwa vizuri, nina uhakika kwamba zinaweza zikafanya kitu kizuri zaidi.

## **Makazi Bora Vijijini**

### **MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA aliuliza:-**

Kwa kuwa Serikali imetekeleza vizuri sana miradi ya elimu ya njia ya MMEM na MMES kwa kuunga mkono nguvu za wananchi katika ujenzi wa madarasa na kuboresha elimu:-

(a) Je, ni miradi gani ya aina hiyo inatekelezwa katika sekta ya makazi ili kusaidia wananchi wengi hususan vijijini wawe na nyumba bora ili kuboresha makazi?

(b) Kwa kuwa miaka iliyopita Mkoa wa Ruvuma uliongoza kwa kuwa na vijiji vyenye makazi bora. Je, Serikali ipo tayari kuendeleza miradi hiyo kwa Mkoa wa Ruvuma na Mikoa mingine kwa kushirikiana na wananchi?

(c) Je, Serikali iko tayari kuanzisha mashindano ya makazi bora vijijini ili kuleta ari kwa wananchi kujenga nyumba bora vijijini?

### **WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Devota Likokola, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inatekeleza miradi mbali mbali ya sekta ya makazi ili kuwawezesha wananchi waishi kwenye nyumba bora. Miradi hiyo ni pamaja na miradi inayotekeliza na Shirika la Nyumba la Taifa, Wakala wa Majengo, Usambazaji wa teknolojia rahisi ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu n.k. Aidha, kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 inaelekeza kuwa, jukumu la kuboresha makazi hususan vijijini linahusisha wadau wengi ikiwemo Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Asasi zisizo za Kiserikali (*NGOs* na *CBOs*) na wananchi wenyewe. Serikali kwa upande wake imeanzisha Wakala wa Utafiti wa Ujenzi wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (*National Housing and Building Research Agency*) kwa lengo la kutafiti, kukuza, kushauri na kusambaza matokeo ya utafiti wa vifaa vya ujenzi. Pia, Wakala unajenga nyumba za mfano kama zilivyojengwa Wilaya mbali mbali zikiwemo Wilaya ya Mwanga, Kongwa, Ileje, Karagwe, Bagamoyo, Kinondoni, Namtumbo Mkoani Ruvuma na kadhalika. Matumaini yetu ni kwamba wananchi wengi hasa vijijini wataiga mifano hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, nawapongeza wakazi wa Mkoa wa Ruvuma kwa hatua nzuri waliiyofikia ya kuboresha makazi yao. Zaidi ya asilimia 60 ya nyumba za Mkoa wa Ruvuma zimejengwa kwa kutumia matofali ya kuchoma na imara. Tatizo linalowakabili wananchi hawa katika ujenzi wa nyumba zao ni ubora wa vifaa vya kuezekeea, ambapo kwa sasa wengi wao wanatumia nyasi. Serikali kuitia Wakala wake *wa Utafiti wa Ujenzi wa Nyumba Bora* imeanza kutoa mafunzo katika vikundi kwa ajili ya kutengeneza vigae vya gharama nafuu kwa ajili ya kuezekeea. Mafunzo kwa ajili ya uzalishaji wa vigae

na teknolojia rahisi za ujenzi Mkoani Ruvuma yamefanyika katika Wilaya ya Namtumbo. Pia, kimeanzishwa kikundi cha ufundi kijiji Msindo katika Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Halmashauri za Miji na Wilaya kuwahamasisha wananchi kuwa na nyumba bora. Wakala uko tayari kutoa mafunzo na kusaidia uanzishaji wa vikundi nya kuzalisha matofali bora, vifaa nya kuezekea na vifaa vingine nya ujenzi katika Halmashauri pale utakapohitajika.

(c) Mheshimiwa Spika, ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Mbunge kuhusu kuanzishwa kwa mashindano ya ujenzi wa makazi bora vijijini ni mzuri na Serikali itaufanya kazi.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, asante! Nashukuru pia kwa majibu mazuri ambayo Wizara imeyatoa. Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili: Swali la kwanza, kwa kuwa wananchi wengi wanapenda kujenga nyumba nzuri na makazi bora, lakini wanakosa pesa za kujengea nyumba. Je, Serikali ipo tayari kuanzisha Benki ya Nyumba ili wananchi wengi waweze kukopa na kuejnga nyumba nzuri?

Swali la pili; kwa kuwa nyumba nyingi hapa nchini Tanzania zinamilikiwa na wanaume na wanawake wengi hawamiliki nyumba; Serikali ipo tayari kutoa motisha maalum kwa wanawake ili waweze kujenga na kumuliki nyumba nchini Tanzania?

**SPIKA:** Majibu, Mheshimiwa Waziri! Sijui motisha itolewe na Serikali au itolewe na wanaume! (*Kicheko*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la kwanza, ni kweli kujenga nyumba ni gharama na wananchi walio wengi hiyo gharama hawawezi.

Kwa kuzingatia hali hiyo, Serikali ina mpango wa kuanzisha sheria ambayo itaunda vyombo na utaratibu wa wananchi kuwezesha kukopa ili kujenga au kununua nyumba. Sheria hiyo ambayo inaitwa *mortgage finance* ilikuwa iletwe katika Bunge hili, lakini maandalizi yake hayajakamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, Bunge lijalo la Bajeti kwa sababu ya umuhimu na udharura na ucharaka wa suala hili, Serikali itaomba ilete katika Bunge lijalo ili sheria itungwe na vyombo viwepo, wananchi wakope.

La pili; kwamba wanawake hawamiliki nyumba. Sina hakika kweli kama Tanzania tunao taratibu wa kuwapiga marufuku wanawake wasimiliki nyumba! Wako wanawake, wacha nyumba, sasa hivi sheria yetu na sera yetu inaruhusu kwanza wamiliki ardhi kwa sababu nyumba lazima ikae katika ardhi.

Sheria inaruhusu wanawake wamiliki ardhi na vile wamiliki nyumba. Na kwa sababu unakuja sasa utaratibu wa mikopo ya kujenga nyumba, wanawake vile vile watapata fursa ya kukopa katika benki hizi ili nao wajenge nyumba. (*Makofi*)

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana! Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ni kweli hali ya kujenga nyumba bora hasa za matofali ya kuchoma katika Mkoa wa Ruvuma ni nzuri kama alivyosema Mheshimiwa Waziri ni zaidi ya asilimia 60; na kwa kuwa vifaa vya kuezekeea kama batii ni ghali sana ndiyo maana wanaezekeea nyasi, na utaratibu wakutengeneza hii teknolojia ya kuezekeea kwa vigae hunaenda taratibu sana. Je, Serikali inaweza kuweka utaratibu wa makusudi kabisa wa kuwadhamini wakulima vijijini ambao wanawenza kulipa mkopo wa batii usiozidi 40 kuweza ku-speed up maisha bora kwa Mtanzania?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kama nilivyosema mwanzoni kwamba ujenzi wa nyumba ni ghali na vifaa vya kuezekeea ni ahali. Sasa Serikali inafanya mambo mawili. Kwanza, kuna ule Wakala wa Utafiti wa Ujenzi wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi.

Halmashauri yoyote ambayo inataka huduma ya Wakala hawa, wanawenza wakaleta maombi, wakaenda hawa kuwfundisha vijijini wananchi jinsi ya kutengeneza vigae vya gharama nafuu kama walivyofanya katika zile Wilaya ambazo nilizitaja. Hiyo fursa ipo na kwa bahati nzuri kule Namtumbo hiyo shughuli imeishaanza na tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge ili tuongeze kasi kwa sababu utaratibu ule kule Namtumbo umekwishaanza kufundisha wananchi kutengeneza vigae kwa gharama nafuu kabisa. La pili kuhusu wakulima wadhaminiwe kununua batii.

Kama nilivyosema mwanzoni, utaratibu unakuja wa mikopo ya nyumba. Mikopo hii inahusu watu wa mijini na vijijini. Sasa vijijini ili waweze kukopa, ni vizuri wajipange na wajiunge katika Ushirika ili ushirika ule umdhamini aweze kukopa vifaa vya kujengea hapo mikopo itakapoanza mapema mwakani. (*Makofi*)

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana! Naomba kuuliza swali moja tu la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kuuza nyumba za *National Housing* ambazo ni kongwe ambazo ziko pale. Kwa mfano nyumba za Upanga ambazo wananchi wanakaa?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nyumba za *National Housing* zile ambazo ni chakavu sasa hivi haziuzwi, badala yake zinabomolewa na zinajengwa kubwa zaidi za kisasa zaidi ambazo zitahudumia watu wengi zaidi.

### **Kupanda kwa Bei za Umeme Nchini**

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN NGWILIZI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Taifa letu linayo gesi asilia ya Songo Songo na *Mnazi Bay* na pia kuna umeme unaozalishwa kutokana na nguvu za maji (Mtera, Kidatu, Nyumba ya Mungu na kadhalika) na kwa kuwa vyote hivi ni sehemu ya rasilimali za taifa;

Je, kwa nini bei za umeme zinazidi kupanda badala ya wananchi kufaidika na rasilimali zilizopo nchini.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Athuman Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mhehimiwa Spika, uzalishaji wetu wa umeme kwa kutumia vyanzo vya maji ni megawati 555 wakati uwezo uliopo unakadiriwa kufikia zaidi ya Megawati 4700 iwapo vyanzo vyote vya kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu za maji vitaendelezwa na kutumika kikamilifu. Uzalishaji wa umeme kwa kutumia chanzo cha gesi ya SongoSongo ni megawati 328, wakati uwezo unaoweza kufikiwa ni 437, baada ya kupanua Miundombinu ya kusafirisha gesi iliyopo songosongo. Aidha, uzalishaji wa umeme kutokana na mitambo ya gesi ya *Artumas* ni Megawati 12 kwa sasa. Mipango ya *Artumas* ni kuzalisha MW 300 hadi MW 400 ambazo zitaingizwa kwenye gridi ya Taifa hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa umeme kutokana na gesi ya Mkuranga bado unafanyiwa kazi ili kujua kiasi cha umeme kinachowenza kuzalishwa na chanzo hicho. Uzalishaji wa umeme utakaozalishwa baada ya miradi ya Kiwira na Mchuchuma kukamilika ni Megawati 800, ingawa vituo hivyo vina uwezo wa kuzalisha kiasi cha MW 4000 kwa kutumia Makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya uwekezaji mdogo ambao haujapanuka ili kuongeza uzalishaji wa umeme nchini, ongezeko la mahitaji limekuwa kubwa kulinganisha na uzalishaji. Kwa kutumia vyanzo asilia kwa kiwango kikubwa zaidi ni dhahiri kuwa gharama za uzalishaji zingeshuka

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa umeme unaozalishwa kutokana na rasilimali za nchi yetu unatakiwa umfaidishe mwananchi licha ya gharama kubwa za uzalishaji, *TANESCO* wamekuwa wakitoza bei ndogo ya umeme kulinganisha na gharama halisi za umeme ambazo kimahesabu hujumuisha gharama halisi za umeme ambazo kimahesabu hujumuisha gharama za uzalishaji *generation*, usafirishaji (*transmission*) usambazaji (*distribution*), uendeshaji (*operation*) na faida ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, hadi mwaka 2007 wastani wa gharama halisi za umeme tangu kuzalisha hadi kuufikisha kwa walaji hapa nchini ilikuwa shilingi 164 *kwa unit moja kwa kilo watt hour (kWh)*, wakati mteja alitozwa wastani wa shilingi 96 kwa *unit* moja. Kwa mantiki hiyo, *TANESCO* ilikuwa ikipata hasara ya wastani wa shilingi 68 kwa *kila unit* iliyoiuza kwa mteja wake.

Mheshimiwa Spika, hasara iliyotokana na *TANESCO* kuuza umeme kwa bei pungufu ya gharama zake kati ya mwaka 2004 na 2007, ilikuwa kati ya shilingi bilioni 109 na shilingi bilioni 189 kila mwaka. Kwa miaka ya nyuma, Serikali ilikuwa ikiipatia *TANESCO* ruzuku kwa ajili ya kufidia tofauti kati ya bei ya kuuzia umeme na gharama halisi za umeme nchini.

Hata hivyo, kuanzia mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali imesitisha utoaji wa ruzuku kwa *TANESCO* na kuridhia kuwa bei za umeme ziwe zinarudisha gharama halisi za umeme. Yaani shirika lijiendeshe kibashara. Kutokana na hatua hii chanzo pekee cha mapato ya *TANESCO* ni uuzaji wa umeme

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* hufanya tathimini ya bei za umeme ili kupata bei zenyenye uwiano sawa na gharama halisi ya uzalishaji umeme, kwa kushirikisha wadau na kisha kuwasilisha maombi ya kuongeza bei kwa *EWURA*. Iwapo *EWURA* wakiridhia kwa kuzingatia uwiano wa gharama halisi za uzalishaji na bei ya mlaji. Basi bei mpya huanza kutumika, vinginevyo hukataliwa. Mategemeo yetu ni kuwa bei za umeme ambazo zitaendelea kutumika zitakubaliwa na pande zote zitatunufaisha wadau wote wa sekta ya umeme nchini.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN NGWILIZI:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi. Naomba nimwuulize Mheshimiwa Waziri maswali mawili madogo kama ifuatavyo:-

(1)Kwa vile Serikali inakusudia kuondoa ruzuku kwa *TANESCO* hii moja kwa moja inamaanisha kwamba bei ya umeme itazidi kupanda kuliko hii. Je, kwa nini kama Songo Songo mali ya *TPDC* shirika la Kitanzania ambalo linauza gesi kwa bei ndogo kwa Songas kwa nini Songas na *TANESCO* waendelee kutoza bei kubwa wakati gesi wanayouziwa ni bei ndogo?

(2) Kwa vile juzi tumejadili sheria Mpya ya umeme. Je, kulingana na sheria hiyo kama ikipata sahihi ya Mheshimiwa Rais Je, itawezekana kuwa na Mini *grid* katika nchi hii ambayo kwa wawekezaji wapya kama vile Artumas wanaweza sasa kuruhusiwa kutoza bei ya chini kuliko ile ambayo inatozwa na grid ya Taifa?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ngwilizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni sahihi kabisa kama alivyosema kwa usahihi Mheshimiwa Mbunge; gesi yote iliyopo hapa nchini ni mali ya Serikali na umiliki wake

unapitia shirika letu la tpdc, kuhusu ni kwa nini bei ya Songas na *TANESCO* inakuwa ni ya juu wakati wao wanauziwa kwa bei ya chini.

Mheshimiwa Spika, napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba uendelezaji wa matumizi ya gesi ambayo tumekuwa nayo nchini imetokana na uwekezaji uliopo.

Mheshimiwa Spika, katika mikataba ambayo imeingia na Serikali kupitia *TPDC* kuna għarama ambazo mwanzoni inabidi zifidiwe lakini kadri ambavyo tunaendelea itafikia mahala ambapo mwelekeo utabadilika na hatimaye Serikali itanza kupata mapato makubwa, lakini hilo pia litaonekana katika bei ambazo wao wawekezaji watakuwa wanaliuzia shirika la *TANESCO* ama Serikali na baadaye zinakwenda kwa mlaji.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine niseme tu kwamba kama ambavyo Taifa mnafahamu limearifiwa mara kadhaa hivi karibuni, Serikali inaendelea na juhud za kupitia hiyo mikataba na tunaamini kwamba baada ya hapo yapo ambayo tunawzea kuyabaini na kuyarekebisha kwa ajili ya manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalì la pili la nyongeza kwamba kwa sababu tupo kwenye mchakato wa kujadili sheria mpya na tunaomba iwe hivyo kama ambavyo Mheshimiwa Ngwilizi ameomba iwe Muswada huu upite. Ni kweli kwamba Muswada huu ukipita sheria hii itakuwa imefungua wingi na upana wa ushiriki wa sekta binafsi na katika hilo yapo mambo mengi ambayo yanawezekana ikiwa mojawapo ni hilo la kuwa na *minigrid*, lakini niseme tu kwamba kwa sababu utaratibu mzima unawekwa kwenye sheria ni jambo la kusubiri tuone kitakachoendelea lakini tunaomba sana muswada huu upite halafu mambo mengine kama hilo alilosema Mheshimiwa Mbunge yatekelezze kwa utaratibu ambao sheria imeelekeza.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kuwa swalì la msingi linahusu bei za umeme nchini, na kwa kuwa pale Ludewa Mjini kuna mradi ambao unaendeshwa na *TANESCO* wa kuleta umeme katika Mji wa Ludewa na Vijiji vinavyozunguka, na kwa kuwa jenereta iliyofungwa sasa hivi ni mali ya wananchi siyo ya Serikali hadi hapo Serikali itakapoleta jenereta yake ambayo najua imeagiza na ninajua Mheshimiwa Waziri anajua. Je, bei ya umeme tukianza kupata pale Ludewa itakuwa ya chini kuliko bei ilivyo sasa hivi ya *TANESCO* kwa kuwa jenereta siyo mali ya Serikali?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalì la Mheshimiwa Prof. Mwalyosi la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kweli kama alivyosema Serikali inaendelea na utaratibu wa kupata jenereta pale na kweli Mheshimiwa Mbunge tumekuwa naye mara nyingi tu lakini niseme tu kwamba mara Jenereta ya Serikali itakapofungwa pale masuala ya bei kama ambavyo tunafahamu yanasmamiwa na Mdhibit Mkuu katika sekta hii ya maji na Nishati *EWURA*. Kwa hivyo mambo yote yatazingatia taratibu na vigezo ambavyo vimeainishwa kwa mujibu wa sheria yetu ya *EWURA*, lakini niseme tu kwama ni nia ya Serikali

kuhakikisha kwamba kila wakati bei zinakuwa za unafuu na kuzingatia gharama za uwekezaji.

**MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH:** Nashukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Katika kupunguza gharama za gesi ili tupate umeme nafuu, naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri huko *Songas* kuna *Pan African Energy* ambayo ni *broker* wa *Songas* na kwamba anasimamia hata upandaji wa bei ya gesi. Hivi *Pan African Energy* haiwezi ikaendeshwa na wataalamu wa *TPDC* badala ya kuwa ni mzigo wa kuagiza *Brokers* kutoka nje?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba inawezekana kabisa kwamba tungeweza kutumia wataalamu wa Tanzania badala ya kutumia *broker* ambaye kimakubaliano ametokana na makubaliano hasa ya *Songas* nay eye, lakini niseme jambo hili ni la kimakubaliano ya kimkataba, na kwa sababu hiyo fursa ya kiuwekezaji ipo na katika shughuli yote ndiyo maana imejitokeza kwamba *Pan African Energy* ndiyo ambayo sasa hivi ni *broker* kwa yule ambaye alimu-*engage*. Cha msingi hasa ni kuangalia kwamba matokeo ya kuwepo huyu kuna athari gani kwa masuala ya huduma kwa nishati ama umeme kwa nchi yetu, juhudhi zinaendelea mojawapo ikiwa tunahakikisha kwamba tunatumia gesi zaidi kwenye mitambo iliyopo badala ya kutumia mafuta ambayo kimsingi yana gharama kubwa. Lakini pia tunazingatia uwezo wa gesi inayozalishwa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo napenda kumhakikishia Taifa na Mheshimiwa Mbunge kwamba juhudhi zinaendelea kuona ni jinsi gani tunaweza kufanya ili kunufaika lakini pia watumiaji wapate huduma iliyobora na kwa viwango ambavyo vina nafuu zaidi.

**MHE. FATMA ABDALLAH MIKIDADI:** Kwa kuwa Tanzania kuna umeme asilia ambao uliana zamani sana kwa maana ya *Mnazi Bay* uligunduliwa tangu mwaka 1982 na *SongoSongo* uligunduliwa tangu mwaka 1974. Kwa nini kulikuwa na kipengele cha suala la Umeme wa dharura, kwa sababu kipengele cha suala la umeme wa dharura ndiyo chanzo cha mikataba feki na mibovu. Kwa mfano mikataba ya *RICHMOND* na *DOWANS, IPTL* chanzo chake ni umeme wa dharura.

Je, Mheshimiwa Waziri utakaubaliana na mimi kwamba kipengele cha umeme wa dharura kinaleta mwanya wa mikataba mibovu? Kwa nini umeme asilia usitumike kuanza kufanya mpango maalum wa kuweza kuzalisha ememe nchini?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Fatma Mikidadi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba pengine si wakati muafaka kusema kipengele cha umeme wa dharura ndiyo kinaleta mikataba mibovu au la. Lakini labda cha msingi nielezee kwa nini tulikuwa na mitambo ya kukodi hasa ambayo tumeiita ni mitambo ambyo imekuwa ikitoa huduma wakati wa dharura.

Mheshimiwa Spika, sote tunakumbuka kwamba kuanzia mwaka 2003 - 2006 nchi yetu ilikumbwa na tatizo la mvua hatukupata maji ya kutosha na kwa sababu chanzo chetu kikubwa ni maji, baada ya kupata hilo tatizo kufikia mwaka 2006 - 2005 hali yetu ilikuwa ni mbaya sana na kutokana na hali ilivyokuwa ingewezekana kabisa tukafikia mahali ambapo mfumo wetu wa usafirishaji ungeweza ku-collapse ndiyo maana kukawa na mpango wa kupata mitambo ya dharura kuja kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo niseme kwamba kuwepo na mitambo ya dharura kwa kipindi kile ilikuwa ni jambo ambalo haliepukiki.

Mfano mfumo wetu wa usafirishaji nchini umeshazidiwa kwa asilimia 10 na matokeo yake tunapoteza umeme mwangi na wataalamu wanatuambia ifikapo mwaka kesho mfumo wetu unawenza kuzidiwa kwa asilimia 33.7.

Mheshimiwa Spika, jambo hili linatuweka mahala ambapo kwa mazingira tuliyonayo sasa, ni lazima tutumie mitambo ya dharura iliyopo kwa sababu uwezekano wa kuendeleza vyanzo vilivyopo vya uhakika zaidi kama rasilimali ya chanzo cha maji si mpango wa muda mfupi. Ni mpango wa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye swalii la msingi tunarasilimali ambazo tunaweza kuzalisha mpaka megawati 4700 lakini kwa sasa hivi ni mipango ambayo hatuwezi kuifanya kesho na kesho kutwa, mahitaji yanaongezeka, mipango ya uchumi inaenda vizuri matokeo yake ni kwamba kadri umeme unavyoongezeka ndiyo umeme unavyoongezeka lakini uwezo wa rasilimali unakuwa hauendani na mfumuko huo.

Mheshimiwa Spika, naomba mheshimiwa Mbunge aamini kwamba ule mpango ulikuwa ni kwa maslahi ya Taifa, lakini kama nilivyosema kwa hiyo mikataba ambayo ipo Serikali itaendelea kuipitia kuona kama kulikuwa na udhaifu mahala turekebishe.

Na. 123

#### **Mashine za Kufulia umeme – Mafia**

**MHE. ABDULKARIM ESMAIL HASSAN SHAH** aliuliza:-

Kwa kuwa hali ya mashine mbili za kufulia umeme kwenye Wilaya ya Mafia zenye uwezo wa kuzalisha kilowati 425 kila moja ni chakavu sana na kwa kuwa mashine

hizo zimeshapitisha zaidi ya miaka kumi hivyo uzalishaji wake umwakuwa mdogo sana kiasi cha kusababisha mgao mkubwa wa umeme au kukosekana kwa umeme kabisa. Wilaya ya Mafia inakua kwa kasi sana na kwa sasa inahitaji mashine zenye uwezo wa kuzalisha megawati 4.

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta mashine mpya zenye uwezo wa kuzalisha hizi megawati?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani mwengine wa kusambaza umeme katika vijiji vya Wilaya ya Mafia?
- (c) Je, ule mpango wa uzalishaji umeme kwa kutumia mzunguko wa upopo (*wind mill*) bado upo?

#### **WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Shah, Mbunge wa Mafia, naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kuwa suala la upatikanaji wa umeme wa Mafia ni suala linalohitaji kupewa kipaumbele haswa ikizingatiwa kuwa Mafia ina mwelekeo mkubwa wa uwekezaji wa utalii (*potential tourist destination*). Aidha, miradi ya ujenzi wa uwanja wa ndege na bandari itakapokamilika inatarajiwu kuwa uwekezaji kwenye maeneo ya kitalii na viwanda vya samaki utaongezeka sana na hivyo kuongeza sana mahitaji ya umeme. Kwa kuzingatia hayo, ni dhahiri kuwa lazima tuanze kufikiria na kupanga upatikanaji wa umeme mwangi zaidi wa uhakika na nafuu kwa Mafia.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Shah, Mbunge wa Mafia, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mahitaji ya umeme ya Mji wa Mafia ni megawati 1.1. Kwa sasa Mafia kuna mitambo miwili yenye uwezo sawa ambayo kwa pamoja huzalisha kilowati 848. Hivyo kuna upungufu wa kilowati 252. Ili kukabiliana na upungufu wa umeme Mafia, mitambo iliyoko Njombe yenye uwezo wa kuzalisha kilowati 630 ambayo kwa sasa haitumiki baada ya Mji wa Njombe kuunganishwa kwenye gridi ya Taifa itahamishiwa Mafia. Aidha, Serikali ina mpango wa kuikarabati mitambo iliyopo Mafia kwa awamu ili kuwa na uhakika kuwa itaendelea kuzalisha umeme bila kuharibika haribika kama inavyojiteza kwa sasa.

(b) Mheshimiwa Spika, usambazaji wa umeme katika Vijiji vya Mafisa kama ilivyo kwa vijiji vingine nchini utatekelezwa chini ya Wakala wa Nishati Vijijini ambayo imepewa majukumu ya kuhamasisha na kuwezesha sekta binafsi na za umma kutoa huduma za nishati bora kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii Vijijini. Mfuko

wa Nishati Vijijini utatumika kutoa ruzuku kwa wawekezaji wenye sifa watakaowekeza kwenye miradi ya Nishati Vijijini kwa ajili ya ushindani.

(c)Mheshimiwa Spika, mpango wa *TANESCO* wa kuzalisha umeme kwa kutumia mzunguko wa upepo (*wind mill*) bado upo. Kazi inayoendelea kufanyika sasa ni ya ukukusanyaji wa taarifa zinazohusiana na upatikanaji wa upepo na nguvu ya upepo kwa lengo la kuona iwapo umeme wa kutosha utaweza kuzalishwa kwa njia hiyo. Vifaa vya kujenga mnara wa kupima upepo vimeshawasili nchini. Gharama ya ufungaji wa vifaa vya mnara huo ni shilingi milioni 28. *TANESCO* imeomba Wizara kutenga fedha ili kukamilisha ufungaji wa mnara wa kupima upepo. Wizara inakamilisha mpango wa kupata fedha kwa ajili ya ufungaji wa vifaa hivyo.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Ahsante, samahani sana Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wakati uliopo ni mdogo na Mheshimiwa Waziri amesema kwamba umeme unaozalishwa Mafia ni kilowati 800 na mimi nimeandika kwenye karatasi yangu tunahitaji megawati 4 kwa sababu tuna viwanda vya usindikaji ambavyo vyenyewe peke yake vinatumia umeme zaidi ya megawati moja na nusu au moja na kilowati 800. Kwa kuondoa utata huu, je mheshimiwa Waziri atakuwa tayari baada ya kikao hiki cha Bunge kumalizika, yuko tayari kufanya ziara Mafia na kuweza kwenda kuona hali halisi ya umeme katika Wilaya ya Mafia na shida tunazopata tukiwa kisiwani na adha inayotupata na hata kufikia umauti unatufika pale tunapokosa huduma hii muhimu kwa jamii? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Shah kwamba ni kweli Mheshimiwa Spika, ninakubali mimi na Wizara yangu tuko tayari kushirikiana naye tutakwenda kujiridhisha na kile kinachoendelea ili kujiridhisha na kinachoendelea ili kuboresha huduma ya umeme Wilayani Mafia.

Na. 124

#### **Huduma ya Maji - Kineng'ene - Lindi.**

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, maji ni uhai wa mwanadamu na kwa kuwa wananchi wa eneo la Kineng'ene Mkoani Lindi wanakunywa maji yasiyo salama lakini bado wanafuata umbali wa km 8:-

Je, ni lini wananchi hao watapelekewa maji safi na salama ili kunusuru afya zao na kuwaondolea usumbufu mkubwa wanaopata kuendea maji hayo umbali mkubwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika Mbunge wa Viti maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Kineng'ene kinachoundwa na vitongoji vya Mchochoro, Mmukule na Nanembo kiko nje kidogo ya Mji wa Lindi. Kwa bahati mbaya uchunguzi wa maji chini ya ardhi uliofanywa mwaka 2006 ulionyesha kutokuwapo na maji katika kijiji cha Kineng'ene.

Serikali iliendeleza uchunguzi katika maeneo mengine jirani na hatimaye maji yakapatikana karibu na kijiji cha Chikonji, kilomita nane kutoka Kineng'ene. Mwaka 2006, Serikali kwa msaada wa Serikali ya Japan kuptitia Shirika la *JICA* ilichimba kisima na kujenga tanki la maji katika kijiji cha Chikonji. Tatizo lililojitokeza ni kwamba kulingana na masharti ya wafadhili *JICA*, wasingeweza kupeleka maji zaidi ya mita 600 Kineng'ene kutokana na umbali mrefu wanaotakiwa kusafiri kufuata maji. Tatizo jingine jipya ni kwamba kisima hicho hivi sasa kimekauka.

Mheshimiwa Spika, Serikali bado inaendelea kutafuta chanzo kingine cha maji kwa ajili ya Kineng'ene. Aidha, tayari shilingi milioni 36 zimetengwa kuptitia *TASAF* kwa ajili ya uendelezaji wa mradi wa Kineng'ene lakini kazi ya kulaza mabomba iliyokuwa ikifanywa na wananchi sasa imesitishwa hadi hapo chanzo kipyta kitakachopatikana. Wizara yangu sasa kwa kushirikiana na wakala wa Serikali wa kuchimba Visima (*DDCA*), Mamlaka ya Maji Lindi na Halmashauri ya Mji wa Lindi inatafuta chanzo kingine cha maji ili mchangano wa nguvu za wananchi na *TASAF* uunganishwe na mchangano wa Serikali kutekeleza mradi huo. Aidha, napenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba kijiji cha Chikonji ambapo kisima chake kimepata matatizo kimo katika vijiji 10 vya Mradi wa maji na usafiri wa mazingira Vijijini. Pamoja na kwamba mradi huu unatarajia kukoma mwezi juni 2008 mradi wa Chikonji utatekelezwa moja kwa moja na programu ya kuendeleza sekta ya maji katika mwaka wa 2008/2009

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika pamoja na majibu mazuri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Lindi vyanzo vyake vingi vya maji ni vya maji chumvi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuunganisha mabomba yake kutoka Chitopa na Rutanda ambako kuna maji mengi safi na salama?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama nilivyosema tunaendelea kutafuta vyanzo vingine vya maji na kwa vile kuna tatizo hili la chumvi. Lindi na sehemu nyingi za maeneo hayo, basi tutaendelea kufanya uchunguzi na tuangalie kama hivyo vyanzo anavyovitaja Mheshimiwa Mbunge vitaonekana ndivyo vinafaa basi tutajitahidi kuvichunguza. Lakini naomba niseme tu kwamba wakati mwingine vyanzo vinapatikana mbali sana kiasi kwamba gharama za utekelezaji na uendeshaji zinakuwa kubwa. Hata hivyo tutakachoweka mbele ni maslahi ya wanavijiji na si gharama kama hakuna njia nyingine.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hivi karibuni na mimi nilipata nafasi ya kutembelea vijiji vya Kineng'ene, Chikonji, mionganoni mwa malalamiko ya wananchi ni kwamba maji wanayotumia hayafai kabisa kwa matumizi ya binadamu, na wakanipa hata sampuli nimletee Mheshimiwa Waziri hapa aone. Je, Serikali iko tayari kupeleka timu ya wataalam ili iangalie afya za wananchi hao ili ikiwezekana iwasaide matibabu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Kwanza, katika majibu yangu ya swali la msingi nimeelezea jinsi tulivyojipanga, Wizara, *DDCA*, Halmashauri ya Lindi kuendelea kutafuta vyanzo vipyta vya maji, kuhusu wataalamu wa afya kuenda kukagua hali za afya za wananchi wale nadhani kama nimemwelewa Mheshimiwa Mbunge ndiyo ilikuwa ombi lake kwamba *commitment* hii ifanywe na Wizara ya Afya.

Na. 125

#### **Wananchi wa Kigoma Vijijini kupatiwa Maji Safi**

**MHE. SIJAPATA FADHILI NKAYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi waishio wilaya ya Kigoma Vijijini, Kijiji cha Nkungwe wanatumia maji kutoka mto Luiche ambapo wakati wa masika maji hayo huwa machafu kwa kuchanganyika na mizoga ya wanyama pamoja na maiti za binadamu; na kwa kuwa wananchi hao hawana kimbilio lingine bali kuyatumia maji hayo:-

(a) Kwa kuwa, maji hayo siyo salama kwa matumizi ya watu. Je, Serikali haioni kuwa ni vema kuwaweka katika mpango wa kupata maji kutoka katika chanzo cha maji Mkongoro?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kunywa maji hayo machafu ni hatari kwa afya na kwamba inaonekana hawawajali wananchi wake?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba Serikali haiwajali wananchi wake ndiyo maana Serikali kwa kushirikisha wananchi na wadau wengine inabuni miradi na

programu za kuendeleza sekta ya maji kwa kuzingatia maelekezo ya ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ibara ya 67(a) inayosomeka kama ifuatavyo:-

Kutokana na umuhimu wa maji, Serikali chini ya CCM katika kipindi cha mwaka 2005 - 2010 itaendelea kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika sera ya Taifa ya maji ya mwaka 2002 na kusisitiza yafuatayo.

Kuwawezesha wananchi Mijini na Vijiji kupata maji safi salama na ya kutosha kwa matumizi yao ya kawaida karibu na sehemu wanazoishi na kwa mahitaji ya kiuchumi. Lengo ni kuwafikishia huduma hiyo asilimia 90 ya wakazi wa Mijini na asilimia 65 ya wakazi wa Vijiji ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji ya mtiririko wa Mkongoro 11 unaotekelizwa kwa ushirikiano kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma na Shirika la *Ingeneria Sin Fronteras* (Wahandisi wasio na mipaka) umepangwa kuhudumia vijiji sita ambavyo ni Mahembe, Chankabwimba, Msimba, Kamara, Simbo na Kasuku. Chanzo cha cha mto Kaseke, kijiji cha Nkungwe hakijajumuishwa katika mradi huo kwa sababu chanzo cha mto Kaseke kipo bondeni. Kwa kuwa mradi wa Mkongoro 11 ulibuniwa kuwa ni wa maji ya mtiririko (*Gravity Scheme*), maji hayawezi kutiririka kufika kijiji Nkungwe kwa kuwa kijiji hicho kipo katika ukanda wa juu.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha wananchi wa kijiji cha Nkungwe kupata maji safi na salama, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma Vijiji imepanga kuanza na kukamilisha usanifu wa mradi wa maji katika kijiji cha Nkungwe katika mwaka wa 2008/2009.

Mchakato wa kupata wataalamu washauri watakaosaidia Halmashauri ya Wilaya kusanifu na kusimamia utekelezaji wa mradi unaendelea.

Tunatarajia kuwa wataalam hao watapatikana mwezi Julai 2008. Wataalam hao watafanya uchunguzi kuhusu vyanzo vya maji na kutoa mapendekezo ya mradi utakaojengwa katika kijiji cha Nkungwe.

Hivyo wakati Serikali inafanya juhudu kuboresha upatikanaji wa maji safi na salama wananchi wote pamoja na wale wa Nkungwe wanashauriwa kuchemsha maji yao kama njia rahisi ya kuyatibu ili kuepukana na milipuko ya magonjwa yanayosababishwa na maji machafu.

**MHE. SIJAPATA FADHILI NKAYAMBA:** Kwa kuwa katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuwa wananchi hawa watapata maji kutokana na chanzo cha Mto Kaseke na akasema kuwa mradi huo utafanyiwa utafiti kuanzia 2008/2009. Tunataka tujue itakuwa ni mwezi gani? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie ndugu yangu Mheshimiwa Nkayamba kwamba suala la mchakato lilipitia vikwazo vingi. Mimi naomba aamini kwamba utaratibu huu upo na mimi aeewe kwamba ni mdau. Lakini kusema ni mwezi fulani nitakuwa nataka labda nimdanganye kwamba mwezi fulani tayari mnapata maji kwa sababu mchakato unaanza halafu tutaanza sasa utaratibu wa kupeleka fedha. Lakini nimhakikishie kwamba katika mwaka 2008/2009 mradi huu utaanza kushughulikiwa.

Na. 126

### **Ujenzi wa soko la Kimataifa Makambako**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeamua kujenga soko la kimataifa pale Makambako:-

- (a) Je, maandalizi ya ujenzi wa soko hilo umefikia hatua gani sasa?
- (b) Je, ni lini ujenzi utaanza na ni eneo la ukubwa gani linahitajika?
- (c) Je, wakazi wa Makambako wafanye nini zaidi ili kuongeza kasi ya ujenzi wa soko hilo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kuwezesha ujenzi wa soko la kimataifa katika mji mdogo wa Makambako, Wizara imeajiri Mshauri Mwelekezi wa kufanya upembezi yakinifu (*feasibility study*) ili kuainisha kwa kina faida na mahitaji ya ujenzi wa soko hilo. Taarifa ya awali imewasilishwa Wizarani na uchambuzi unafanyika na pia maandalizi ya mkutano wa wadau yanafanyika ili kupata maoni kutoka kwa wadau wengi.

(b) Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya awali ya utafiti huu yanaonyesha kuwa ukubwa wa eneo litakalohitajika katika ujenzi wa soko hili ni mita za mraba 10,732. Eneo la wazi linakadirwa kuwa mita za mraba 2,470 na eneo la majengo ni mita za mraba 8,262. Ujenzi wa soko utaanza mara baada ya ripoti ya upembezi yakinifu kukamilika na Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kupata fedha za ujenzi.

(c) Mheshimiwa Spika, mradi huu wa ujenzi wa soko utakwenda kwa kasi pale ambapo wananchi watahamasishwa kushiriki kuchangia kikamilifu gharama za ujenzi wa masoko. Michango ya wananchi ni pamoa na kutenga eneo la ujenzi ambalo ni tayari,

kushiriki kikamilifu katika kutafuta wadau wa Maendeleo watakaoshiriki katika ujenzi na kuchangia nguvu kazi.

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, kwa vile program hii vile inahusu ujenzi wa soko la kimataifa pale Segera Wilaya ya Handeni na kwa kuwa tulikwishaiezwa kwamba tunasubiri shughuli za mshauri mwelekezi na matokeo ya utafiti huo na kipindi kilichopita sasa ni karibu miaka miwili sasa. Je, anaweza kutueleza kwa maendeleo ya soko la Segera vile ambalo ni la kimataifa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mradi huu wa ujenzi wa masoko ya kimataifa katika eneo la Makambako linakwenda sambamba na ule wa eneo la Segera katika Wilaya ya Handeni. Kama nilivyotoa maelezo hapa mpango huu masoko yote mawili mshauri mwelekezi aliteuliwa pamoja na ripoti iliwasilishwa Wizarani wakati mmoja. Niseme tu kwamba ripoti hii kwa kumbukumbu zangu iliwasilishwa mwezi Novemba, mwaka jana. Kwa hiyo, haijafikia miaka miwili kama anavyooleza Mheshimiwa Mbunge. Lakini nimpe matumaini tu kwamba hizi shughuli ambazo zinafanyika katika eneo la ujenzi wa soko la Makambako zinakwenda sambamba pamoja na zile za ujenzi wa Soko la Segera katika Wilaya ya Handeni.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa masuala haya ya ujenzi wa masoko ya kitaifa na mahitaji ya masoko hayo ni pamoja na hitaji kubwa la soko la kimataifa katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji eneo la Muhukulu, Kata ya Muhukulu kule Songea Vijijini, ambako sasa hivi daraja kubwa sana la kuunganisha Tanzania na Msumbiji linakaribia kukamilika kujengwa. Je, Mheshimiwa Waziri anasema nini kuhusu kusaidiana pia na Halmashauri ya Wilaya ya Songea kuhakikisha soko jingine la kimataifa la kwanza lijengwe katika Mkoa wa Ruvuma na maeneo ya Kusini kuliko ilivyo katika maeneo mengine ya nchi hii?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nipongeze juhudzi za Mheshimiwa Mbunge, kwa kuona umuhimu wa kujenga soko hili katika eneo hilo la mpakani.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba katika maandalizi ya ujenzi wa masoko ya aina hii, pamoja na aina nyingine Serikali tunachohimiza na kuomba wenzetu kule Wilayani kuibua miradi hii na kuiwekea katika mipango yao na hatimaye wakishirikiana na Serikali kuweza kutafuta wadau wa maendeleo ambao watashirikiana katika ujenzi wa masoko haya.

Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge waanze kule Wilayani kuibua mradi huu. Sina shaka Wizara itaunga mkono katika kutafuta wadau wa maendeleo.

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kikwete, aliahidi kuititia Ilani ya Uchaguzi ya CCM kuwa atafufua Viwanda ndani ya Jiji la Mbeya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha hilo linatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson M. Mpresa, Mbunge wa Mbeya Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa na Serikali kuhakikisha ufuluaji viwanda katika Jiji la Mbeya kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais Kikwete, ni hizi zifuatavyo:-

Kwanza, kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuvutia wawekezaji toka ndani na nje kwa kubuni sera nzuri na kuimarisha miundombinu. Kutohana na haya viwanda vilivyofufuliwa Jijini Mbeya ni pamoja na *Afri Bottlers Ltd, Marmo E. Granito Mines (T) Ltd, SBC Tanzania Ltd, Malick's Refractory Bricks Co. Ltd* na Viwanda vyakula, kushona viatu, kukamua mafuta ya alizeti, kutengeneza matofali, useremala, kutengeneza vyakula vyamini vya mifugo, kutengeneza sabuni na kushona mavazi.

Aidha, viwanda vidogo vinaendelea kufufuliwa na vingine vipyta kuanzishwa kutohana na juhudzi za *shirika* la kuhudumia viwanda vidogo (*SIDO*) mkoani Mbeya. Viwanda hivyo ni pamoja na vile vya kutengeneza mashine na vipuri, kusindika vyakula, kushona viatu, kukamua mafuta ya alizeti, kutengeneza matofali, useremala, kutengeneza vyakula vyamini vya mifugo, kutengeneza sabuni na kushona mavazi.

Pili, Serikali inawahimiza wawekezaji walionunua viwanda vya zamani na ambavyo vina maslahi makubwa kwa Mkao wa Mbeya na Taifa, kwa ujumla kutokubadili aina ya uzalishaji ili kukidhi faida binafsi. Kwa mfano, Serikali imemhamasisha mwekezaji wa kiwanda cha zana za kilimo (ZZK) aliyekuwa ameng'oa mashine za mitambo hiyo kuukuu na kupeleka Dar es Salaam ili itumike kama malighafi kwenye kiwanda chake cha nondo kuwekeza na kukianza kiwancho hicho upya Mkoani Mbeya.

Viwanda vingine vya aina hii vilivyofufuliwa ni pamoja na kiwanda cha nguo (*Mbeya tex*), kiwanda cha saruji (*Mbeya Cement*) na kiwanda cha *Kiwira Coal Mine*.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na juhudzi za kuvutia wawekezaji waendelee kuwekeza katika Jiji la Mbeya Mkao wa Mbeya na Tanzania nzima kwa ujumla kwa kuendelea kuboresha zaidi mazingira ya uwekezaji na kubainisha fursa zilizopo katika sekta ya viwanda katika Mkao wa Mbeya.

Aidha, Serikali itaendelea kutatua matatizo yanayokwamisha uzalishaji hususan matatizo ya umeme, maji na miundombinu ili kuimarisha ufanisi katika viwanda vya Jiji la Mbeya na Mkoani Mbeya kwa ujumla.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa katika *mini tiger plan* 2020 Mbeya iliahidiwa kuanzishwa *Special Economic Zones* ifikapo mwaka 2008 amba ni mwaka huu. Katika mipango ya Serikali hilo halijajionyesha katika bajeti ya mwaka 2008/2009. Je, Serikali, haioni kwamba kuingiza mpango huu katika bajeti ya mwaka huu itakuwa ni kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kama alivyoahidi Rais katika ukurasa 59?

(b) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametaja viwanda kwamba vimefufuliwa atakubaliana na mimi kwamba viwanda alivyoitaja ni vile vilikuwepo kabla ya uchaguzi wa mwaka 2005 Rais alipopata ahadi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, la kwanza naomba nikubaliane naye Mheshimiwa Mbunge ya kwamba katika hii mipango ya *mini tiger* aliyoieleza na mimi nakubaliane naye kwamba mipango hiyo ipo lakini juhudzi za Serikali ninazozifahamu mimi kwenye Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ni kwamba tayari mipango ya kuainisha maeneo ya *Special Economic Zone* yalikuwa yameshaanzwa na Wizara na kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba baada ya zoezi hili kukamilika na kuainisha hayo maeneo bila shaka mipango hiyo itaanza kuingizwa kadri ambavyo Mheshimiwa Mbunge anashauri.

La pili, nakubaliana naye pia kwamba baadhi ya viwanda ambavyo nimevitaja katika jibu la msingi hapa vilikuwa viko tayari kipindi kile cha uchaguzi.

Lakini katika kuainisha shughuli ambazo zinaendelea sasa hivi nimekwisha kusema hapa kwamba Serikali inajitahidi kuboresha mazingira ili wawekezaji wa ndani na nje waweze wakashiriki katika hili na hapa nichukue nafasi hii kuwapongeza viongozi na wananchi wa Mkoa wa Mbeya kwa kuhamasika sasa hivi kuanzisha utaratibu wa kuanzisha kiwanda cha mbolea kule Mbeya kwa hiyo, Serikali itakuwa iko tayari kuwaunga mkono.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la msingi la kufufua viwanda vya ndani Mbeya linafanana kabisa na ufuluaji wa viwanda Mjini Moshi. Serikali ina mpango gani wa kufufua viwanda vya Moshi kama vile vya magunia na *Macintosh*?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, mipango ya Serikali katika ufuluaji wa viwanda vya kule Moshi kusema kweli inakwenda sawa kabisa na ile mipango niliyoieleza katika jibu langu la msingi.

Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba zile jitihada zinazofanywa katika kufufua viwanda vilivyoko Mbeya ni pamoja na viwanda vingine ambavyo viko hapa nchini. Suala zima la uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji pamoja na kuboresha miundombinu ambazo ndiyo jitihada zinazofanywa na Serikali hivi sasa. (*Makofî*)

Na. 128

### **Ufugaji Bora na wa Kisasa**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MHE. ROSEMARY KIRIGINI)** aliuliza:-

Kwa kuwa elimu na mafunzo ya ufugaji bora na wa kisasa kwa wataalam na wafugaji ni hitaji muhimu katika sekta ya mifugo na uvuvi kwani yanawawezesha kuimarisha mchakato wa matumizi ya teknolojia ya kisasa katika sekta hizo mbili:-

- (a) Je, Serikali ina utaratibu upi wa kuhakikisha kwamba, mbinu mpya za sayansi na teknolojia zinawafikia na kutumiwa na wadau wa sekta hizo?
- (b) Je, Serikali inaendesha Vyuo na Taasisi ngapi kwa lengo la kuwapata wataalam wa fani hizo mbili ni kukidhi mahitaji ya taifa letu?

### **NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalí la Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na wadau mbalimbali huendesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu kuhusu mbinu mpya za sayansi na teknolojia kwa wadau hao.

Mafunzo hayo hutolewa na wataalam wa ugani, jambo ambalo linasaidia kuufikisha utaalamu kwa wafugaji na wavuvi hao kwa haraka na kwa uhakika. Serikali ina jumla ya wataalam 2,581 wa ugani katika fani ya mifugo na 624 wa fani ya uvuvi katika Halmashauri zake.

Mafunzo hayo ya ugani hutolewa pia kupitia vyombo vya habari. Kwa mfano, kwa mwaka 2007/08, Wizara imetayarisha na kurusha vipindi 52 vyenye mada mbalimbali kuhusu ufugaji na uvuvi bora na wa kibiasara.

Vile vile Wizara yangu huandaa na kusambaza machapisho yanayohusu mbinu bora na za kisasa kuhusu ufugaji na uvuvi kama njia mojawapo ya kuwafikishia wadau hao teknolojia mpya.

Kwa mfano, katika mwaka 2007/2008 jumla ya vijitabu 1,974, vipeperushi 45,000 na mabango 30,000 yalitayarishwa na kusambazwa kwa wafugaji kote nchini.

Aidha, Serikali kupitia taasisi zake za utafiti, Vyuo Vikuu na wadau wengine hufanya tafiti shirikishi katika maeneo ya wafugaji na wavuvi na hivyo kuwapa uzoefu wa namna ya kutumia teknolojia mpya. Taasisi za utafiti za Wizara ni pamoja na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo ya Mpwapwa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI).

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine huandaa na kuratibu maonyesho ya siku zinazolenga wafugaji na wavuvi. Wadau hao hupata fursa ya kuona kwa vitendo matumizi ya sayansi na teknolojia mpya kutoka kwa wataalam na wafugaji na wavuvi wenzao. Siku hizo ni pamoja na Nane Nane, Siku ya Chakula Duniani, Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa, yaani Saba Saba na Wiki ya Maziwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara inasimamia vyuo vinane (8) vya mafunzo ya mifugo na uvuvi. Lengo la mafunzo hayo ni kupata wataalamu watarajali ambao wanawenza kukidhi mahitaji na matarajio ya wafugaji na wavuvi.

Kwa upande wa mifugo, vyuo hivyo vya mafunzo ni Tengeru (Arusha), Mpwapwa (Dodoma), Mabada (Songea), Buhuri (Tanga) Temeke (Dar es Salaam) na Morogoro. Vyuo hivi vina uwezo wa kutoa mafunzo kwa wanachuo 1,185 kwa sasa. Aidha, kwa upande wa uvuvi, vyuo hivyo ni Nyegezi (Mwanza) na Mbegani (Bagamoyo). Vyuo vya Uvuvi vina uwezo wa kuchukua wanafunzi 205.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali ninashukuru sana kwamba Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba kuna vyuo vinavyotoa elimu kwa ajili ya watalaam wa mifugo na uvuvi. Je, Serikali inaweza kuniambia sasa katika vyuo hivyo mnazingatia mafunzo ya kupambana na maradhi ya samaki? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, tunapotoa mafunzo ya samaki tunahakikisha kwamba tunazingatia ufugaji bora wa samaki na mojawapo ni kuwa na samaki ambao ni wazuri ambao ni wa kisasa na kuhakikisha kwamba wanapata chakula ambacho ni kizuri na kuzingatia kwamba vyovyote vile maradhi nayo yanadhibitiwa katika hali hiyo. Kwa hiyo, huwa tunatoa mafunzo hayo. Ahsante.

**Mfuko Maalum wa Kuwawezesha Wananchi**

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilitenga mfuko maalum kwa ajili ya kuwawezesha wananchi katika kupata maisha bora na kuondokana na umaskini maarufu kama mabilioni ya JK na kwa kuwa, tathmini imeonesha kuwa, wananchi wengi waishio vijiji hawajanufaika na mfuko huo:-

- (a) Je, ni kiasi gani cha fedha kilitengwa kwa ajili ya Wilaya ya Siha?
- (b) Je, vikundi vipi katika Wilaya hiyo vimenufaika na mfuko huo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Siha ni mionganii mwa Wilaya 22 ambazo hazikufanikiwa kupata mikopo kabisa katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Mpango wa utoaji mikopo kwa wajasiriamali iliyopitishwa katika Benki za *CRDB* na *NMB*. Katika Awamu ya pili ya mpango huu, Wilaya ya Siha imetengewa shilingi milioni 200 zitakazopeshwa kwa wajasiriamali kupitia Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro (*Kilimanjaro Cooperative Bank Ltd (KCB)*) ambayo imeteuliwa kutoa mikopo na kusimamia urejeshaji wa mikopo yote itakayochukuliwa. Benki hii tayari imekamilisha mchakato wa kuibua *SACCOS* zilizokidhi vigezo vya kukopeshwa na imepanga kuanza kutoa mikopo kuanzia mwezi huu wa Aprili, 2008.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Siha, haikufanikiwa katika awamu ya kwanza ya utoaji wa mikopo, idadi ya vikundi na wajasiriamali watakaonufaika na mfuko huo itajulikana baada ya utekelezaji wa awamu ya pili ya mpango kuanza kutekelezwa Wilayani Siha kama nilivyokwisha eleza.

(c) Mheshimiwa Spika, utaratibu utakaotumika katika utoaji mikopo hii ni kuwalenga wanufaika amba ni wajasiriamali mmoja mmoja, vikundi na *SACCOS*, Wajasiriamali na vikundi watawasilishwa maombi yao ya mikopo kupitia kamati za vijiji au mitaa, kata na hatimaye kwenye benki au asasi ya fedha husika. Kwa upande wa

SACCOS zitawasilisha maombi yao ya mikopo kuptitia Afisa Ushirika wa Wilaya na hatimaye kwenye benki au asasi ya fedha.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoo. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kwamba mwaka uliopita Wilaya ya Siha ni mionganoni mwa Wilaya 23 ambazo hazikupata kabisa chochote pale.

(a) Je, atakubaliana na mimi kwamba kutakuwa kuna haja ya kuipa Wilaya ya Siha *areas* kwa sababu haikupata mwaka jana kwa mujibu wa maelekezo ya Serikali?

(b) Kwa vile sasa tunaambiwa kwamba Wilaya ya Siha imetengewa shilingi milioni 200. Je, Wizara itakuwa tayari kutoa maelekezo katika Wilaya ya Siha na kama ikiwezekana watalaan wapelekwe kule ili kuwaelekeza vizuri namna ya kutumia sasa hizo shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuwaletaa maendeleo na manufaa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba kuna Wilaya kadhaa nchini ambazo hazikufikiwa na ule mpango wa awamu ya kwanza ikiwemo Wilaya ya Siha. Kwa hiyo, katika hili ndiyo maana tumeamua kipindi hiki kwamba zile Wilaya ambazo hazikufikiwa kabisa zitengewe kwa ujumla kwa kuanzia shilingi bilioni 2.29 ikiwemo na Wilaya ya Siha kupewa hiyo fursa ya kupata mikopo safari hii. Kwa zile Wilaya ambazo zilifikiwa kiasi hizo kwa safari hii zimepewa kiasi pungufu. Kwa hiyo, kwa aina kwa sababu uwezo wa Serikali ndiyo huo kwa kuwapa wale wengine pungufu na hizo Wilaya zingine ambazo hazikufikiwa kabisa kwa namna fulani inakuwa kama ni *compensation* kwa wale ambao hawakupata.

Lakini nataka nitoe wito hapa kwamba fedha hizi zikumbukwe kwamba ni kichocheo tu na kusema kweli ni fedha za mzunguko ambazo wale ambao wanakopa wanatakiwa warejeshe mapema ili fedha ziendelee kuzunguka mionganoni mwa wale waliokopopo.

Mheshimiwa Spika, la pili, la maelekezo nakubaliana naye kabisa Wizara yangu imeshaanza kutoa maelekezo na kusema kweli wakati mwininge ilikuwa ni kutoa mafunzo kwa wale wote ambao wanahusika katika ukopaji wa mikopo hii na nitoe wito kwamba wale wajasiriamali wote ambao wanaamua kwenda kukopa wasiamue kwenda kukopa tu bila kuwa na malengo. Ni lazima wawe na miradi ya kufanya shughuli ili wanapokopa mikopo hii iwalettee tija.

**SPIKA:** Mheshimiwa nakusudia angalau tumalize haya ya miundombinu haya mawili yanayofuata. Kwa hiyo, tunahamia Wizara hiyo. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Estherina Julio Kilasi, Mbunge wa Mbarali.

Na. 130

**Ujenzi wa Barabara ya Igawa – Rujewa – Madibira – Kinyanambo**

### **MHE. ESTHERINA J. KILASI aliuliza:-**

Kwa kuwa Serikali kupitia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 iliahidi kujenga barabara ya Igawa – Rujewa – Madibira – Kinyanambo yenyewe urefu wa kilometra 156 kwa kiwango cha lami na kwa kuwa Serikali kupitia mpango wa *AMSDP* iliamua kujenga barabara hiyo kwa urefu wa kilometra 71 kuanzia Rujewa mpaka Madibira kwa kiwango cha changarawe kwa gharama iliyokaribia shilingi bilioni 1.3.

Je, Serikali haionti kuwa ni vizuri matengenezo hayo ya kilometra 71 yangeenda sambamba na maandalizi ya ujenzi wa lami ili kupunguza gharama ya kuanza maandalizi mapya ya ujenzi?

### **NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Estherina Kilasi, nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza na kumshukuru Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Dr. Maua Daftari kwa kujibu maswali ambayo yalikuwa yameelekezwa kwenye Wizara yetu wiki iliyopita kwa umahiri mkubwa wakati mimi na Waziri wangu tulipokuwa tuna udhuru wa kutohudhuria Bungeni hapa.

Aidha, nimshukuru vile vile Mheshimiwa Celina Kombani kwa kujibu kwa umahiri maswali yetu. Nimshukuru pia Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, kwa kuwasilisha vizuri mikataba na itifaki ambazo ziliidhinishwa, zilipitiwa na Bunge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada shukrani hizo napenda kujibu sasa swalii la Mheshimiwa Estherina Julio Kilasi, Mbunge wa Jimbo la Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Igara – Rejewa – Madibira – Kinyanambo (km. 156) ni barabara ya Mkaoa inayohudumiwa na Wizara ya Miundombinu kupitia wakala wa Barabara Mkaoa wa Mbeya na Mkaoa wa Iringa. Barabara hiyo inaunganisha eneo la Madibira lenye mradi mkubwa wa kilimo cha mpunga na barabara kuu eneo la Kinyanambo katika Wilaya ya Mufindi na Igawa katika Wilaya ya Mufindi na Igawa katika Wilaya ya Mbarali.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, juu ya kuutumia mradi wa ukarabati wa kiwango cha changarawe unaoendelea hivi sasa kuanzia Rujewa hadi Madibira km 71 kupitia mradi wa *AMSDP*, kuwa sehemu ya maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara hiyo.

Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa baadhi ya maandalizi muhimu yanayolenga kupunguza gharama wakati wa ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami yamezingatiwa katika mradi huu unaoendelea.

Maandalizi hayo ni pamoja na kujenga madaraja na makalvati ya kudumu kwenye mwelekeo wa barabara iliyopimwa (*surveyed alignment*), kupanua barabara kulingana na

viwango vya barabara za lami za Mikoa na kujenga matabaka ya chini ya barabara yenye viwango vinavyokubalika.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana nina uhakika anajibu kwa uhakika kwa sababu ametembelea barabara hii na ameona athari zake. Tatizo langu la kuleta swali hili ni kwa sababu ya matumizi ya fedha nyingi ambazo zimekuwa zikitumika tangu mwaka 2000 mpaka sasa.

Nilipokuwa naleta swali hili fedha za *AMSDP* zilikuwa zimetolewa bilioni 1.3 bajeti hii zimetolewa bilioni 1.8 na barabara wakati wa mvua imekuwa haipitiki na makalvati yamekuwa yakiharibika.

(a)Je, Mheshimiwa Waziri, atakuwa tayari kukiwekea kipaumbele barabara hii hasa ukizingatia kwamba fedha nyingi sana zimetumika ili kuanza kwanza kutengeneza madaraja na baadaye utaratibu mwingine wa kutengeneza barabara ufuate.

(b)Ningependa kujuwa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu yeye alihutubia mkutano pale Kata ya Madibira na kuwaahidi kabisa kwamba Bajeti ya mwaka 2008. Sasa itaunganishwa na kuanza kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami na ukizingatia ilani hii ni ya miaka mitano na sasa ni miaka miwili tu imebaki.

Kwa hiyo, Naibu Waziri aweze kujibu kuweza kuwardhisha wananchi wa Mbarali. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ushauri wake kwa kweli wa kuanza kujenga madaraja na makalvati kama maandalizi vile vile ya barabara hiyo ya kiwango cha lami itakapoanza kujengwa ni ushauri nzuri ambao tutawaambia wataalam wafanye wakati wanatekeleza mradi huu wa *MSDP*. Ni kweli ni fedha nyingi lakini kwa sababu ni msaada ambao tumeupata na kwa kuwa tayari tulikuwa hatujawa katika hatua ya kwanza kujenga kwa kiwango cha lami tuliona tuondoe adha wanayopata wananchi kwa kutekeleza mradi huu ambao utasaidia sana wakati tunajiandaa kwenye barabara ya lami. Kuhusu barabara ya lami ni kweli kwamba Ilani imeeleza kwamba barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami katika miaka mitano hii ijayo, kama alivyosema ni kwamba bado miaka miwili na katika Wizara yetu tunajiandaa ili tuanze kuomba fedha kutoka Hazina ili katika Bajeti zinazokuja tuweze kuanza ujenzi huo. Kwa hiyo, itategemea sasa upatikanaji wa fedha kwa sababu kwa kweli barabara hiyo inategemewa kujengwa kwa fedha za ndani.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Kanuni.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 46 ukurasa wa 28. Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anajibu maswali yaliyopita alikuwa anasema hapa kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, hivi yupi? Au anatakiwa aseme nini katika wakati kama huu? (*Kicheko*)

**SPIKA:** Ninavyomwelewa Mheshimiwa Makongoro ni Naibu Waziri mwenye nidhamu, ni mtu safi kabisa. Lakini kama ambavyo sote binadamu huwa tunaghafilika. Kwa hiyo, nadhani alighafilika tu hapa. Hakuna haja ya kuliedeleza zaidi.

Na. 131

### **Kuboresha Huduma za Reli ya TAZARA**

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSIM** aliuliza:-

Kwa Kuwa, njia mojawapo ya kuboresha usafiri unaosimamiwa na nchi mbili za Tanzania na Zambia ni kuwa na matumizi mazuri ya ushirikiano wa Reli ya *TAZARA*; na kwa kuwa, lengo hilo litafanikiwa kwa kusimama na kuboresha huduma za Reli itokayo Dar es Salaam hadi Zambia:-

(a) Je, malalamiko ya tofauti ya mishahara yaliyopo kwa watumishi wa pande zote mbili baada ya madai kuwa watumishi wa Zambia wanalipwa vizuri zaidi yamechukuliwa vipi na Serikali?

(b) Je, nini mchango wa kila nchi katika kuhakikisha huduma hiyo inaboreshwa na kuwa nzuri tofauti ilivyo sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, umenikwaza kweli kwa sababu ningesema kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, nimesema kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu na Ofisi ipo sasa *anyway* sijui nisemeje. Lakini napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassim, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:- (*Kicheko/Makofsi*)

(a) Mheshimiwa Spika, tatizo la tofauti ya mishahara ya wafanyakazi wa *TAZARA* kwa upande wa Tanzania na Zambia limekuwa likiathiri pande zote mbili kwa nyakati tofauti. Chanzo cha tatizo ni kutokana na mishahara ya *TAZARA* kupangwa kwa kutumia Dola ya Marekani ingawa hulipwa kwa fedha za ndani ya kila nchi (*local currency*), yaani shilingi kwa upande wa Tanzania na Kwacha kwa upande wa Zambia.

Uzoefu umeonyesha kwamba mabadiliko ya thamani ya fedha za ndani ikilinganishwa na Dola ya Marekani hutegemea sana hali ya uchumi wa kila nchi kwa wakati huo na hivyo kupelekeea kuleta tofauti kwa kiasi kile kile cha Dola kinapolipwa

kwa fedha ya ndani ya kila nchi. Serikali ya Zambia na Tanzania kwa pamoja zimeshughulikia malalamiko ya tofauti ya mishahara ya wafanyakazi wa *TAZARA* upande wa Tanzania kwa kurekebisha kiwango cha Dola kutokana na thamani halisi ya fedha ya nchi kutoka viwango vilivyokuwa vikitumika huko nyuma.

(b) Mheshimiwa Spika, michango ambayo Serikali mbili imekuwa ikitoa mara kwa mara katika kuhakikisha kwamba huduma za reli ya *TAZARA* zinaboreshwani pamoja na zifuatazo:-

(i) Kuingia Mikataba ya kiufundi ya Itifaki (*Technical Protocols*) kati ya Serikali zetu mbili na Serikali ya watu wa China. Kupititia Mikataba hii *TAZARA* imekuwa ikisaidiwa vifaa mbalimbali vya shughuli za utendaji na wataalam kutoka China. Hadi mwaka wa fedha 2006/2007, jumla ya Itifaki 12 zimetekelizwa. Itifaki ya 13 imekwishatiwa saini na kwa sasa ipo katika mchakato wa utekelezaji

(ii) Serikali ya Tanzania na Zambia, zimeisamehe *TAZARA* ushuru kwa vipuri na malighafi zote zinazoagizwa kutoka nje kwa ajili ya matumizi na shughuli za reli.

(iii) Serikali ya Tanzania na Zambia zimeisamehe *TAZARA* kodi za mtaji, mapato na mali nydingine zisizohamishika.

(iv) Serikali hizi mbili zimekuwa zikiipatia *TAZARA* kupitia bajeti zake za mwaka fedha kwa ajili ya ukarabati wa maeneo korofu ya reli ya Mpanga – Kitete na uboreshaji wa miundombinu ya mawasiliano.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSIM:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Shirika la *TAZARA* liko katika hali mbaya sana. Je, Serikali ni lini itaisaidia *TAZARA* ili iweze kuendeleza reli hii na iwe katika hali nzuri?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba *TAZARA* iko katika hali mbaya sana, miundombinu kwa maana ya injini na mabehewa kwanza ni machache na yako katika hali mbaya. Aidha, mtaji umekuwa ni mdogo.

Sasa mambo ambayo Serikali zetu mbili zinafanya ni kuelekea katika mchakato wa kumpata mwekezaji ambaye atakodishwa reli hii ili aiendeshe. Tunadhani kwamba kwa sababu wenzetu wa China ndiyo walijenga reli hii tunazungumza nao na kama mlivyosikia hivi karibuni, Mheshimiwa Rais alipokuwa China amezungumzia suala la *TAZARA* alipokuwa China amezungumzia suala la *TAZARA* na Serikali ya China ambao kwanza wamekubali kufuta deni la dola 500 milioni na hivyo itakuwa imesaidia sana. (*Makofi*)

Lakini vile vile wameahidi kuleta makampuni ya reli ya China ili yaje yafanye utafiti wa kuona kwamba nani anaweza akaingia katika kukodisha reli hiyo. Tunadhani kwamba kwa kufanya hivyo tutaweza kupata njia sasa ya *TAZARA* kuendelea. Kwa sasa

tunajaribu tu kuhakikisha kwamba *management* ambayo kidogo ina uhafifu pale inafanya kazi vizuri na madeni ya ndani kwa sababu wana madeni mengi kama pensheni na madeni mengine ya *suppliers* kwa kweli inalipwa. Kwa hiyo, tunaisimamia *TAZARA* wakati tunaendelea na mchakato wa ukodishwaji. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita. Maswali yale mawili ya Wizara ya Fedha tutayapangia siku nyingine.

Matangazo naanza na wageni. Wageni wetu kwa siku leo ni kama ifuatavyo:- Kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka, Mbunge wa Morogoro Mjini, Mzee Kupera. Mzee Kupera ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Kata ya Kihonda. Naomba Mzee asimame. Ahsante sana. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir kama ifuatavyo:- Bi. Mariam Makungu, naomba asimame. Yule pale. Bi. Mwanamkuu Khamis. Bi. Kazi naona hii imekosewa, lakini imeandikwa Kazi Haji Suleiman. Yule pale na Bi. Shekh Mohamed ambaye ni Mkewe Mheshimiwa. Wengine wote ni kutoka Jimboni kule Dimani. Karibuni sana kutoka Zanzibar, tunashukuru sana kuwaona hapa. (*Makofi*)

Pia miongoni kwa leo wapo wanafunzi 70 kutoka *St. John University Dodoma*. Nadhani hawa ni viongozi wa wanafunzi pale Chuo Kikuu St. John. Wale pale, karibuni sana. Pia tunao wanafunzi 50 kutoka Shule cha Kiwanja cha Ndege Sekondari hapa Dodoma. Naomba wasimame, Sekondari Kiwanja cha Ndege wale pale wanaopunga. Ahsante sana vijana wetu tunawatakania mfanye vema katika masomo. (*Makofi*)

Mikutano na Vikao. Mheshimiwa Estherina Kilasi, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, anaomba leo tarehe 21 mwezi huu wa nne 2008 Wajumbe wote wa Kamati hiyo ya Hesabu ya Mashirika ya Umma watakuwa na kikao kifupi na Msajili wa Mashirika ya Umma katika Ukumbi wa Pius Msekwa saa 5 asubuhi. Kamati ya Hesabu ya Mashirika ya Umma saa 5 leo hii Ukumbi wa Pius Msekwa. Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama ameniomba nitangaze kuwa Wajumbe wote wa Kamati hiyo, wakutane leo baada ya kipindi hiki cha Maswali, Ukumbi Na. 219 Jengo la Utawala. Kwa hiyo, Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama, mara baada ya matangazo yangu haya Ukumbi Na. 219.

Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Katibu wa Kamati ya Waheshimiwa Wabunge wa CCM ameniomba nitangaze kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati ya Uongozi leo saa 7 mchana katika Ukumbi 118. Kamati ya Uongozi ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi saa 7.00 mchana Ukumbi Namba 118.

Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mwenyekiti wa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Tabora ameniomba nitangaze kuwa baada ya Ofisi yangu kutenga magari kwa ajili ya kwenda kwenye msiba wa Mheshimiwa Ditopile aliyetutoka jana, basi wale Wabunge hususan wa Mkoa wa Tabora ambao ndiyo marehemu alikuwa Kituo chake cha kazi cha mwisho akuwa Mkuu wetu wa Mkoa basi mnaombwa mkutane mara baada ya matangazo

haya ili kupanga utaratibu wa safari. Kwa sababu itabidi kuondoka leo jioni ili kuweza kushiriki shughuli za mazishi kesho kule Kinyerezi. Ahsante. (*Makofi*)

Hili tangazo la mwisho hili limeniomba, Wabunge kadhaa wamejiorodhesha hapa wameniomba nitangaze kuipongeza Timu ya Yanga kwa kuchukua Ubingwa. Sijapata taarifa rasmi kutoka *TFF*. Lakini kwa kuwa Waheshimiwa waliojiorodhesha hapa ni watu waheshimika kweli kweli inawezekana hii ikawa ni kweli. Kwa hiyo, ikiwa hivyo ni kweli basi kwa niaba yenu nyote tunaipongeza Timu ya *Young Africans* kwa kuchukua ubingwa wa Tanzania Bara mwaka huu wa 2008 kuelekea 2009. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, natumia Kanuni Na. 68(7) ili niweze kupata mwongozo wako. Kwanza nikupongeze Mheshimiwa kwamba wewe ndiyo Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na katika kujadili tumepitisha Kanuni mpya ambazo zinashughulikia masuala ya UKIMWI.

Kwa kuwa UKIMWI ulikuwa ni janga kubwa na unaendelea kuwa janga kubwa katika nchi hii. Je, utakubaliana na mimi kwamba Kamati yako ni vyema kabisa sasa ikakaa ikaangalia namna itakavyoweza kuanzisha Kamati mpya kushughulikia masuala ya Ufisadi katika nchi yetu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwanza ngoja nitoe mwongozo wa jumla kuhusu miongozo mnayoomba Spika aitoe. Hii miongozo sio ya kulipuka tu.

Lazima iwe inaungana na kinachoendelea wakati huo lazima iwe shughuli zinazoendelea basi mwongozo unalingana. Vinginevyo itakuwa kila wakati Mbunge anatumia Kanuni lakini analouliza ni jambo amelifikiria tu kwa wakati huo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa itakuwa vigumu sana kuendesha Bunge kwa namna hiyo. Mara nyingi tunahitaji miongozo kwa mfano sasa matangazo haya niliyoyatoa ama shughuli za maswali mtu angeomba mwongozo ama utaratibu kwa maana kumetokea jambo ndani ya Ukumbi hivyo tunavyofanya.

Kwa hiyo, kwa kuwa mwongozo ulioombwa ni haramu. Haulingani kabisa na Orodha ya Shughuli tulizokuwa tunaendelea nazo. Naliacha kwa sasa hadi utakapouлизwa wakati muafaka na ndiyo nitatoa mwongozo wangu. (*Kicheko/Makofi*)

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Umeme wa Mwaka  
2007 (*The Electricity Bill, 2007*)**

(*Kusomwa mara ya Pili*)

(*Majadiliano yanaendelea*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada wetu huu wa masuala ya umeme, ninayo orodha ya wachangiaji 36 na ninakusudia kuwaruhusu wote. Kwa hiyo, tutaendelea hadi kesho saa 7 kuweza kuwapitia. Kwa hesabu zangu tunaweza kufika hapo, ili kumwezesha Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini aweze kuanza kujibu hoja saa 11 kesho.

Kwa hiyo, tunayo nafasi nzuri tu na kwa maana hiyo sasa wasemaji wangu niwataje wanenye wa kwanza, ni Mheshimiwa John M. Cheyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi, halafu Mheshimiwa Fatma Mikidadi halafu Mheshimiwa Raynald Mrope.

Kwa wale Waheshimiwa Wabunge ambao wanasaifiri kwenda kwenye mazishi Dar es Salaam ambayo inawabidi waondoke mchana huu basi nitaangalia maana yake sasa hivi wana kikao basi watakaporejea nitawatambua. Kwa hiyo, nitawapa nafasi ili wasikose kuchangia. Kwa hiyo sasa namwita Mheshimiwa John Momose Cheyo wakati huo huo Mheshimiwa Godfrey Zambi, ajiandae.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nataka kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa leo kwa Muswada huu muhimu juu ya umeme. Kabla sijachangia nataka kutumia nafasi hii kuwapa pole sana ndugu zangu wa Bariadi hususan Nkoma kwa kushindwa kupita kwenye daraja lao kwa sababu ya mvua na daraja hilo pamoja na fedha kutolewa na Mheshimiwa Rais, lakini limepata Mkandarasi mbaya. Lakini mvua pia zimeleta neema ambayo kwamba mwaka huu natumaini zao la pamba litakuwa zuri. Kwa hiyo, natumia nafasi hii kuiomba Serikali ijiandae kuhakikisha kwamba angalau bei haishuki chini ya shilingi 500 kwa kila kilo moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Muswada uliyo mbele yetu siyo Muswada wa kuleta umeme vijiji. Muswada huu maana yake unainyang'anya Serikali ukiritimba wa kuweza kutumia rasilimali tulizopewa na Mwenyezi Mungu ili zitumiwe na watu binafsi kuweza kupata umeme na kuusambaza. Hiyo ndiyo *debate* ambayo tuliyonayo. Msimamo ambao mimi naona haujalezwa bayana je, ni kweli kwamba Mungu ametupa zaidi ya megawats ya *hydro power* za megawats ambazo tunawenza kupata kwa kutumia maji, zaidi ya megawats milioni 4.7. Ametupa makaa ya mawe zaidi ya tani milioni elfu moja mia mbili. Ametupa gesi asilia zaidi ya bilioni 45 *cubic metres*.

Hivi kweli sasa hivi ndiyo tupitishe Muswada ambao unasema vyote hivi vifunguliwe kwa mtu yoyote yule anayetaka kuzalisha umeme bila kuweka utaratibu mahususi wa ushiriki wa Serikali. Tumefanya makosa hayo hayo kwa madini, tumefungulia mlango makampuni makubwa ya madini yamechukua mali zetu na hatujaona faida ya aina yoyote. Muswada huu unatupeleka huko huko ni mwaka gani Tanzania tutajifunza, kwamba Miswada au Sheria ambazo zinahusu rasilimali ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu ni lazima kwanza zifanyiwe utafiti unaofaa, itengenezewa *impact assessment* yaani ulinganishwe ni jinsi gani kutakuwa na madhara ya namma gani. Sijaona ripoti ya aina yoyote ambayo inaonyesha baada ya Muswada huu ni viyi Serikali na Watanzania watafaidika bila kupoteza rasimali hizi.

Mheshimiwa Spika, tayari mtindo umeanza kuonekana kwamba mahali ambapo Mwenyezi Mungu ametupa pa kutengenezea makaa ya mawe kwa mfano, tumetoa kwa bure. Kinachosikitisha pamoja na kusema kwamba ufisadi siyo kwamba hulijibu lile swalii, lakini kinachosikitisha kwamba ni viongozi wa nchi hii wanunuua kwa ajili ya kutengeneza umeme, rasilimali kwa bei ya chee. Muswada huu unatupa nini ili kulilinda Taifa hili kwamba kwa kufungua milango tena bila masharti hatutapoteza kama vile tumeanza kupoteza kwa madini, kama vile tumeanza kupoteza Kiwira kwa mfano. Nina wasi wasi sana juu ya Muswada huu. Kama Muswada huu unatupeleka kwa sababu ya shinikisho la watu wanaotufadhili mimi nashauri ni afadhali Tanzania tusimame kidete. Tuseme hii fedha weka huko, tutaangalia kwanza maslahi ya Taifa letu. Ufisadi huu utatumaliza na kwa Muswada kama huu ambao unafungua kila kitu, milango na kila kitu ndiyo njia mzima kabisa ya kuhakikisha kwamba ufisadi utaendelea.

Mheshimiwa Spika, ukiona kuna *too many disrecreations* sana hapa yaani kuna uhuru mkubwa sana wa *EWURA*. *EWURA* katika *section 11* anaambiwa anawenza

kugeuza hata masharti. Kama *EWURA* anaweza kugeuza hata masharti ndiyo kusema hata mwekezaji yoyote atakayekuja Tanzania atataka atengenezewe mkataba unaompa, kitu ambacho tumeona kwenye madini *feasical stability*. Yaani uhakika wa hali halisi, la sivyo hatawekeza. Kwa hiyo, Muswada huu haujafanyiwa utafiti wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kama Muswada huu ungekuwa umefanyiwa utafiti wa kutosha huwezi katika *Section* ya 14 kifungu kidogo 5(b) ukasema kwamba umeme utatolewa au kuingia katika shughuli za umeme utafunguliwa bila masharti ya aina yoyote.

*None discriminatory license.* Halafu kwenye *Section* ya 41 unasema kwamba eti *TANESCO* itapata nafasi kwa wale ambao ni watumiaji wakubwa wa umeme. Hii ni njia nyingine ya kutoa nafasi ya rushwa. Kwa hali halisi iliyopo sasa hivi kinazuia nini mtu kwenda kwa Mkuu wa *TANESCO* na kusema jambo hili bwana huliwezi, hebu nipe kibali.

Kibali kikatolewa na ukaona watu wanaanza kutengeneza umeme kwa kutumia rasilimali zetu, kwa kutumia mito yetu. Kwa kutumia gesi yetu na Mungu ametupa hata *uranium* wakaenda tu kwa watumiaji ambao ni wakubwa kama vile Gabanga ambayo itakuja, kama vile *North Mara*, kama vile *Geita Gold Mines*, *TANESCO* ikaachiwa kuwashasha vikoroboi tu katika vijiji. Kwa hiyo, hiyo ni njia mahususi kabisa ya kuiua *TANESCO* moja kwa moja. Mimi naona Muswada huu haujafanyiwa utafiti wa kutosha.

Wale wanaofikiri eti kwa kuwekeza kwa kumleta mwekezaji binafsi ndiyo tutapata umeme vijijini, wanajidanganya wao wenyewe pamoja na watu ambao wanawasiliza. Hakuna mfanyakishara atakayeweza kuwekeza katika umeme ili apeleke umeme ili apeleke umeme Gambasiu hakuna. Itabakia tu kuwa kwamba watakatengeneza umeme watakimbilia huko huko kwenye Shirika la *REA* ili waweze wakapata ruzuku kwa ajili ya uwekezaji katika umeme.

Jambo hili nasema pia halijafanyiwa utafiti wa kutosha. Sio hivyo tu, *EWURA* tumeambiwa kila kitu ukisoma kila *section* ya hapa *EWURA* juzi hapa tumekutana na hali mbaya sana katika Taifa hili ambapo mafuta yanachanganywa ya dizeli na mafuta ya taa. Tulipouliza tukaambiwa kwamba jibu *EWURA* yenyewe ni juzi ndiyo tumeianzisha. Haina fedha, haina wataalam, ni *EWURA* gani ile ambayo Mheshimiwa Waziri anafikiria itakayoweza kusimamia jambo muhimu kama hili. Muswada huu haujafanyiwa utafiti wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, mimi naona kuna uwezekano kabisa wa kuwa na ushirikiano kati ya Serikali na *Private Sector* na Wazungu siku hizi hawazungumzii juu ya *private sector* peke yake wanazungumzia juu ya *PPP Public and Private Sector Participation*. Wote wawili wanakwenda pamoja.

Muswada huu unafungua mlango tu, *open*. Mimi ninashauri kama haitawezekana kuweka *amendment* katika Sheria hii basi Waziri kwa sababu ya hali halisi ya Bunge hili najua atapitisha huu Muswada basi mimi nashauri katika *regulations* au Kanuni atakazotunga, angeweka wazungu wanasma *caping*, agawanye wale binafsi ambao wanaruhusiwa kuingia katika soko hili kwa mfano, kwa kutengeneza umeme kutumia rasilimali tulizopewa na Mwenyezi Mungu ni lazima wawe na *share* na Serikali asilimia isiyopungua angalau 25 ndiyo ya mwisho kabisa ili tupate mtu wetu kuchungulia mle wanafanya kitu gani. Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Pili, nashauri na ni hatari kabisa kwa mfano kama kuna vita wewe unasema kila mmoja anaweza akawasha umeme na kupeleka kokote anakotaka. Unataka leo kwa sababu umeshambuliwa kuzimisha umeme, ukizimamisha umeme wa mtu binafsi, *transmission* yake unapata *bill* ya kulipia kwa sababu umemkatisha asitoe ule umeme. Nchi nydingi zimejaribu, na ripoti zipo za *World Bank*.

*Transmission* ndiyo mshipa, ndiyo njia ya umeme. *Transmission* isitolewe holela kwa watu binafsi, hapo pia la kwanza ningeshauri iimarishe *TANESCO* ikiwezekana tuikatekate *TANESCO* iwe katika mashirika mbalimbali na mojawapo ya jukumu la shirika tutakalokatakata iwe kusafirisha umeme, *transmission*. Kama kuna ulazima wa kuingiza mtu anayetoka nje basi Serikali iwe na *share* katika kampuni hiyo angalau asilimia 25 ili jicho letu la Serikali la matumizi makubwa ya umeme liwepo.

Mheshimiwa Spika, natoa angalizo. Najua muswada utapita wala Mheshimiwa Waziri asiwe na wasiwasi. Lakini tusipojikinga baadaye tutakuja kujuta kama vile tunavyojuta sasa na kusingizia sheria zetu za madini na mikataba ilikuwa mibovu. Tumechoka kusikia hadithi hizo, ni lazima tuamke sasa tutengeneze muswada utakaoishi leo na kesho na keshokutwa huku ikilinda maslahi na rasilimali za taifa hili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuzungumza.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia huu muswada wa umeme ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba tu niseme kwamba mimi ni mionganoni mwa Wabunge ambaio mara ya kwanza muswada huu tulipoletewa kwenye semina niliukataa. Lakini niliukataa kwa sababu ambazo wenzangu walikwizhazieleza lakini pia namshukuru sana Waziri na Kamati, nadhani wamefanya kazi kubwa sana. Kwa sehemu kubwa yale mapungufu mengi ambayo Wabunge wengi tulikuwa na wasiwasi wamejaribu kuyaondoa, kwa hilo naomba sasa niseme kwamba naunga mkono muswada huu (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, muswada huu wadau wake wakubwa ni wananchi watakaotumia umeme kwa hiyo, naiomba Wizara kwamba muswada huu ukishapita na

Mheshimiwa Rais akishauridhia kuwa sheria, uchapishwe kwa wingi na usambazwe vijijini au mahali kote kule ambako wananchi watakuwa wanatumia umeme kwa sababu kuna mambo mengi ambayo wananchi wanapaswa wayajue yatakayohusu haki zao. Pale ambapo inawezekana wale watakaokuwa wazalishaji wakienda kinyume na yale ambayo yamezungumzwa kwenye muswada wachukuliwe hatua. Kwa hiyo, ni vizuri sheria ikishapita isambazwe kwa wananchi vijijini. (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo naomba nizungumze baadhi ya mambo ambayo yapo kwenye muswada wenyewe. Kuna *section* ya sita kifungu cha 1(b) kinazungumza *accessibility* na *affordability*. Sina shaka juu ya *accessibility* kwamba nia ni kupeleka umeme huko kwa watumiaji. Lakini tatizo langu ni pale tunapozungumza *affordability*.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kuzungumza kwenye semina ile kwamba wafanyabiashara hawa wa umeme ambao tuna hakika baada ya muswada kusainiwa watakuja, hawaji kufanya matembezi ya hiyari wala hawaji kufanya biashara ya hisani. Wanakuja kufanya biashara ambayo lengo lake ni kupata faida na wakati wote hakuna mfanyabiashara ambaye anaingia kwenye biashara ya kutoa huduma kwa mtu ambaye anakusudia kufanya biashara, wanataka wapate faida. Sasa hili limenipa tabu kidogo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu anifafanulie hii *affordability*. Maana yake unaweza ukajiuliza *how affordable* huu umeme utakuwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, najiuliza hivyo kwa sababu leo ghamra za mwananchi wa kawaida kuingiza umeme kwenye nyumba yake ni kati ya shilingi 400,000 na 500,000. Huu muswada unalenga tusambaze umeme kwa kasi kubwa sana vijijini. Sasa ni wananchi wangapi vijijini wanaweza waka-*afford* hizi bei za umeme kama ndio ziko hivyo? Na mimi sidhani kama kweli bei ya umeme itashuka sana pamoja na kwamba hawa wawekezaji wengine wanakuja. Kama nilivyosema madhumuni yao ni kuja kufanya biashara. Kwa kuwa wananchi wanasubiri kwa hamu sana kupata umeme lakini *affordability* yake ambayo huu muswada inaisema ikoje? Naomba Mheshimiwa Waziri atufafanulie vizuri ili na kuwaondoa wasiwasni wananchi. (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, jambo jingine la pili ni la *section* ya sita kifungu kidogo cha (2)(b)(i) *compulsory acquisition of land*. Tumeona mahali pengi ambapo huduma nyingine zinapelekwa na panahitaji pengine nyumba za wananchi ziondolewe, mashamba ya wananchi yakatwe ili huduma hiyo iweze kupita. Hiyo ni dhahiri kwa sababu ardhi ni mali ya Serikali na Serikali inaweza ikaitumia ardhi muda wowote ambapo inafikiri ni muafaka kufanya hivyo.

Tatizo langu ni pale ambapo vitu hivyo vinachukuliwa, vitu hivyo vinaharibiwa lakini wananchi hawawi *compensated* mapema au inakuwa kesi kuwalipa wananchi. Kule kwangu Mbozi limetokea, tumepitisha *line* za simu hizi za *Celtel*, makampuni mbalimbali lakini kumekuwa na kesi na wananchi wale ambao mali zao zimeharibiwa. Sasa katika hili tunaomba Mheshimiwa Waziri awahakikishie wananchi kwamba usumbu ule ambao umetokea kwa wananchi wale wakati huduma nyingine zinapelekwa sasa hautatokea wakati huduma hii inafanyika.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine *section* ya 11(2) kwenye muswada, uhamishaji wa leseni. Hapa pananipa tabu kidogo. Kwamba kuna mtu ambaye atakuwa anafanya biashara hii ameweka *service line* yake anasambaza umeme. Umefika muda anatoa *notice* ya miezi 12 kama unavyosema muswada, kwamba sitegemei sasa kuendelea kuzalisha umeme na kuuzia wananchi wa eneo hili. Anatoa *notice* ya miezi 12 na hajitokezi mtu mwingine wa kuchukua ile biashara. Hapa naomba nielezwe maana yake wananchi hawa ambao walikwishatumbia umeme pengine miaka 5, 10, wanaweza sasa wakaachwa gizani. Na pengine huduma ya *TANESCO* wakati huo haiko jirani, iko mbali.

Katika mazingira hayo tutafanya namna gani? Je, hautakuwa sasa usumbufu kwa wananchi tena? Sasa hapo nataka nishauri kwamba pale ambapo *TANESCO* iko mbali lakini wawekezaji hawa binafsi wameweka *service line* zao naomba *TANESCO* sasa ifanye jitihada ya kufikisha *transmission line* kule ili mwekezaji anayendoka na wakati huo huo hajitokezi mwingine, basi *TANESCO* iweze kuchukua hiyo huduma na kuwapelekea wananchi ili ku-*avoid* wasipate usumbufu. (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie suala la *exemption*. Kwenye muswada *section* ya 18 inazungumzia *exemption*. Mimi nina wasiwasi sana, tumeona *exemption* mahali pengi zilivyotumika vibaya. Sasa muswada unasema wale ambao watazalisha umeme *off grid*, na chini ya megawati tatu nadhani watapewa *exemption*. Na wale ambao hawatatumia huduma za *TANESCO* lakini wanazalisha chini ya megawati tatu watapewa *exemption* kadri ya muswada unavyosema.

Mheshimiwa Spika, lakini megawati tatu ni biashara kubwa. Kama ukizalisha umeme na kuwauzia watu 100, watu 200 nadhani ni bisahara kubwa. Lakini wasiwasi wangu mkubwa ni kwamba hii *privilege* inaweza ikatumwa vibaya. Kama *EWURA* ndio watapewa madaraka hayo na hali iliyopo nchini nadhani *privilege* hiyo itatumika vibaya na kwa maana hiyo tukawanufaisha watu wengine wachache badala ya kuwanufaisha wananchi kama tulivyokusudia. Kwa hiyo, naomba niseme *exemption* iondolewe, na kama haiondolewi basi kuwe na *a certain percentage* ambayo wanatozwa si sawa pengine na wale ambao watakuwa na leseni ambazo watahitaji kutumia *transmission line* au kuingiza umeme huu kwenye gridi ya Taifa. Lakini walau wapewe tozo ya aina fulani kuilipa Serikali kuliko kusema kwamba watakuwa *exempted* kabisa. Kwa vyovyote vile watawauzia wananchi umeme na watapata faida. Kwa hiyo, kifungu hicho nina wasiwasi nacho na ningeshauri kiondolewe kwa sababu hivi ndivyo vinavyoleta ushawishi wa mwanzo kabisa kwa wale ambao watakuwa wanahusika na shughuli hiyo moja kwa moja kwa maana ya *EWURA*.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo kubwa sana katika nchi yetu kubwa sana. Na mimi hapa nazungumzia jinsi *EWURA* walivyopewa nguvu kubwa sana kwenye muswada huu, wamepewa nguvu kubwa sana. Lakini nchi hii, na jambo hili lazima tulizungumze sana kwasababu sisi tuko Bungeni tunazungumza maslahi ya wananchi na maslahi ya Taifa hili. Unapotembea mahali pengi kinachozungumzwa leo kwamba Wabunge angalieni maslahi ya nchi, Wabunge angalieni maslahi ya wananchi. Sasa kumekuwa na tatizo kubwa, kubwa sana la ufisadi, kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mimi natoka Mbozi, kule kwetu kuna kitendawili kimoja kinaitwa kwa lugha ya Kinyiha, *katetekayembe*. *Katetekayembe* maana yake, hata dada yako angekuwa mzuri namna gani huwezi kumuo. Ndio maana ya *katetekayembe*. Dada yako hata angekuwa mzuri namna gani huwezi kumuo. Lakini leo katika nchi hii, leo katika Serikali hii kumekuwa na viongozi akina *katetekayembe*. Kumekuwa na viongozi akina *katetekayembe* ambao sasa wameamua kuoa dada zao; wameamua kuoa na mamazao pia. Maana yake watu wanaila nchi hii bila aibu kabisa. Viongozi wengi wamekuwa hawana uchungu na nchi hii kabisa. Tunaomba haya yasitokee kwa wenzetu wa *EWURA*.

Tunaomba haya yasitokee, lakini pia wenzangu walizungumza, hii itakuwa ndiyo *taste* kubwa sana kwa Mheshimiwa Waziri. Tunajua ni kijana anarekodi nzuri lakini miswada hii ndiyo inayoweza ikamchafua, ikampaka matope, na *career* yake katika umri wake inaweza ikawa mbaya. Kwa hiyo, tuna matumaini na yeze na kweli asimamie vizuri ili wananchi hawa wapate kile ambacho wamekitumaini. (*Makofî/Kicheko*).

Mheshimiwa Spika, nizungumze kidogo ya Jimboni kwangu. Tunaomba *TANESCO* iimarishwe ili ipate uwezo wa kupeleka umeme kule ambako wawekezaji wengine hawa inawezekana wasifike. Na mimi naomba *TANESCO* iimarishwe lakini pia imalizie hata miradi ya umeme hata ambayo imebaki kule Mbozi kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, nimekwishapiga kelele sana humu ndani. Kuna miradi ya umeme Mbozi ambayo ni ya miaka nane sasa. Kuna mradi wa kutoka Ruanda, Iyula, Idiwili, kilomita 26, umeanza mwaka 2000 mpaka leo nguzo zimewekwa lakini hakuna kinachoendelea. Kuna umeme wa kutoka Mahenje kwenda Igunda kilomita tatu, nguzo zimewekwa mpaka leo, tangu mwaka 2000. Lakini kuna umeme kutoka Vwawa, Hasamba kwenda Nyimbili nguzo zimewekwa miaka karibu sita hakuna kinachoendelea. Sasa kama hatuwezi kuimarisha *TANESCO* tukaipa uwezo wa kufanya kazi hii, nachelea kusema kwamba haya yote ambayo tunayategemea yanawezekana kabisa yasifanyike. Na nilishamwandikia Mheshimiwa Waziri, kwamba Wilaya ya Mbozi kimsingi ni Wilaya ya Uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri wakati tunataka kusambaza umeme kwa wananchi basi azifikirie sana Kata hizi ambazo nilishamwandikia. Kuna Kata ya Iyula wanazalisha sana kahawa na kule ndiko nguzo zipo lakini hakuna umeme. Kata ya Isansa, kata ya Nyimbili, kata ya Msia, kata ya Halungu, Itaka Nambinzo na Mlangali. Hizi zote ni kata za uzalishaji, zile ambazo sijazitaja ndizo pale umeme umepita walau wananchi wachache wana umeme lakini bado usambazaji wake haujawa mzuri sana.

Kwa hiyo, naomba wale ambao wanakuja kuwekeza, Waziri atuangalie kwa sababu nia ni kuinasua nchi hii kutoka kwenye umaskini, kuwaondoa wananchi kwenye umaskini kwenda kwenye maisha bora. Kama hatuwezi kuhakikisha kwamba maeneo haya yanapata huduma ya umeme tutakuwa hatuwezi kuwaondolea wananchi umaskini kama vile tunavyozungumza kwenye Ilani yetu ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba niseme kwamba tunajua kumekuwa na *pressure* kubwa sana za shirika la fedha la dunia na *World Bank*, na ndio haya yaliyosababisha *reforms* kwenye sekta mbalimbali na sekta ya umeme ikiwa mojawapo. Na hizi *reforms* kimsingi zimeanza kwa kasi sana miaka ya 1990. Mashirika haya yamejaribu ku-*push* lakini kwa sehemu kubwa kwa maslahi yao wenyewe. Sasa haya mashirika mengine yatakayokuja kwenye kuwekeza vyovoyote vile yatakuwa yanakuwa *backed-up* ya nchi zao. Sasa tusipokuwa waangalifu kwenye mikataba ambayo tutaingia tukifikiri kwamba tunaingia mikataba hii na mtu mmoja mmoja kumbe tutakuwa tunaingia mikataba na nchi tajiri ambazo nia yake ni kutaka kuendelea kuzinyonya nchi masikini kwa faida yao zenyewe. Na pengine huu ndio tunaweza tukawa tunauita sasa ukoloni mamboleo unarudi kwa *form* nyininge.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri awe mwangalifu sana aisaidie nchi hii ili kweli asilimia moja hiyo ya umeme ambayo wananchi wa vijijiini wanaipata leo basi itoke hapo. Na hata tunapofika mwaka 2010 tuwe timesogea mbele.

Mheshimiwa Spika, nikishasema hivyo, naomba nirudie kusema kwamba naunga mkono hoja hii. Asante sana.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuzungumzia muswada huu wa umeme wa mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuwapongeza Wizara, Waziri, Naibu waziri pamoja na Kamati ambayo imefanya kazi kubwa sana usiku na mchana. Nafikiri hawa vijana hawakulala kwa kweli, na mimi nimeshuhudia kwa sababu tulikuwa tunagongana mitaani wakihangaika kuukarabati muswada huu kwa vile kwa mara ya kwanza walipouleta kwenye semina, Dodoma na Dar-es-Salaam, kwa kweli watu waliupigia makelele sana. Kwa hiyo, ilibidi kwa kweli waukarabati ilii Wabunge waukubali pale ambapo utakapoletwa Bungeni. Na sasa kwa kweli muswada huu umeletwa wakati muafaka.

Lakini wakati ule ulipoletwa Dodoma halafu ukaletwa Dar-es-Salaam kwa kweli watu waliupigia kelele. Kwa sababu mtu alipokuwa anazungumzia tu suala la umeme basi hakuna kingine alichofikiria, ni *RICHMOND* na *DOWANS*. Hakuna kingine alichofikiria ni *IPTL* au *capacity charge*. Kwa hiyo, kulikuwa na makelele mengi sana. Hao vijana wanastahili pongezi kwa kazi waliyoifanya ya kuukarabati mradi huu mpaka wenzetu Wabunge na wananchi sasa hivi wametulia na kukubali mradi huu. Karibu wengi walitangulia wanasema tumeukubali, tunaukubali nafikiri na mimi nitauunga mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye hoja ambayo ipo hapa mezani petu ya muswada huu. Kama walivyotangulia kuzungumza wenzangu hapo mwanzo kwamba aliyeumwa na nyoka hata akiona kamba hushtuka. Aliyeumwa na nyoka hata akiona kamba akikanyaga hushtuka, wengi wamezungumza suala hilo, kwa nini? Kwa sababu ni kuumwa kuumwa tu. Watu wamezungumza hivyo wana maana yao. Na hii nadhani

maana yake ni yale yale yaliyotokana na kukataliwa kwa muswada huu pale walipozungumzia kwenye semina Dodoma na kwenye semina Dar-es-Salaam. Kwa sababu walidhani ni yale yale ambayo watu wameyazungumza ya *RICHMOND, DOWANS, IPTL, Kiwira, Net Group*, na kadhalika. Wakasema haya ni yaleyale, lakini kumbe sivyo. Sasa hivi mradi umekarabatiwa na mzuri utashangaa.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nitoe angalizo kwa mambo yafuatayo kabla sijasema kwamba naunga mkono mia kwa mia. Naomba nitoe angalizo kwa mambo yafuatayo: Kwanza, kuna kipengele kimoja kinachozungumzia umeme wa dharura. Wakati nauliza swali la nyongeza nafikiri niligusia kitu kama hicho. Kipengele cha umeme wa dharura.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna umeme wa asilia kwa miaka mingi tu. Kwa mfano, Songo Songo tulikuwa na umeme wa asilia tangu mwaka 1974 na *Mnazi bay*, tulikuwa na umeme wa asilia tangu mwaka 1982. Lakini miaka yote tulikuwa tunategemea umeme wa *hydro*, yaani umeme wa maji. Hayo yote hatukuwa tunafikiria na sasa hivi tunao umeme mwingine ambao umegunduliwa pale Kisarawe. Haya yote mpaka sasa hatujafikiria, tunangoja umeme wa dharura. Sasa kipengele hiki cha umeme wa dharura kwa kweli mimi kinanitia wasiwasi. Kwa sababu sasa hivi kipengele cha umeme wa dharura kinaleta matatizo na hiki kipengele cha umeme wa dharura ndicho kinachotusababishia kuleta mikataba ya dharura vilevile.

Mheshimiwa Spika, nasema mikataba ya dharura vilevile kwa maana ya mikataba mibovu. Kwamba lete mikataba tufanye haraka kwa sababu kila kitu ni dharura. Sasa hivi watu hawategemei tena umeme wa maji (*hydro electric*). Kwa sababu Mwenyezi Mungu anaweza akayaleta maji, mvua ikanyesha, Mwenyezi Mungu pia anaweza asiyalete, mvua isinyeshe. Lakini gesi asilia ipo tayari chini ya ardhi, ipo pale tayari. Kwa mfano, gesi ya *Mnazi bay* Mkoa wa Mtwara ipo pale.

Wataalamu wenyewe wanasema kwamba itakuwepo kwa miaka 140 kwa sababu watu wa Lindi hawaitumii. Wanatumia megawati tano tu basi, itakuwepo kwa miaka 140. Sasa kuna haja gani ya kusubiri maji ya Mtera ambayo kila mwaka bahati nasibu. Nafikiri tuweke angalizo kipengele hiki cha umeme wa dharura, tusingoje masuala ya dharura kiasi kwamba yakatuweke katika mtego wa kina *RICHMOND, DOWANS, Kiwira, NET GROUP, SONGAS, AGGRECO, IPTL*, na mambo mengine. Mimi naomba sana tuanje sasa hivi kuutumia umeme asilia, hilo ndilo angalizo langu la kwanza.

Mheshimiwa Spika, si hilo tu *TANESCO* ilianza kufa kidogo kidogo, ilianza mwaka 2005 kuchechemea, ikaanza kwenda, mwaka 2006 ikaanza kuzimia kidogo kidogo. Ilipofika 2007 ikafa, 2008 tumezika, hakuna tena *TANESCO*. Sababu kwa nini? Nimejiuliza, kwa nini *TANESCO* imekufa? Kuna mambo kadhaa ambayo yamefanyika lazima sasa tuyaaangalie upya tusaidiane kuyaangalia upya. Na hapa ndipo mahali ambapo sisi lazima tuzungumze tuwaambie wenzetu ili tusaidiane tufanye nini. Hilo ni angalizo lingine. Mimi binafsi niliona kwamba suala hili la mikataba mibovu ni mojawapo ambalo lilisababisha kufa kwa *TANESCO*. Wenzangu waliotangulia wamezungumza kwamba

kufa kwa *TANESCO* ni kwamba wamejitala wenye. Sasa mimi nasema mojawapo ni mikataba mibovu.

Mheshimiwa Spika, nyingine ni makandarasi wabovu. Kwa sababu kulitokea wakati *TANESCO* walikuwa wanawapata makandarasi kwa dharura lakini kumbe makandarasi wale ni wabovu. Hasa pale wanapotaka vitu vya dharura kwa mfano kutengeneza umeme, kuleta injini, makandarasi wale wanakuwa wabovu, sio wakweli. Kwa mfano, walipotaka kutengeneza umeme wa kituo cha Tegeta kwenda Mwenge, tulisikia wale makandarasi ni wabovu. Wale makandarasi hawakutengeneza vizuri na umeme ulikuwa sio mzuri, walitengeneza chini ya kiwango kiasi kwamba waliigharimu *TANESCO* shilingi milioni 81 walipe ili umeme uweze kuwaka, walifanya chini ya kiwango. Sasa makandarasi wabovu vilevile walituletea hasara *TANESCO* kuweza kuizamisha.

Mheshimiwa Spika, si hilo tu, tunalo suala la wizi, wizi wa mafuta. Kulitokea wizi wa mafuta Kigoma, Dar-es-Salaam, wafanyakazi sio waaminifu. Si hilo tu kulitokea na suala la mahesabu. Watu wanatoa hela tu bila mpango. Sasa tuangalie hayo maangalizo, wafanyakazi wasio na ujuzi wasio na utaalamu wa masuala ya pesa waangaliwe vilevile. Na suala lingine ni uwezo mdogo wa kiufundi. Kwa hiyo, haya yalifanya shirika kuchechemea, kuzimia, mpaka kuzikwa. Sasa tena tusije tukajiingiza katika masuala hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka kusema kwamba sasa hivi lazima twende na wakati. Kwamba Tanzania kila mwaka tunahitaji karibuni megawati 10 kila mwaka. Yaani kadiri tunavyokwenda kila mwaka mahitaji ya umeme yanaongezeka. Sasa lazima twende na wakati. Kwa hiyo, ni lazima tutafute mbinu ambazo tutafanya umeme uweze kurudi tena mahali pake. Na si tena suala la kulalamika tu, sasa nasema basi yaliyopita si ndwele tugange yajayo. Sasa tunafanya nini? Tunafanya nini baada ya matukio haya yote? Ndio maana tupo hapa, tunaukubali huu muswada ili tuurekebishe.

Sasa katika kuukubali kwangu, nashukuru kwamba mambo kadhaa nimeyafurahia yaliyorekebishwa. Mambo haya kwa kweli yatatuletea maendeleo katika masuala ya umeme kwa sababu muswada uliopita ulikuwa na miaka 76, niliona msemaji mmoja alizungumza juzi kwamba muswada uliopita ulikuwa na miaka 76, ultengenezwa mwaka 1931. Sisi tulikuwa na miaka mingapi wakati huo? Ni miaka mingi kabla hatujazaliwa. Mimi nilikuwa na miaka 15 kabla sijazaliwa, je, wenzangu vijana walikuwa na miaka mingapi? Mingi tu, na mpaka sasa unapata akili una miaka mingapi? Mingi tu! Kizazi kwa kizazi kimepita, kwa hiyo, ulikuwa na mapungufu mengi tu.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi inabidi tuukubali mradi na hivi ulivyoletwa mezani sisi tupo tayari kuukubali na kuusahihishwa. Mimi binafsi kwa kweli nimefurahishwa na vipengele kadhaa ambavyo vimesahihishwa. Kwa kuuangalia muswada huu nimeona kuna masuala manane ambayo kwa kweli yataleta tija katika nchi hii. Kwanza bei ya umeme kupungua kwa maana ya *capacity charge* hasa katika baadhi ya maeneo kwa sababu pengine wafuaji umeme wengine watapeleka moja kwa moja kwa *EWURA* na mdhibiti wa bei atakuwa *EWURA*. Pale *TANESCO* tena hatakuwa ndani ya eneo lile.

Hiyo naona inaweza ikasaidia masuala mazima ya kupunguka kwa *capacity charge*. La pili ni kushindanisha kwa kibiashara kati ya shirika na shirika. Hii itakuwa nzuri vilevile kwa sababu hiyo itawafanya wengine wapunguze masuala mazima ya *capacity charge*.

Mheshimiwa Spika, halafu lingine ambalo limefurahisha katika Muswada huu mpya ni suala la umeme vijijini kifungu kipy Cha 39(4), hilo ndilo suala ambalo sisi wote wananchi tulikuwa tunalisubiri. Sisi Wabunge pamoja na wananchi wengi ambao tupo vijijini kifungu cha 39(4), kwa kweli ni kifungu kizuri sana.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kusambazwa kwa umeme vijijini, halafu kingine ambacho kilinifurahisha ni haki ya kumlinda mlaji akiharibikiwa na chombo cha umeme, hicho ni kizuri sana. Vingine ni mwekezaji akihitaji umeme, nikipitisha umeme atalipwa na lingine ni kwamba watu binafsi wataruhusiwa kufua na kusambaza umeme. Zamani kilikuwa kinawazuia kitu kama hicho. Ibara ya 7 ilikuwa inawazuia watu binafsi kutengeneza umeme. Sasa hivi inaruhusu kwa sababu wapo vijijini watu binafsi wanataka kutengeneza umeme lakini inawazuia, sasa hivi inaruhusu mtu binafsi kutengeneza.

Katika sehemu mbalimbali vijijini kuna watu binafsi wanaweza kutengeneza umeme sehemu nyingi. Kwa mfano, Mtwara kuna kampuni moja inaitwa *ARTUMAS*. *ARTUMAS* ina uwezo mkubwa wa kutengeneza umeme wa kupeleka Lindi na Mtwara na yenye we inasema inaweza kupeleka Tabora mpaka Mwanza. Lakini ilikuwa inazuiliwa na kipengele cha 7 cha Muswada wa zamani kinachowakataza watu binafsi kusambaza umeme. Lakini sasa hivi watu binafsi wataruhusiwa kusambaza umeme baada ya kipitishwa muswada wa sheria hii kwa sababu sheria inaruhusu na kwamba ile sheria ya kipengele kilichoandikwa sasa hivi kitaruhusu kuwasambazia watu umeme vijijini.

Kwa hiyo, *ARTUMAS* yenye we inavyozungumza haitokuwa na *capacity charge* kitu ambacho kwa kweli kitawavutia wananchi wengi. Badala ya kutoza umeme kwa shilingi 500,000, kuweka umeme kuanzia shilingi 500,000, itakuwa inaweza kwa shilingi 60,000, 70,000 mpaka 90,000 badala ya kuweka kwa shilingi 500,000. *ARTUMAS* ina jenereta sita na ina uwezo wa kutengeneza megawati 12 na uwezo wa kutengeneza umeme na kusambaza Mtwara na Lindi na ina uwezo wa kutengeneza nyumba 40,000 kwa kuanzia kwa miaka minne. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba ndugu zangu Wabunge tuupitishe huu Muswada ili na sisi Kusini tuweze kupata umeme kwa kumtumia huyu mtu aitwaye *ARTUMAS* ambaye amedhamiria kabisa kueneza umeme katika mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kutoa shukrani zangu kwa dhati kwa kunipa nafasi hii ya kuzungumza, nasema asante sana. (*Makofî*)

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nami kupata nafasi hii ili nichangie katika Muswada huu. Kwanza kabisa napenda kuwapongeza sana Waziri pamoja na Naibu Waziri, wameingia na wamechangamsha sana sana Wizara hii, unaweza kusema kwamba unaona matokeo ya *boys II man*, kwamba sasa hivi ndiyo wanakua. Pia nawapongeza wataalamu walioletea na kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu nionavyo mimi ni ukombozi mkubwa kwa mikoa yote inayoishi pembezoni. Kwa mfano, wenzetu wa Kigoma, Malagalasi ukiangalia hawangeweza kuendeleza vyanzo vyao vya umeme bila ruhusa ya *TANESCO*. Kwa hiyo, ukija Njombe ukienda mpaka Ruvuma huko kuna vyanzo vingi vizuri ambavyo vilikuwa vinaendelezwa na wamisionari lakini hawawezi kufanya biashara au hawawezi kueneza kwa sababu ya ukiritimba wa *TANESCO*.

Ukija Sumbawanga wenzetu wanalamika sana kwamba umeme wao nao una matatizo makubwa, katika mwaka mmoja umekatikati, walituambia hapa mara elfu moja. Sasa hii yote ni kuonyesha kwamba *TANESCO* wamezidiwa na kama wamezidiwa wakiwa na ukiritimba, njia pekee ya kukwamua au kuendeleza nchi ni katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na Muswada unaoruhusu watu wengine kushiriki pia katika kuzalisha na kusambaza umeme.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wengi wameelezea juu ya vyanzo mbalimbali vya umeme na mwenzangu aliyepita sasa hivi amezungumzia juu ya vyanzo vya *Mnazi Bay Mtwara*. Sasa mimi kwa kuwa ni mdau ambaye nipo katika *Government Negotiating Team (GNT)* inayofanya mazungumzo na kampuni hii ya *ARTUMAS*, halafu pia ninahudhuria vikao wanavyojadili watafanya nini katika kampuni ya *ARTUMAS*. Kwa hiyo nina uhakika wa mambo mengi zaidi yatakayotokea kwa mikoa hii ya Mtwara na Lindi, naomba nisahihishe kidogo *ARTUMAS* sio mtu ni kampuni, hivyo, ni taasisi, ni kampuni ambayo inachimba gesi na wakati huo huo kutengeneza.

Sasa hawa wana uhakika wa mambo wanayoyafanya. Kwanza *ARTUMAS* wana uhakika kwamba wanaweza kutumia teknolojia yao ili kuingiza umeme katika nyumba za nyasi au zilizoezekwa kwa majani. Wamesema kwamba yale makondakta yao ni madogo madogo yenye nguvu ndogo kiasi kwamba hata unaweza kushika waya usidhurike.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wanataka wao kutumia teknolojia ili waweze kusambaza kwa watu wengi zaidi na kwa kuanzia wako tayari kusambaza katika nyumba au katika mawakala 47,000 kwa mikoa ya Mtwara na Lindi. Sasa hili ni jambo la faraja kubwa kwa wananchi mikoa ile.

La pili, wengi wamezungumzia kwamba hawa hawatatumia *capacity charge* watatumia *tariffs* zinazowekwa na *EWURA*. Kwa hiyo, kwa kuongeza wateja gharama zao zitarudi namna hiyo. La tatu ni kwamba bei ya kuunganisha laini ya umeme wameiweka chini.

Kwa sasa hivi *TANESCO* wanatoza bei ya kuunganisha umeme katika nyumba za watu shilingi 467,000 na *ARTUMAS* watakuwa wana-charge shilingi 60,000 mpaka 80,000 ili kuhakikisha wanaweza kuwashudumia wananchi wengi zaidi.

Ndugu zangu suala hili la *capacity charge* hata mimi lilikuwa linanisumbua na nimelifanyia utafiti, *capacity charge* inatozwa katika nchi tatu tu duniani, nchi hizo ni Nigeria, Angola, na Tanzania. Kwa upande wa Nigeria na Angola tunaelewa kwa sababu kule nchi hizi zina ulaji mkubwa sana. Kwa sababu Nigeria mtu atastaafu, ataacha kazi

basi *capacity charge* ile inaendelea kumlipa na ndiyo maana wameing'ang'ania, na Angola vile vile.

Sasa sisi Tanzania mchezo huu tumeanza lini? Yaani unajiuliza kweli, hivi haiwezekani kwamba kuna watu wametoka kule *IPTL* wamestaafu bado wanalipwa hela, sasa kuna baadhi ya mambo mengine tunakuja kugundua siku hizi unajiuliza jamani vipi? Kwa hiyo, mimi naiona *capacity charge* kwamba njia moja ya ulaji wala haina maana yoyote.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Mheshimiwa Waziri kwamba umetoa kabisa suala la *capacity charge*, ikiwezekana hizi *capacity charges* zilizopo kwa kina *RICHMOND, DOWANS, IPTL, SONGAS, AGGREKO*, Serikali itafute kila njia ili ziweze kufutwa, tunawajengea ulaji watu baadaye tukija kuchunguzana ndiyo tutakuja kuona nani aliyekuwa anakula. Je, kwa nini Uingereza au Kenya hawana *capacity charge*?

Mimi naamini kabisa kwamba wenzetu wengi katika mikoa mingine watauunga mkono Muswada huu. Kama nilivyosema toka mwanzo muswada huu ni mkombozi kwa sehemu zile ambazo ziko pembezoni kwa sababu sasa hivi zitakuwa na uhakika wa kupata umeme wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia sisi tunaotoka Kusini karibu kila kitu, elimu duni, afya duni, maji duni, sasa jamani umeme huu hebu utuinue tuwe juu na sisi kwa sababu umeme ule wa Mtwara siyo tu utanufaisha Kusini. Kuna megawati 300 za ziada ambazo zitaunganishwa kwenye gridi ya taifa. Kwa hiyo, umeme huu utafika mpaka kwenye migodi yote ya Mwanza, Arusha, Tabora, kila mahali umeme wa Mtwara utakwenda.

Mheshimiwa Spika, katika kumalizia nataka kusema kwamba ushindani kibashara ni kitu kizuri sana. Tumeona baadhi ya mashirika yetu baada ya kubinafsishwa kwa mfano *TBL* sasa hivi inazalisha bia za kila aina na inafanya kazi vizuri, *TCC* nayo imefanya kazi vizuri sana na hivi karibuni shirika letu la umma jipya la *TBC* au zamani lilikuwa *TVT*. *TVT* wakati inaanishwa ilikuwa inashindana kweli kweli na *ITV*, *Chanel Ten* na *DTV* lakini leo *TBC* ambalo ni shirika la umma sasa hivi linaongoza kwa kutoa huduma nzuri.

Kwa hiyo, na *TANESCO* nayo tukiipa ushindani naamini itatoa huduma nzuri bila mizengwe hii inayotokea sasa hivi. Lakini ningombaa wakati tunafanya kazi hii Mheshimiwa Waziri nikirudi Jimboni kwangu katika huu mradi huu wa *ARTUMAS* tafadhali naomba toka Nyangao umeme uende kijiji cha Mkungu, ukitoka Mkungu-Mkwera-Chipite-Nanganga- Nkang'u-Mumburu-Nangoo-Liputu-Ndanda-Mwena-Chikundi-Chigugu-Mandiwa-Chikukwe-Liloya-Namakongwa-Milambo na Masasi.

Mheshimiwa Spika, naomba vijiji hivi viwepo kwenye rekodi kabisa ya Mheshimiwa Waziri ili ahakikishe kwamba watakapokuwa wanakamilisha tafadhali tusikose umeme kwa sababu njia kuu ya umeme ndiyo inapita katika vijiji hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nawatakieni kila la heri, Muswada huu tuupitishe vyema ili utekelezaji wake uweze kuanza mapema iwezekanavyo wananchi wengi waweze kupata umeme hasa wa vijijini. (*Makofi*)

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana asubuhi hii ya leo kunipa nafasi na mimi niungane na Wabunge wenzangu kuchangia Muswada ulio mbele yetu.

Lakini kabla sijaanza kuchangia naomba kwanza niipongeze sana Serikali pamoja na Waziri wa Nishati na Madini na wataalamu na pia Kamati iliyosughulikia Muswada huu kwa marekebisho makubwa ambayo yamefanyika na hivyo kuboresha sana Muswada huu ukilinganisha na ule Muswada wa awali amba tulipewa. Kwa hiyo, napenda niwapongeze kwa kufanya marekebisho na kuleta Jedwali la Marekebisho ambalo limezingatia katika mchango wangu.

Aidha, napenda niipongeze Kamati pamoja na Waziri kwa kuongeza vipengele vipyta ambavyo vimeboresha zaidi Muswada huu. Moja ni lile linalohusu *TANESCO*, Muswada wa awali ulikuwa hakuna mahali popote ambapo *TANESCO* ilitajwa lakini katika Muswada huu angalau *TANESCO* imezingatiwa, napenda niwashukuru sana. Kitu ambacho sijaelewaa vizuri ni kwamba majukumu ya *TANESCO* pale hayakueleza vizuri, ningependa nimwombe Waziri mhusika ajaribu kuangalia *TANESCO* inapewa wajibu gani ama majukumu gani katika sheria hii tunayotunga.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo naomba nitoe maoni ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Kondoa Kusini kuhusu Muswada huu na yatakuwepo maoni hayo machache na nitakwenda aya kwa aya. Kwanza, tuchukue ukurasa wa 16 wa Muswada wenyewe aya ya 15(7) inayozungumzia juu ya utoaji wa taarifa za ajali katika shughuli za wamiliki wa leseni. Inasema katika eneo hili kwamba kutakuwa na taarifa za aina mbili za ajali, moja ni ya vifo, kifo kikitokea katika shughuli za mmiliki wa leseni ikitokea taarifa inatolewa mara moja kwa mamlaka inayohusika.

Lakini kipengele cha pili ama aina ya pili ya ajali ni zile ambazo hazitawezza kusababisha kifo. Inasema hizi ajali zitaripotiwa kwa mwaka. Wapiga kura wangu wanasema kwa kweli hiyo ni dosari kwa sababu kungoja kuripoti ajali kwa mwaka mara moja nafikiri sio sahihi na wanachopendekeza ni kwamba ajali ni ajali, iwe imesababisha kifo ama kuumia ni lazima zitolewe taarifa mara moja. Kwa mfano, walikuwa wanasema hivi mtu akiumia akakatika mguu au mkono tunasubiri mpaka mwaka upiti ndiyo tupeleke taarifa? Taarifa zinatakiwa zipelekwe. Kwa hiyo, naomba kuungana na wapiga kura wangu kusema kwamba ajali zitolewe taarifa mara moja kama ilivyo kwa ajali inayosababisha kifo ama vifo.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni lile ambalo Wabunge wenzangu wameligusia suala la gharama ya kuunganisha umeme. Nimsaidie tu Mheshimiwa Waziri kwamba hili linazungumzwa katika ukurasa wa 21 wa Muswada na ni aya ya 23(1)(c). Aya hii inaweka masharti kwamba kila mteja anapotaka kuunganishiwa umeme lazima alipie gharama ya kuunganishiwa umeme. Na hapa wachangiaji waliotangulia wamesema kwamba gharama hiyo ni kati ya shilingi 400,000 mpaka 500,000 iwe vijijini iwe mjini,

gharama ni hiyo. Wapiga kura wangu wa Jimbo la Kondoa Kusini wanasesma kwa kweli huu ni mzigo mkubwa sana labda nivitaje na vijiji ambavyo walitoa maoni wakasema sisi tumekwishapewa umeme hapa vijijini ama katika vijiji vyetu lakini wananchi wameshindwa kuunganisha umeme katika majumba yao kwa sababu gharama ni kubwa mno.

Vijiji hivyo nivitaje kwa sababu ya kuweka kumbukumbu. Vijiji hivi ni Mondo, Kelema Maziwani, Jenjeluse, Goima, Songolo, Hamai, Chandama, Soya, Mrijo Juu, Mrijo Chini na Oloboroti. Kama nilivyosema hivyo hapo awali kwamba hivi vijiji tayari vilikwishapatiwa umeme kuitia *TANESCO* lakini ni wachache sana waliounganisha umeme kwa sababu gharama ya kuunganisha ni kubwa mno. Kwa maoni yao wamesema hatuoni tunanunua nini wakati tunapochangia gharama ya kuchangia umeme kwa sababu katika sheria hii inaonyesha kwamba anayekuunganishia umeme ni mmiliki wa leseni anayesambaza umeme katika eneo lako.

Sasa kinachogharamiwa pale ni nini maana sheria inatamka kwamba vifaa vyote vitakuwa vya mmiliki wa leseni. Na wapiga kura wangu wanasesma hivi sisi ama mteja anahusika kulipa umeme anaotumia, sasa hii gharama ya kuunganisha unalipia kitu gani, haieleweki. Kwa hiyo, ombi lao kama inawezekana wanaomba gharama hii ingeondolewa moja kwa moja. Na mimi napendekeza katika Muswada huo eneo hilo ama aya ya 23(1)(c) ingeondolewa moja kwa moja. Hiyo ndiyo itarahisisha hata wananchi wa vijijini waweze kuunganisha umeme kwa urahisi. Kama haitaondolewa tutapeleka umeme bure vijijini hakuna atakayetumia kwa gharama hiyo ya kuunganisha kwa 400,000 ama kati ya 400,000 na 500,000 hiyo ndiyo uhakika na mimi nitasimama kwenye vifungu baadaye kama sitapata jibu zuri kwa hili.

Eneo la tatu ambalo nalo lipo katika Muswada huu linahu malipo ya awali kwa mteja kabla hajaunganishiwa umeme, hiyo inaitwa *deposit*. Jamani hawa wateja watalipa gharama ngapi? Kabla ya kuunganishiwa umeme *deposit* ina kazi gani, sijaelewa na wananchi wangu kwa kweli kabisa na naamini Watanzania wote hawataelewa hii *deposit* ina maana gani na hasa hasa kwa sheria hii. Sheria hii imebainisha vizuri sana majukumu ya mteja na mmiliki wa leseni. Endapo patatokea uharibifu wa vyombo vinavyotumika kufikisha umeme kwa mteja na imeweka bayana kabisa namna ya kulipiana fidia, sasa unataka *deposit* ya nini? Na kitakuwa kiwango gani, naamini kabisa kwamba kiwango cha *deposit* kitakuwa kikubwa zaidi kuliko cha kuunganisha umeme kwa sababu kinachoelezwa hapa ni kwamba eti hiyo ni tahadhari unaweka ili ukiharibu haribu ama mteja akiharibu vifaa pale iweze kufidia. Lakini sheria iko bayana kwamba mtu akiharibu vifaa mteja ama mmiliki akileta hasara katika vifaa vya mojawapo kuna utaraibu za kulipana. Sasa hiyo *deposit* ina kazi gani? Wapiga kura wanasesma jamani kama mnataka kuwasaidia na kama kweli mtafikisha umeme vijijini suala la *deposit* lifanyiwe kazi na ikiwezekana liondolewe ili kupunguza mzigo wa kuunganisha umeme kwa mteja kabla hajapata umeme.

Mheshimiwa Spika, nilizungumzie eneo la mwisho, nalo linahu Ibara ya 39(4), hiyo imeongezwa katika Jedwali hili la Marekebisho. Sasa naomba kwa ruhusa yako uniruhusu nisome kidogo tu hiyo sehemu: “*For the promotion of the national energy*

*policy in relation to rural electrification every licensee shall be required to supply electrical energy to local communities where electrical supply installation are located or along transmission lines.* “ Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, sehemu hiyo ni nzuri na baadhi ya Wabunge waliotangulia kuchangia walisifia sana ongezeko la sehemu hiyo. Maana yake ni nini? Kwa kifupi ni kwamba kuzingatia hiyo sera ya Nishati kwamba umeme unapopita katika vijiji ni lazima vile vijiji vipatiwe umeme.

Kwa kuwa bila shaka sheria yetu ya *TANESCO* ilikuwa na mapungufu, umeme ulikuwa unapitishwa kutoka eneo moja hadi eneo lingine lakini vijiji njiani havipatiwi umeme, nyaya zinapita juu ya vijiji lakini imekuwa kama picha pale wanachari hawanufaiki na umeme unaopita kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. Mfano katika jimbo langu la Kondo Kusini umeme kupitia mradi wa *electricity II* ulipitishwa kutoka Kondo Mjini kwenda Kibaya, Kiteto na katikati pale kulikuwa na vijiji vingi. Ama viro vijiji vingi mpaka sasa lakini kwa kuwa sheria ya *TANESCO* ilikuwa na upungufu, vijiji hivyo havikupatiwa umeme. Sasa katika sheria hii ni lazima mmiliki wa leseni anayepeleka umeme katika maeneo ya vijiji pale umeme unapopita lazima vipatiwe umeme.

Sasa kwa kuwa kosa hili lilifanyika wakati wa kutekeleza ule mradi, vijiji vifuatavyo ambavyo havikupatiwa umeme navyo ni Waida, Pongai, Diho, Mirambo, Igunga, Madaha, Mapango, Mwailanje, Nkulari, Songa-Mbele na Isusumia, hivi vimepititiwa na umeme wa *TANESCO* lakini havikupatiwa umeme. Kwa kipengele hicho ama kile nilichosoma katika Jedwali la Marekebisho, sasa hivi vijiji vinawajibika kupata umeme. Kwa hiyo, namalizia kwa kusema kwa kuwa huku nyuma kosa lilifanyika, tunaomba sheria itakapopitishwa basi hayo makosa yarekebishwe na hivi vijiji vipatiwe umeme haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, nimemaliza mchango wangu, ahsante sana kwa kunipa nafasi naunga mkono Muswada huu. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Paschal C. Degera na niamwita sasa Mheshimiwa Aziza S. Ally, atafuatiwa na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis na wakati huo huo simwoni Mheshimiwa Janeth Mourice Massaburi. Kwa hiyo, atakayefuata ni Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, ajiandae. Mheshimiwa Aziza S. Ally karibu!

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Muswada huu. Awali ya yote naomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba nichukue nafasi hii pia kutoa pongezi kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia hasa nikizingatia Bwana Said Nzori kwa kuweza kutusaidia zaidi kwa muda mrefu ambao tumemsumbua ili aweze kutusaidia kutufafanulia, na ametufafanulia vizuri sana vipengele vya Sheria hizi, kwa kweli

tunampongeza sana. Bila ufanuzi kwa kweli tusingeweza kuelewa vizuri kama mwanzo tulivyokuwa tukipata taabu katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba dhana nzima ya kupeleka umeme vijijini au kuleta Muswada huu ni dhana nzuri kabisa lakini kama dhana hii itawenza kutekelezeka na kufuatwa. Leo au keshokutwa tutapitisha Muswada huu, kwa hiyo, wananchi wengi watakuwa na imana ya kuelewa kuwa umeme wataupata bila tatizo lolote, maana miji mingi na vijiji vimeweza kuendelea kwa kupata barabara, umeme na afya. Kwa hiyo, mojawapo watakaopata umeme watakuwa na imani kubwa ya kuwa na maendeleo. (*Makofti*)

Lakini suala zima ambalo linanitia wasiwasni *TANESCO*. Kwa kweli napenda niwe muwazi, lazima tukubali *TANESCO* ibadilike, *TANESCO* iwe ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya lakini ikiwa kama ilivyo sasa itakuwa ni tatizo.

Ninavyouangalia Muswada huu *TANESCO* imekwishakuwa katika shirika la kibashara na kama limekuwa tayari katika shirika la kibashara ni lazima libadilike na lazima kuwe na ushindani. Lakini kwa kuwa ni mwanzo nina imani kuwa tumelibeba na katika kubebwa kwake ndiyo maana halikuwepo katika tenda. Kwa hiyo, tumeona ni shirika ambalo tunaweza tukaliinua likapewa chanzo na likafanya kazi. Lakini napata wasiwasni mmoja, hatukatai kuwa limekwishawahi kusaidiwa liwe la kwanza katika usambazaji wa umeme, lakini je, tukiangalia mbele litawenza kufanya kazi sawasawa? Kitu gani ambacho kinakuwa ni kinga katika Serikali ya kuweza kubanana na *TANESCO* ambayo tayari ni shirika la kibashara? Hatuna mkataba ambao unaonesha *TANESCO* tunawapa muda wa miaka mitano ili waweze kusambaza umeme vizuri. Tunawapima, tunaona kuwa wamefanya kazi yao vizuri na wameendelea, kwa hiyo, tunakubaliana kwa kuwa kazi yao ni nzuri basi waweze kuendelea.

Nadhani tatizo hilo litatusumbua baadaye kwa sababu wanaofanya kazi ni binadamu, kwa hiyo, ni lazima tuwape na wao *challenge* ya kuwaambia kwamba mna mkataba wenu kwa miaka mitano. Miaka mitano mtakapofanya vizuri mtawenza kuendelea, lakini tukiacha hivi hivi waziwazi tukaendelea kubebana nina imani kuwa huko mbele tunakokwenda tatarudi tena kwenye Bunge hili na kuweza kuwaambia ni lazima tuwe na mkataba wa mashirika haya.

Mheshimiwa Spika, kutokuwekeana mkataba kutatuletea shida kwa sababu sasa hivi nikiangalia mwananchi yejote anao ushahidi wa kuona kwamba anapohitaji umeme uende nyumbani kwake kwanza atachukua miezi miwili au hata mitatu pamoja na kulipia ile 400,000/=. Lakini atachukua miezi miwili hata mitatu mpaka afungiwe umeme nyumbani kwake.

Lakini kuna tatizo lingine, tatizo hilo ni la nguzo. Mteja yeye anahitaji kufungiwa umeme ndani ya nyumba lakini bado anatakiwa kugharamia nguzo zipatazo 6 au 7 mpaka anavuta umeme nyumbani kwake. Zile nguzo tu peke yake atakuwa amekwishashalipia zaidi ya shilingi milioni 2 au hata 3. Lakini anapochelewa kulipa umeme hawakumbuki hata kwamba yule alilipia zile nguzo mpaka kufika nyumbani kwake kuvutiwa umeme,

hilo wao wala hawalifikirii. Lakini bado hakuna sehemu yoyote anayofidiwa ya kusema kuwa aliingiza nguzo zile kwa hiyo lazima arudishiwe kiasi chake ambapo kazi ile ilikuwa ni ya *TANESCO*. Lakini bado ye ye anakuwa kama ameisaidia *TANESCO* kuvuta nguzo mpaka zimefika nyumbani kwake.

Lakini bado hapa katikati kuna nyumba nyingine ambazo zinavutiwa umeme kutokana na zilezile nguzo ambazo amezilipia huyu mteja ambaye yuko mbali, hawa nyumba za katikati zote zinavutiwa. Kwa hiyo, yule mteja mwenyewe anakosa ule umeme wa nguvu ambao anauhitaji kwa sababu ye ye ni lazima atapata nguvu ndogo, hawa wengine katikati tayari wamekwishavutiwa umeme katika nyumba zao. Ndiyo hilo ambalo ninalolisema kwamba ni lazima tukubaliane kwamba na wao wawepo ndani ya mkataba ambao utawa ni makubaliano kati ya *TANESCO* na Serikali ingawa na *TANESCO* tayari limeshakuwa shirika la Serikali lakini tayari ni shirika la biashara.

Katika biashara ni lazima kuwe na ushindani wa namna gani ambayo tukiamua kama ni biashara twende kwenye biashara, tuache suala la kusema ni shirika la Serikali lakini limo kwenye biashara lakini tuwe na utaratibu wa kuwabana. Mteja vitu kama hivi atapata shida sana kwa kuweza kuvilipia kwa sababu atashindwa namna gani sehemu yake ya kwenda kulalamika ingawa sasa hivi ndiyo asilimia kubwa inayoweza kufanyika na wananchi wengi wanapata shida.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna suala lingine ambalo nimelifikiria la kusema hatuukatai Muswada huu tunaupitisha, lakini tunaangaliaje utumiaji wa umeme wa *solar*? Sasa hivi kuna sehemu nyingine vijijini kuna mtu tu ana *solar* yake, amenunua na anavuta umeme na anaweza kupata mahitaji kwenye nyumba yake.

Kama kweli Serikali ina imani na inapenda wananchi waweze kuendelea kwa nini isiangalie na kufikiria suala la kutoa kodi kwenye *solar* ambazo zitaingizwa ndani ya nchi? Kwa sababu hata huu utaratibu wa kuanza kuvutana kusema *TANESCO* ifanya hivi na vile lakini mtu akishafunga umeme ndani mwake, akishafunga waya na akaweka *solar* yake, anao uwezo wa kuhudumia nyumbani kwake au hata upande wa sehemu nyingine kwa watu wake wawili au hata watatu wakaweza kupata umeme wa *solar* na vijijini. Watu wengi hawahitaji matatizo ya kuanza kuvutana na kucheleweshana.

Mheshimiwa Spika, kama *solar* itatolewa kodi wananchi wengi watapenda zaidi kununua *solar*, hata huu umeme ukiwa bado haujapita wananchi wale watapata *solar* iweze kuwasaidia kwa haraka zaidi kuliko kusubiri huu umeme ambao nina imani hautawenza kufika kwa wakati. Huu ndiyo ukweli kwamba tuseme baada ya miaka tuletewe hapa Bungeni kuambiwa baada ya Sheria hii kuipitisha leo muda wetu wa miaka mitatu tumetembea vijiji vyote kukamilisha umeme. Hii kwa kweli nina imani kuwa itakuwa si rahisi kwa sababu kuna mambo mengi ambayo tunayaona hayakuweza kutekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili kwa kuongea na Waziri wa Fedha ili angalau *solar* ziweze kupunguziwa pamoja na jenereta kwa wale wengine ambao wana uwezo wa kutumia majenereta sehemu mbalimbali ziweze kutolewa kodi.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna suala lingine ambalo Sheria yetu kwa kweli hajawenza kuonyesha kuwa mteja anapoharibikiwa na vifaa vyake ni muda anaohitajika kuweza kulipwa vile vifaa ambavyo vimeharibika. Tunaona sasa hivi umeme unawaka na kuzimika, kuna watu ambao vitu vyao chungu nzima ambavyo vinaharibika lakini sheria ionyeshe kama ni mwezi mmoja au miwili au mitatu uwepo kabisa utaratibu ni miezi miwili mteja anatakiwa alipwe vifaa vyake ambavyo vimeharibika. Na kama miezi miwili bado hajalipwa huyu mteja awe na uwezo wa kwenda Mahakamani kulishitaki shirika ili aweze kulipwa vile vitu ambavyo vimeweza kuharibika. Mimi nafikiria hilo ambalo litaweza kumsaidia mteja lazima katika Sheria mbalimbali na zenyewe ziwe zinamwangalia yule mtumiaji wa mwisho, zisiwe tu sheria zinazoangalia kwa yule mteja lakini zisiwe zinaangalia kwa mwekezaji au Serikali lakini bado pia zimwangalia mteja kuwa baada ya miezi miwili anatakiwa kulipwa ili mteja naye aweze kuelewa miezi miwili mimi nakwenda zangu mahakamani kwenda kulishitaki shirika halijawenza kunilipa. Nina imani hiyo itaweza kutusaidia kumpa kile ambacho mtu anakidai kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine la *TANESCO*, kwa kweli upunguzaji wa ada zile ambazo anatakiwa mteja kupunguza kila wakati kutumia nina imani ni lazima tuweze kuziangalia kumpunguzia mwananchi. Tuangalie kwanza kipato cha mwananchi yaani katika mshahara wake anaweza kwa mwezi akapokea shilingi 80,000/=, anahitaji kulipia umeme, maji, ada ya mtoto wa shule na chakula cha kula nyumbani. Sasa ukiangalia umeme analipia shilingi 20,000/=, maji kama hivyo wanavyoomba kila siku *EWURA* iweze kuwaongezea. Kwa hiyo, wanahitaji na wao wafike hata shilingi 20,000/=, yule mwananchi atabaki na shilingi ngapi?

Maana tukiziangalia zote hizi zinasumbua lakini bado *TANESCO* leo ukiwaambia watoke kutoza umeme au wasiwasambazie umeme katika migodi hawawezi kukubali kwa sababu asilimia kubwa wao wanaangalia katika migodi, ni sehemu yao ambayo inawainua zaidi kuweza kuzalisha umeme na kupata kipato kikubwa zaidi. Kama kule ni migodi yetu kila siku inaongezeka na wao wanazidi kusambaza umeme, kama wanazidi kusambaza umeme kwa nini isifidie kwa mwananchi huyu wa kawaida kwa kuwasha taa mbili au tatu ziweze kumfidia angalau alipie umeme kwa kiasi kidogo zaidi.

Kwa kweli mimi ninaseme angalau basi yule mwananchi afaidike na ile migodi ambayo ipo katika nchi yetu na ukiangalia *TANESCO* na Madini wote wako Wizara moja, kwa hiyo, waangalie zaidi mwananchi ufaidikaji wake uwepo wapi. Huku kwenye migodi wao wenyewe wanaweza, tena nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri wakati anamaliza aweze kutufahamisha kwenye migodi kwa muda wa mwezi mmoja tu wanapata kiasi gani.

Tukiangalia ule muda wa mwezi mmoja kipato ambacho wanakipata, nina imani mwananchi hata wangesema alipe umeme wake shilingi 80,000 au 10,000 kwa mwezi wala isingembana zaidi kwa sababu wangemfidia na yeye kule katika migodi ambako wanasantaza kila siku. Na bado tuangalie ile migodi ni kila mwaka au baada ya miaka miwili inapatikana migodi mingapi? Kwa sababu inapatikana migodi mbalimbali. Kama

inavyopatikana na wao huku wanamzidishia mwananchi kuweza kulipia umeme mkubwa zaidi. Mimi nafikiri migodi jinsi inavyofunguka mingi mwananchi basi apunguziwe kulipia ule umeme kama kweli tutaliangalia suala hili na kuweza kumsaidia mwananchi wa kawaida. Nina imani kuwa Mheshimiwa Waziri lazima atalizungumzia jambo hilo ili tuweze kulifahamu vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo na ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Aziza S. Ally nakushukuru sana. Katika orodha yangu nilikuwa na Mheshimiwa Benito W. Malangalila lakini ameniandika kwamba yeche atatoa mchango wake kwa maandishi. Kwa hiyo, sasa naendeleo kama nilivytamka awali, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Janeth Mourice Massaburi hayupo! Atafuata Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri na wakati huo huo Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge ajiandae.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Lakini kabla ya yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Naibu Waziri na timu yake yote ya wataalamu kwa juhud zao zote zisizokata tamaa ambazo mmekuwa mkizifanya mpaka hii leo Muswada huu umeingia Bungeni na kuna kila dalili kwamba Waheshimiwa Wabunge wataukubali na kuupitisha.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wote wanalia hawana umeme kutoka Kaskazini ya Tanzania wanalia hawana umeme, Kusini hawana umeme, Mashariki hawana umeme na Magharibi hawana umeme lakini hata kule Pemba hawana umeme. Kwa kipindi kirefu kuna mgawo usiotabirika wa umeme, kwa kweli ni kiza kitupu na baya zaidi ni kwamba kwa muda wa mwezi mzima uliopita hata petroli na dizeli zilikuwa hakuna hivyo ni magari machache tu yalikuwa ndiyo yanayotembea. Hiyo ndiyo Tanzania!

Mheshimiwa Spika, wataalamu wa umeme wanasema tafsiri halisi ya maendeleo kitaalamu si kisia, ni kuangalia jinsi gani nchi inatumia umeme, iwe nchi au mtu binafsi katika shughuli zake za kila siku. Msumbiji kwa mfano kwenye kiwanda kimoja tu wanatumia megawati 900, hapa Tanzania nasikia kwamba sasa hivi ndiyo tumefikisha megawati 1000 lakini malengo ni megawati 4000. Kwa hiyo, tupo katika asilimia 25 tu ya malengo na katika hiyo labda ni 1% tu ndiyo iko vijijini, hivyo utaona ni kiasi gani Tanzania tuko nyuma kimaendeleo kwa tafsiri hii ya wananshati.

Mheshimiwa Spika, madhumuni makubwa ya Muswada huu kwa ujumla ni kubinafsisha umeme ili uweze kuenea katika sehemu zote za nchi yaani mijini na vijijini. Kwa kufanya hivyo kunaandaa mazingira ambayo sekta ya umeme itafanya kazi katika soko huria. Kwa hiyo, matarajio ya Watanzania ni kwamba baada ya Muswada huu kuitishwa na kuanza kufanya kazi kero hizo ambazo kabla zilikuwapo au upungufu huo utaondoka.

Mheshimiwa Spika, *privatization* ya umeme ambayo tunasema kwamba si *fully* ni *partial* kwa sababu TANESCO iko hapa, TANESCO ni shirika la Serikali. Ukitazama *concept* yake utaona labda ni nzuri kwa sababu kama nilivyosema Tanzania yote haina umeme. Lakini sasa hivi Watanzania wameanza kuwa na wasiwasi. Katika baadhi ya

maamuzi yetu Bungeni, nataka nitoe mfano kidogo. Wakati wa Bajeti hii ya 2007/2008 ilipokuwa inasomwa tulielezwa kwamba ni nzuri na italeta maisha bora kwa Watanzania wote na Waheshimiwa Mawaziri wakazunguka nchi nzima kuisifia bajeti hii lakini leo hali halisi inaonekana jinsi maisha yalivyokuwa magumu, vyakula ni ghali mno, mafuta yamepanda bei, kwa ujumla Mtanzania sasa hivi hana maisha bora kabisa.

Kwa hiyo, matarajio ya wananchi ni kwamba labda ubinafsishaji wa umeme unaweza kuleta suluhisho au jibu la matatizo yao inawezekana ikawa siyo hivyo. Sasa hivi tunasikia kwamba yako baadhi ya makampuni ambayo yanazalisha umeme wako *stand by* wanasubiri Sheria hii ipitishwe ili na wao waingie. Sasa kama hivyo ndivyo inaweza kuwa hii ni janja tu ya nyani lakini lengo wanalijua wenyewe mafisadi.

Mheshimiwa Spika, mimi nashangaa kwa nini *TANESCO* au Serikali isubiri mpaka *TANESCO* imekuwa taabani iko *ICU* kama wanavyosema Waheshimiwa Wabunge. Sasa nasema ndiyo tunaanza kubinafsisha sekta ya umeme. Kwa nini hali ya *TANESCO* isiboreshwe kabla halafu ndiyo mkaanza kubinafsisha ili uweze kupata mshindani wa kweli. Siyo leo *TANESCO* iko hoi bin taabani halafu unasema unabinafsisha.

Lengo lake ni kuwapa nafasi wajanja amba wanakaa, wanaviziavizia ili waingie wafanye vitu vyao. Kwa hiyo, nina wasiwasi kwamba pamoja na nia nzuri ya ubinafsishaji katika sekta mbalimbali lakini hili linaweza kuwa ni moja kati ya hila ambazo mafisadi wa nchi hii wanazitumia ili kupata matakwa yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pendekezo langu ni kwamba kwanza tuihuise hii *TANESCO*, tuipe kila aina ya msaada wa kifedha na kiutalaamu. Itakapokuwa tayari sasa basi tukaribishe na wageni waanze kushindana vinginevyo tukisema ziende sambamba huku tunakaribisha wawekezaji binafsi na huku *TANESCO* tunaisaidia kifedha kama ilivyo ile *Financial Recovery plan* ya Wizara basi nina wasiwasi kwamba tutafikia pahala *TANESCO* itashindwa.

Mheshimiwa Spika, kero kubwa ambazo hapa Waheshimiwa Wabunge wanavyozungumza ni juu ya bei na umeme wa uhakika. Bei ya umeme sasa hivi ni kubwa sana. Kwa mwananchi wa kawaida imekuwa kama ni bidhaa ya anasa, si ya lazima na wengi wanaishia kwenye vibatari na kandili. Lakini bayu zaidi katika hili ni kwamba kwa wale wapangaji wanapofikia wakati umeme unakatwa, kwa mfano, ana bili ya deni la 100,000/= linamshinda kulipa basi baada ya mwaka mmoja inakuwa 300,000/= badala ya 100,000/=.

Utashangaa ni kwa vipi umeme ambao hautumiki baada ya mwaka mmoja malipo yake yanakuwa mara tatu. Wananchi hawaelewi formula zinazotumiwa na *TANESCO* katika kutoza malipo, wao wanadhani kwamba wanalipa zaidi kuliko wanavyotumia kwa hiyo hizi ni katika dosari na kero kubwa. Sasa matarajio ni kwamba baada ya Muswada huu kupita hayo yatakuwa hayapo vinginevyo tutakuwa hatujawasaidia wananchi wetu itakuwa tunawasaidia wengine ambao hatuna haja nao. Mimi ningeshauri *TANESCO* katika hili na wamesema Waheshimiwa Wabunge hapa kwamba gharama za uungaji

umeme ni kubwa sana lakini juu ya gharama kuna urasimu wa hali ya juu. Unaweza kwenda *TANESCO* kuwaomba kuungwa umeme ukaambiwa kuna wenzako wengi sana hapa wa mwaka mzima wamefika kwa hiyo, wewe itabidi usubiri kwanza. Lakini ukifanya kuzunguka zunguka kidogo ukatoa chochote basi kesho utaungwa umeme.

Kwa hiyo, kero hizi nafikiri hazitusaidii katika kuendeleza sekta hii ya umeme ili wananchi wetu wapate umeme wa kutosha. Mimi nashauri kwamba wakati wa kuungwa umeme kwa sababu bili ni kubwa (Waheshimiwa Wabunge wanasesma karibu 400,000/= na zaidi) kwa nini *TANESCO* isibebi gharama hizi halafu mteja akawa analipa kidogokidogo katika bili yake ya kila mwezi au anapokwenda kununua umeme. Lakini tukimwachia mteja kwa kweli Watanzania wengi watakuwa hawana fursa ya kuwa na umeme majumbani mwao.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu *EWURA* ndiye mdhibiti mkuu wa sekta ya umeme. Mimi nasema *EWURA* haina uwezo, *EWURA* kama refa hana uwezo kwa sababu tumwangalie *EWURA* katika kipindi hiki cha hivi karibuni ambaye alikuwa anafanya kazi hizi hizi. Je, *EWURA* amefanya lipi zuri kwa sababu kwa mfano bei za mafuta zimekuwa zikipanda kiholela tu lakini vilevile watu wameweka vituo vya petroli katika maeneo ambayo hayahusiki. Sasa nadhani hili tunesema kwamba tunamkabidhi madaraka zaidi, hii ni kuiangamiza sekta ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, mimi nilifurahi kwamba *TANESCO* haikubinafsishwa lakini imefisadiwa maana kwa muda wa kutoka 2002 – 2007 ina hasara ya takriban bilioni 520.7 na bado wanaendelea kulipa hizo *capacity charges* za makampuni mbalimbali ambayo tumeelezwa. Kwa hiyo, *TANESCO* nasema kama kampuni yetu ipewe nafasi ijiendeleze ili iwe ndiyo msambazaji au mzalishaji wa umeme nchini kabla ya kuleta makampuni binafsi.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nijikite kidogo kwenye Muswada wenyewe ingawa muda umekwisha lakini sehemu ya 2 ya Muswada kifungu 4(1)(a) ambacho kinazungumzia uwezo wa Waziri (*Power of the Minister*) na hapa inazungumzia kuhusu sera ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, najua kwamba Wizara ya Nishati siyo ya Muungano lakini inatumia gesi ambayo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Na katika hili kuna mteja muhimu wa Zanzibar, Shirika la Umeme la Zanzibar *ZECO*, wao wameanza kununua umeme kutoka *TANESCO* toka mwaka 1980 kwa kutumia *submarine cable*. Lakini katika sera hizi *ZECO* haikutajwa.

Siku za karibuni tunesikia kuna matatizo mbalimbali katika vyombo vya habari kuwa *EWURA* imeitaka *ZECO* iongeze bei ya umeme lakini *ZECO* imekataa kwa sababu inasema haiitambui *EWURA* lakini inatambua *TANESCO* kwa sababu wao ndiyo wamewekeana saini.

Mheshimiwa Spika, nafikiri hapa kuna upungufu katika sera hii kwa sababu *ZECO* ni mdau muhimu katika mambo ya Nishati kwa hiyo hawezি kufananishwa na

kampuni nyingine yoyote ya nje lazima awekewe nafasi yake katika hili ili tuweze kwenda vizuri bila ya mgongano wowote.

Mheshimiwa Spika, katika hiyo sehemu ya tatu, Kifungu cha 8(2)(a), kuna suala la kusamehe yaani unasamehe wale ambao wanasamehewa leseni. Misamaha ya kodi kama tunavyojuu ilitupeleka mahali pabaya. Sasa sijui *exemption* hii itakuwa kuwaje kwa sababu inaweza kuwa ni *loophole* hapa itatumiwa ili waendelee kujinufaisha wale ambao wanapenda hivyo. Katika sehemu ya nne ya Muswada wetu kifungu cha 21 kinazungumzia juu ya *Tariff*, wanasema kwamba *EWURA* ndiyo *regulator* wa *Tariff*. Mimi nasema *EWURA* hawezি ku-regulate kama nilivyosema mwanzo. Mtu ambaye au chombo kinachowezza ku-regulate ni *TANESCO*. *TANESCO* ikiwa katika hali nzuri wao wakawa ni mfano wa bei basi na wengine watafuata.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 8 sehemu ya 1 kuna suala la *cross border trade* yaani biashara ya mipakani, wasiwasi wetu hapa ni kwamba wawekezaji binafsi wakiruhusiwa kufanya kazi kama vifungu hivi vilivyosema, *cross border trade* hawatakwenda katika maeneo ambayo hayavutii. Lazima watasafirisha uchumi katika nchi nyingine ili wapate faida kwa sababu malengo makubwa ya mfanyabiashara yejote ni *to maximize profit*. Kwa hiyo, hapa tunasema kwamba lazima kwanza awekewe masharti ya asilimia fulani apeleke umeme vijijini ambako ndiyo kwenye matatizo makubwa na asilimia kidogo aweze kusafirisha nchi nyingine akipenda.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya Muswada huu kifungu 14 (5)(c) kuna suala la *employment of personnel*.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Pole sana Mheshimiwa Salim Hemed Khamis. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri, nadhani kutakuwa na muda wa kumwezesha mmoja tu mwingine ambaye ni Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge sidhani kama tutamfikia, kwa hiyo, ni hao wawili kwa sasa.Naam! Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri!

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika Muswada huu ambao umeletwa hapa na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Mimi nimeshiriki katika semina mbalimbali ambazo ziliendeshwa kuhusu Muswada huu na sasa nafika kwenye Muswada wenye kwa maana ya kusaidia, kushauri ni nini tunafikiri kifanyike.

Mheshimiwa Spika, ukitaka kulielewa jambo hili ni lazima uelewe mahusiano ya uzalishaji mali ya kibepari na mahusiano ya uzalishaji mali ya kijamaa. Lazima uelewe *the political economy of capitalism* na uelewe *the political economy of socialism*. *Political economy* siyo *economics* na *politics go together*, unazungumzia mahusiano ya uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, binti yako akiajiriwa kwenye baa ziko *risks* zake, mahusiano yatakayojengeka pale ndani ya baa toka asubuhi mpaka jioni huna hakika nayo. Unaweza kuamua, ile ni kazi ambayo tunaiheshimu vizuri sana, unaweza kusema mama

saa nne usiku ikifika twende tukamchukue binti tumrudishe nyumbani, lakini mle ndani kwenye baa watu wanakunywa pombe, kwa hiyo, wanaweza kuzaliwa wajukuu kule hujui kwanza ni wa nani au amemzaa nani. Hii ndiyo *risk* tunayoipata katika mfumo huu wa ubepari ambao nauzungumzia hapa, zamani tulikuwa tunasema ubepari ni unyama. Si vibaya kutahadharisha, najua kwamba ubepari na soko huria na soko huru ni sera ambazo zimepitishwa na Chama changu cha Mapinduzi na Serikali imekubali. Lakini hii haitufanyi sisi tusifike mahali tukajua nini maana yake. Unapozungumza habari ya ubepari lazima uainishe hapa na Mheshimiwa Ngeleja mimi wasiwasi wangu nilikwishakuonyesha wala usiwe na wasiwasi kwa sababu nitaingia spidi lakini Muswada huu nauunga mkono. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, nitaeleza kwa nini nauunga mkono Muswada huu, wenzetu mabepari wanapofanya kazi wanatafuta kitu kinachoitwa faida kubwa (*super profit*) wala siyo *profit*, wao wanaendeshwa na kitu kinachoitwa sheria ya utashi na urari, sheria ya mashindano na sheria ya thamani, ndiyo inayofanya kazi. Unapokwenda kwenye nchi za kijamaa njia kuu za uchumi zote zinawekwa mikononi mwa umma, kwa hiyo, mnapokwenda kupima kule hamwangalii *balance sheet*, umeme ukienda kwako Urambo unasema ndiyo faida yenyewe, hukai tena ukasema, unajua kupeleka umeme pale tulipata hasara, shirika la umma linachoangalia ni huduma kwa jamii inayohusika. Kwa hiyo, ukichukua Shirika la kibepari litaangalia kama hii biashara wanayokwenda kufanya izidi (*economically viable*), Mheshimiwa Ngeleja ndiyo wasiwasi walio nao Wabunge wengi humu ndani.

Mheshimiwa Spika, wanachoogopa hapa ni hiyo tabia ya shirika la kibepari ya kutaka kutengeneza faida kibao, matatizo tuliyoyapata katika mashirika haya ndiyo hii hali tulioipata baada ya kuingiza mashirika haya ya kibepari, ndiyo tukafika hapa tulipofika. Leo tunasema kwamba tunataka kuitisha sheria ambayo itaruhusu watu kutoka nje wawekeze kwa maana ya sekta binafsi. Mimi sina ugomvi na hilo, lakini haininyimi kujua tabia ya haya mashirika binafsi yanakwendaje. Anza kwanza na *TANESCO* yenyewe, kwa nini *TANESCO* ilifika hapo ilipofika kwa sababu ya utaratibu wa umilikaji wa shirika lenyewe. Ukisema hili ni shirika la umma maana yake ni shirika ambalo linamiliiki na Watanzania milioni 35.

Mheshimiwa Spika, umilikaji wa jumla kiasi hicho *a such broad declaration of ownership, in fact unachosema ni kwamba hili shirika halina mwenyewe, litakuwaje gari limekaa pale nje useme ni shirika la umma, yaani gari moja hili linakaa pale tunamiliki sisi wote watu milioni 35*. Lazima ufile mahali useme hivi *TANESCO* pamoja na Bodi ya *TANESCO* tunakukabidhi shirika hili kwa nia ya Watanzania, kwa hiyo, mtu mwingine yejote iwe Wizara asiingie mle tena na yeye akataka kufanya yake, haiwezekani watu milioni 35 wanamiliiki shirika la umma, itakuwa ni vurugu. Wakabidhi *TANESCO*, Wizara ikianza kuingia kule ndiyo sasa unasema hili ni shirika halina mwenyewe, wape shirika la umma *TANESCO* walismamie kwa niaba ya Watanzania. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, wape *TANESCO* watu ambao ndani yao wana moyo wa kizalendo. Ukikutana na Mhindi pale Canada ndani ya moyo wake mapigo ya moyo

wake yanakumbuka India. Ukienda ukamkuta Mchina yuko Marekani, ndani ya mapigo ya moyo wake kuna kitu kinaitwa China. Ukienda Israel moyo wake na akili yake yote iko Israel. Weka ndani ya *TANESCO* mtu ambaye mapigo ya moyo ndani yake yana Tanzania.

Shirika la umma hapa, unamkabidhi mtu ye yote hana moyo wa uzalendo, hana *ideological clarity*, unamwambia chukua tu shirika hili unamkabidhi, *what are you doing?* Akina *Lenin*, *Mao Tse Tung* hawakuwahi kukabidhi mashirika ya umma kwa mtu mradi mtu. Unakwenda pale unatiki, unasema Dk. Idris tiki, huyu anaonekana ana moyo wa kizalendo, huyu mwingine anafaa tiki, tiki, tiki! Weka watu ndani ya *TANESCO* ambao ndani yao wana moyo wa kizalendo, wana uchungu na Watanzania!

Mheshimiwa Spika, watu wanapiga kelele, *connection fee*, sh. 500,000/=, Mtanzania gani anaweza hiyo? Mbunge mwenyewe unajipapasa papasa! Nimetumwa hapa na watu wa Siha kumwambia Mheshimiwa Waziri, umeme Siha upo lakini tatizo letu ni usambazaji wa umeme. Ukitsema Sh. 500,000/=, mtu gani wa Siha ataweka umeme, wanasema *EWURA* watasimamia hili jambo. *EWURA* wanakaa wiki ya kwanza wanasema tumeweka ngumu, wiki mbili zikipita wanasema wameruhusu, ndiyo kitu kinachozungumzwa hapa, ndiyo *control* inayozungumzwa hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, ipe *TANESCO* majukumu mapya, weka pumzi mpya mle ndani. Muswada huu kama tumeupitisha leo, nilipokuja hapa nilifikiri wanatwambia labda tunabinafsisha mpaka *TANESCO* yenyewe, nenda kamulize Lord Kenzie, kamulize David Likado, Adam Smith, Biyong Touniers, mahali popote ambapo unahitaji mtaji mkubwa utapeleka mkono wa Serikali. Mahali popote ambapo ni nyeti kwa uchumi wa nchi Serikali itaingilia kati. Hawa ninaokutajia hapa akina Adam Smith wala sio wajamaa, acha mambo ya ujamaa, mimi sizungumzi habari ya ujamaa, maana yake utaonekana kama mwendawazimu, zilipendwa sijui nini. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tuzungumze tu uzalendo wa kawaida, wale wajamaa wa *Railways*, *Telecommunications* na simu na umeme hawatoi kwa mtu binafsi, Serikali ndiyo inasimamia. Sisi hapa tunataka kuwapa watu binafsi, leo hatuwezi kukubali kubinafsisha Shirika hili.

Wenzako wana kitu kinaitwa *synchronization and sequencing* maana yake peleka kama unavyompeleka ngamia, anaingia kwenye *tent*, sukuma kichwa mle ndani halafu baadaye peleka mwili mzima. Ndiyo mashirika mengi yatakwambia unajua *TANESCO* sasa *hai-function* bwana, imefika mahali inaonekana inaendeshwa kwa hasara, sasa tukabidhi shirika binafsi liendeshe kazi hii, ndiyo mmekwenda.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mheshimiwa William Ngeleja aiambie *TANESCO* kwamba kazi ya kupeleka umeme kijijini ni kazi yao. Msitwambie kwamba tunakwenda kuwaauliza, watu wa Mtwara sina tatizo na hilo, Mtwara *ARTUMAS* tunaikubali, mimi nitaeleza kwamba ni kwa nini tunaikubali *private sector* iende pale. Ni kweli kwamba shirika hili limeelemewa, imefika mahali ambapo haliwezi kupeleka umeme nchi nzima. Unaruhusu shirika la watu binafsi liingie pale kwa sababu kuu nne, kwanza, litaleta mtaji. Pili, litaleta teknolojia na sayansi ya kisasa. Tatu, litasababisha ajira na nne utapata kitu

kinachoitwa *Government Revenue*. Sihitaji kwenda Chuo Kikuu kuelewa umuhimu wa hicho kitu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, huduma ile Mtwara kama haipatikani, kama *TANESCO* haiwezi kupeleka umeme Mtwara, tuwaambie *private wapeleke pale* lakini kumwambia *private apeleke umeme Mtwara, must carry with itself a substantial amount of responsibility* ndani yake. Lazima umwambie popote utakapopitisha umeme ule kama kuna wananchi wako hapa chini hakikisha umeme unakwenda pale, muswada huu unatamka hivi na ndivyo unavyosema hapa na mimi kwa msingi huo nasema kwamba naruhusu sheria hii ipite kwa sababu lazima uwalazimishe. Sheria ilivyokuwa kule nyuma, Baba Askofu Martin Shayo kwetu Siha au Dayosisi ya Kaskazini akiwa na umeme pale anauleta hapa. Sheria ilikuwa inamruhusu anaweza kuutumia yeye mwenyewe pale, lakini leo anaruhusiwa kwa muswada wa sheria hii sasa kuusambaza umeme katika vijiji vilivyo karibu karibu. Mimi sioni ugomvi kwenye kuitisha jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nne, nataka nimalizie kwamba sisi tunakwenda kupeleka umeme kule, hatutaki Mheshimiwa Ngeleja arudi atueleze hadithi kama ile ya kule nyuma. Kuna mdudu anaitwa *capacity charge*, wewe hapa unasema kuna umeme wa dharura, wakati huu tunapojuwa kwamba Mtera imejaa, wakati huu tunapojuwa kwamba sasa maji yanapatikana, ndiyo wakati wa kuanza kuweka tena majenereta mapya ambayo kama Mtera itakuwa haina maji, ndiyo unakwenda kuyatumia.

Ngoja nieleze tatizo linalotokea Serikalini, tunasubiri mpaka Mtera ikauke, unaanzisha *frantic move*, unaanza kukimbia kushoto, kulia na katikati, watakupeleka kushoto kwa sababu tutaingia kwenye *black-out* kule mbele, *uta-panick*, itafika mahali utafanya maamuzi. Wewe ni mtoto wa Mungu tunajua, ile *emergency* itakuletea matatizo makubwa, utakuta umefanya maamuzi ya ajabu.

Mheshimiwa Spika, mimi nimetumwa na wananchi wa Wilaya yangu ya Siha kusema maneno yafuatayo:-

Maandalizi ya umeme wa dharura huu wa haraka haraka yaanze wakati tuna neema katika nchi. Kama hivi tunavyozungumza ndiyo wakati mzuri, *capacity yetu tunayozungumzia* hapa ni megawati 105, zile zilizoko Tegeta na ile nyingine 105 haitoshi. Kama umeme utakuwa umekwisha usipopata umeme wakati huu ambapo tumetulia, ukangoja mpaka wakati wa *panic*, ukaanza kukimbia, *capacity charge* hutaikwepa mzee wangu, utachukuliwa mabango hapa, itakuwa tabu, hakuna *investment* itakayofanyika, utasikia, tunataka umeme, utafanya nini, kichwa kinaanza kuzunguka, hivyo unaanza kufanya maamuzi ya ajabu ajabu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu sasa tunapozungumza kwamba Mtera imejaa ndiyo wakati wa kuweka umeme wa dharura. Mashine zikae pale, mtu ye yote mwenye akili akijua umeme huo unazimika hapa ataweka pasi ya mkaa. Akijua kwamba hapa hakuna umeme ataweka misitu, atapanda miti, *this is simple common sense*. Mwanafunzi wa sheria aliwahi kuulizwa *what is law* na *Attorney General* naona unaniangalia,

akasema *law is a simple common sense*. *Simple common sense* inanifanya niamini kwamba umeme katika nchi hii hauwezi kupelekwa na *private sector*, *private sector* itasaidia tu. Lakini jukumu la msingi la kupeleka umeme vijijini liko ndani ya *TANESCO*. (*Makofi*)

Katika Jimbo langu la Siha, vijiji vyangu ambavyo havina umeme ni Kishisha, Mayu, Polikolili, Ngandashi, Lekrimuni, Penemoro, Wandrimae, Msherehe, Mohonjamu, Kartati, Naibilia, Kandashi na Karansi. Hii miradi imekwishaanzishwa na mpaka hivi tunavyozungumza hawana umeme, Mese, Ngaroi, Samaki-Maini na Kata nzima ya *West Kilimanjaro* haina umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, napitisha Muswada huu hapa *with conditions* kwamba Mheshimiwa Waziri tutakwenda kusambaza umeme katika vijiji tulivyovizungumza hapa, wananchi hawa ndiyo wanazalisha viazi, kahawa, nao wanataka wapate umeme kama wananchi wengine wote duniani, *getting electricity is a modern way of living*.

**MBUNGE FULANI:** Sawasawa.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Ndiyo namna ya kisasa ya kuishi, lakini *politics* zake ni ngumu katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nasema kwa uchungu mkubwa hapa, wanalamika pia kuhusu *charges* zinazotolewa. Bili ya mwananchi wa kawaida sasa hivi imefika Sh. 18,000/= mpaka Sh. 20,000/=, hawawezi wale watu, tusaidieni na sisi tunufaiki, tupate maisha mazuri kama Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutamka tena, najua kwamba kengele italia sasa hivi, narudia kusema kwamba huo ndiyo mchango wangu. Mheshimiwa Waziri asiachie *private sector* hapa, itamyumbisha, itafika mahali watamwambia na ye ye acae pembeni, itakuwa matatizo makubwa. Wewe ng'ang'ana na *TANESCO*, sema hii ndiyo *flow back* yangu, hapo utapona.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, napenda kusema kwamba naunga mkono Muswada huu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia maoni yangu kuhusu Muswada huu. Lakini kwanza kabisa nachukua nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Nishati na Madini ndugu yangu Ngeleja, Naibu Waziri na watendaji wote wa *TANESCO* na Wizara kwa ujumla kwa kuleta Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu naanza na kuchangia kuhusu umuhimu wa *Power System Master Plan*. Tumesikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri alipotoa wakatuahidi kwamba *Power System Master Plan (PSMP)* itakuwa tayari mwezi wa Nne. Lakini nataka kusema kwamba hiyo ni hatua nzuri na nampongeza kwa juhudhi yake hiyo

na nataka wengi tulione hili kwamba lina umuhimu kwamba katika kujenga uchumi bila *Power System Master Plan* katika shughuli ya usambazaji wa umeme basi tutakuwa tunaota ndoto tu.

Katika taarifa za hivi karibuni za Benki yetu ya Tanzania tumeelezwa kwamba pato kuanzia 2001 mpaka 2006 lilikua kwa asilimia 7 na sekta ambazo zimechangia sana ilionyesha kwamba ni ujenzi ambayo ilichangia asilimia kumi na moja. Huduma za fedha asilimia 9.7, madini 5.6, viwanda asilimia 8.7, mawasiliano 8 ikionyesha kwamba kilimo mchango wake umekuwa mdogo.

Mimi naamini kwamba kama kwenye *Power System Master Plan* tungkuwa tumeweka mkakati wa kusambaza umeme nchi nzima kwa hakika mtazamo huu wa uchumi usingekuwa kama ulivyo hapa hasa ukizingatia kwamba asilimia 80 ya wananchi wanategemea kilimo. Na hii ingeletekeza kabisa kwamba huenda tusingekuwa kwenye asilimia 7 kama kukua kwa uchumi, ingekuwa imeongezeka zaidi kwani ukiwezesha miundombinu ya barabara na umeme katika nchi nzima utakuwa una maana kwamba kilimo kinapata mafanikio makubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano tu kwamba wenzetu wa Urusi baada ya mapinduzi yale ya mwaka 1917 wakajikuta uchumi wao unayumba sana mwaka 1920. Kwa hiyo, aliyekuwa kiongozi wakati ule Ndugu Lenin akaja na wazo la kuwa na *Master Plan* ya umeme kwa nchi nzima. Kwa hiyo, mwaka 1920 waliunda *Commission* ya watalamu ambao walikaa na kutengeneza *Master Plan* ya kusambaza umeme nchi nzima. Na hii *Master Plan* ilifanyiwa kazi na wanasayansi na wahandisi mia mbili kutoka nchi nzima na wakai-*adapt* na ikapitishwa kwenye *Congress* ya Urusi ya nane na ikawa ya miaka kumi. Kufikia 1931 wakawa tayari wana vinu zaidi ya thelathini na vikiwemo vya kuzalisha umeme katika nchi ile na wakawa tayari wameweza kusambaza umeme katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, wao walikuwa na kaulimbiu moja ambayo nadhani inaungana sana na ndugu yangu Mwanri kwamba walikuwa wanaamini kwamba kujenga ujamaa bila kuwa na umeme katika vijiji itakuwa haiwezekani. Kwa hiyo, wakasema *socialism plus electrification of the whole country* na ndiyo maana wakafanikiwa. Hivyo, mimi naamini kwamba kama tukisambaza umeme tukawa na hii *Power System Master Plan* tukajua kwamba umeme ukishafika kila sehemu nadhani haya yatakuwa mafanikio na nimwombe basi Mheshimiwa Waziri kwamba hiyo *Power System Master Plan* ishirikishe wadau wengi.

Tunao wasomi kwenye Vyuo Vikuu, tunazo Taasisi za Sayansi na Teknolojia, tunao watu viwandani, basi hao washiriki katika kuijadili isiwe tu *TANESCO* wamejifungia ndani peke yao wakaja na hiyo *Power System Master Plan*. Kwa sababu hii inagusa karibu vijiji vyote, kata na wilaya zote, nadhani ni vizuri kabisa hata baada ya wao kuitengeneza ije hapa katika Bunge lako Tukufu ili tuweze kuijadili na kuona ni namna gani inaweza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia maendeleo ya suala la umeme katika Afrika Mashariki. Sisi Tanzania tunasema kwamba tumesambaza asilimia 10, lakini ukienda Kenya nao wamesambaza asilimia 10 na Uganda wamesambaza asilimia 5. Lakini ukiangalia katika uzalishaji Tanzania tuna uwezo wa kuzalisha sasa hivi megawati 800, wa Kenya megawati 1,447, wakati Uganda ni megawati 300. Lakini Tanzania tuna *potential* imeongeleta asubuhi kwa kutumia umeme wa maji tu. Tuna *potential* ya 4.7 megawati na mpaka sasa hivi tumeweza kutumia asilimia kumi tu. Sasa nini maana yake katika hili?

Mheshimiwa Spika, mtazamo wangu ni kwamba kwa kutumia *Power System Master Plan* na sheria hii ambayo tunategemea kuipitisha basi *TANESCO* wawe ndiyo wamiliki wakuu wa kuona kwamba umeme unasambazwa kwa nchi nzima mpaka vijiji na siyo vinginevyo. Lakini vilevile *TANESCO* kwa sheria hii wanawezeshwa basi watumie vyanzo vingine ambavyo vipo vilivyoainishwa katika maeneo mbalimbali kama vile hii mito ya Ruhuji ambayo inatoa megawati 350. Mto Rumakalya huu upo Makete unatoa megawati 220, kuna *Stigler's Gorge* ambayo inakadiriwa kutoa zaidi ya megawati 1,200 na mingine mingi. Kwa hiyo, naamini kwamba sheria hii itawawezesha *TANESCO* kufanya kazi hii kikamilifu. Nami naungana na wenzangu kwamba mtu pekee wa kutusaidia kusambaza umeme ni *TANESCO* yenyewe.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia vilevile suala la ubinafsishaji katika sekta hii ya umeme. Nikajaribu kuangalia wenzetu wa Kenya, Uganda na baadaye Tanzania. Kutowana na *pressure* za *donors* wenzetu wa Uganda waliigawa kampuni yao ya kuzalisha umeme katika makundi matatu, wakawa na Uganda *Electricity Generating Company*, *Transmission Company* na *Distribution Company* na wao kama Serikali wakabaki na *transmission company* wakaacha *distribution* kwa watu binafsi na matokeo yake ikaonekana kwamba kwenye *distribution*, *Electrical Regulatory Authority* ikawa *corrupt* kama vile tunavyosema sisi *EWURA* wanatakiwa wawe waaminifu. Na kwa zile *corruption* ikatokea kwamba bei za umeme kwenye ile kampuni iliyokuwa inasambaza zikaongezeka. Mwaka 2005 waliongeza kwa asilimia 34 na mwaka 2006 waliongeza kwa asilimia 37. Kwa hiyo, mzigo huu ukawa unakwenda kwa wananchi ambaa ndiyo walipa kodi na inaonekana halikuwa na mafanikio.

Mheshimiwa Spika, ukienda upande wa Kenya vilevile wao waliigawa kampuni yao katika sehemu mbili. Kukawa na Kenya *Power and Light Company* ambayo ilijigawa katika makundi mawili, ile ya uzalishaji pamoja na usambazaji, lakini wakaiachia Serikali usafirishaji na usambazaji ambayo pia kwa sababu ya *corruption* ya maeneo mbalimbali haikuweza kufanikiwa. Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali yangu kwamba wazo hili lilipokuja Tanzania mwaka 2006, Serikali yetu ilikataa kubinafsishwa kwa *TANESCO*. Hiki ni kitu kimoja kizuri sana lakini badala yake tukawa na makampuni ya *Songas* na *IPTL* ambayo tumeendelea kuyalipa fedha nyingi. Kwa mfano, *IPTL* wamekuwa wakilipwa dola milioni 3 kwa mwezi. Sasa uzoefu unaonyesha kwamba makampuni ya watu binafsi katika kuzalisha umeme wao wanajali zaidi faida na hawana namna nyingine ya kupata umeme zaidi ya kuongeza bei. Kwa hiyo, gharama hizi anabebeshwa mwananchi na mwananchi anabebeshwa hizi gharama kuitia *TANESCO* yenyewe.

Mheshimiwa Spika, *another reason* ni hiyo tu kwamba *corruption* kati ya watendaji wa hizi *Regulatory Board* na yale makampuni kunakuwa na mazingira ya rushwa na hivyo kufanya hii sekta ya uwekezaji binafsi kutozaa matunda. Nini mapendekezo yangu hapa, ni kwamba, *EWURA* lazima wafanye kazi kwa kufuata maadili kwa kutumia sheria hii na wamepewa hiyo nafasi. *EWURA* vilevile lazima wa-*provide fair, open and competitive process* na sheria inawapatia huo uwezo.

Kwa hiyo, naamini haya yakifanyika tunaweza kufanikiwa. Lakini vilevile ubinafsishaji umejitokeza, tumeona matatizo wakati tunabinafsisha huduma ya maji, *Bi Water Company* ya Uingereza baadaye Serikali ikachukua baada ya ile kampuni kushindwa. Lakini tumeona vilevile *Air Tanzania*, baada ya *poor performance* na wale kuvunja taratibu zetu Serikali imeingilia kati na kuchukua asilimia 49. Vilevile tunaona *TTCL*, baadaye Serikali ikachukua nadhani asilimia 36. Hii inadhihirisha kwamba sekta ya binafsi katika umeme siyo kitu rahisi, watabaki kuiongezea mzigo *TANESCO* na kwa hiyo, tuichukue hii sheria kama ni changamoto kwa *TANESCO* ili wao wenyewe waweze kuchukua hii kazi ya kusambaza umeme.

Mheshimiwa Spika, niseme tena kwamba sisi kama Serikali tusitegemee sana sekta binafsi ya umeme kama ndiyo mkombozi kwa nchi yetu, nadhani tuione sekta binafsi kwenye sehemu ya umeme kama historia na naomba wenzangu watofautishe biashara ya umeme na mazao mengine. Umeme siyo sawa na mafuta ambayo unawenza kununua kwa wingi ukayaweka, halafu baadaye ukasubiri bei ipande ndiyo uyauze, umeme hauna njia ya namna hiyo, ndiyo maana wale wanapandisha bei mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kushukuru sana juhudi za Serikali katika mpango mzima wa *Millennium Challenge Corporation (MCC)*. Nina hakika kwa kupitisha Muswada huu kutasaidia kusambaza umeme katika sehemu ambazo zinategemewa ikiwa ni pamoja na Jimbo langu la Makete ambalo tulikuwa tunategemea umeme utatoka Makete Mjini kwenda Ndulamo, Kisinga, Lupalilo na Tandala kwa mpango huu wa *Millennium Challenge*. Lakini nadhani vilevile kwa kuwa huu umeme umetoka Mbeya, zipo sehemu ambazo zimepitwa na nguzo kama vile Ujuni, Ikenja, Isaplano, kwa hiyo, ni muafaka hawa wakasaidiwa kwa mpango huu wa *MCC* wakapata umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuiomba tena Serikali iweze kupitia miradi yake mikubwa hasa ya kujenga vinu vyta umeme ambavyo vitazalisha umeme wa bei nafuu kwa wananchi. Tunayo mito mikubwa sana ambayo inaweza kusaidia, na kwa hiyo, Serikali ijikite zaidi kutafuta wafadhili wao kama Serikali na sio kwamba tutapata mafanikio kwa kupitia sekta binafsi. Sipingani na ubinafsishaji katika sekta nyingine, zinawezekana lakini siyo sekta ya umeme.

Hata ripoti ya *World Bank* inathibitisha kwamba sekta ya umeme na maji ni sekta ngumu sana katika zoezi zima la kubinafsisha na ina-*recommend* kwamba zile nchi ambazo hazijaanza ubinafsishaji basi waiachie Serikali na zile ambazo zimekwishaanza au zimemaliza kama Uganda basi waendelee kama walivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya nataka kusema kwamba naunga hoja mkono na nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mahenge. Waheshimiwa Wabunge muda uliosalia ambaao ni kiasi kama cha dakika nne hauturuhusu kuendelea na mchangaji yeoyote mwininge ila kwa faida ya namna tutakavyoendelea saa kumi na moja naomba niwataje watano wa mwanzo kuanzia saa kumi na moja ili waweze kuijandaa na kuwepo ukumbini. Tutakaporejea saa kumi na moja tutaanza na Mheshimiwa Anna Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Tatu Ntimizi, halafu Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o na Mheshimiwa Siraju Kaboyonga. Orodha yangu bado, lakini hawa watano wajiandae kwa kuanzia saa kumi na moja. Basi kufikia hapo, sasa naomba nisitishe shughuli za Bunge kabla ya wakati mpaka hapo saa kumi na moja.

(*Saa 6.50 Mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano na kwa kadri ya orodha yangu hapa Mezani, msemajji wangu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Anna Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Tatu Ntimizi. Mheshimiwa Mama Anna Abdallah tafadhali.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaomba kutoa pongozi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mbunge wa Kiteto, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge. Nilishiriki katika mchakato wa uchaguzi wake, ninampa pongozi kubwa sana. Aidha, ninampongeza sana Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge wa Bunge hili. Vilevile, sikupata nafasi ya kumpongeza Mheshimiwa Mchungaji Dr. Gertrude Rwakatare, naye ninampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakupongeza wewe pia kwa kuchaguliwa kwa kauli moja na Bunge hili kuwa Mwenyekiti, kuendelea kwa kipindi kingine cha miaka miwili na nusu. Katika kipindi ulichokalia Kiti, ninasema hasa wewe kwa sababu ni Mwanachama wa Umoja wa Wanawake, umefanya kazi nzuri na unastahili kuendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwanza, niunge mkono hoja hii nisije nikasahau, jambo la lazima ambalo limenifanya kuchangia ni kuunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuipongeza sana Kamati ya Nishati na Madini, kwa kazi yao nzuri waliyoifanya katika kuuboresha Muswada huu uliopo mbele yetu. Aidha, ninampongeza sana Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Adam Kighoma Malima na wataalam wao wote, kwa kukubali mapendekezo yaliyotolewa na Kamati na kuuboresha Muswada huu. Muswada ambao hapo awali ulionyesha matatizo makubwa sana, lakini sasa kwa kweli unakubalika; umekuja katika sura ya kukubalika. Tunawapongeza kwa kazi hiyo nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninapenda kuwashawishi Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwamba, tuupitishe Muswada huu, unayo manufaa mengi na kwa mapendekezo ambayo yametolewa na mabadiliko yaliyotolewa, ninadhani utakuwa na manufaa katika nchi yetu. Kupitishwa kwa Muswada huu na baadaye kuwa Sheria, kunaashiria kuwa sisi wa Mikoa ya pembezoni; mwanga wa maendeleo katika Mikoa hiyo utaanza kuonekana. Hii ni kwa sababu kama tungeitegemea *TANESCO* peke yake, sisi wa Mikoa ya pembezoni, basi tungekuwa ni watu wa kusikia tu habari ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara, wanaweza kusema mbona *TANESCO* ipo kwa jina. Sisi kule umeme wetu ni wa mafuta; mafuta yanaletwa kwa meli wakati mwingine kwa magari. Wakati huu ambapo barabara haipitiki, mafuta hayo yasingeweza kufika Mtwara kwa ajili ya kuendesha mashine zile wala Lindi na wakati mwingine hata hizo meli hazipo. Mgogoro wa mara kwa mara wa kulipana kati ya *TANESCO* na wenye meli, hata kama zile mashine zingekuwa zinafanya kazi, tulikuwa tunakosa mafuta. Kwa hiyo, hospitali na vitu vingi tu vilikuwa haviendi kwa sababu ya kukosa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Mtwara, tuna Kampuni ambayo inachakata umeme kutoka gesi ya Mnazi-Bay. Kampuni hiyo inaitwa *ARTUMAS*, inatengeneza huo umeme na kuuingiza katika miundombinu ya *TANESCO* iliyopo pale Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba chanzo cha umeme pale Mtwara ni kizuri, bado Mtwara wana matatizo ya umeme, kwa sababu miundombinu iliyopo pale ya *TANESCO* haitoshelezi na ni chakavu. Ninadhani suala hili la *ARTUMAS* na sisi kule kupiga makelele kwamba waruhusuni hao wasambaze umeme, basi ile miundombinu imetelekezwa, kiasi kwamba, hata hiyo miundombinu iliyopo sasa hivi kila wakati inaleta matatizo. Kwa hiyo, kupitishwa kwa Muswada huu na hatimaye kuwa Sheria, wakiruhusiwa wao wenyewe wazalishe ule umeme kutoka gesi ya Mnazi-Bay halafu wausambaze, kutakuwa na maendeleo makubwa sana katika Mikoa ile ya Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tu kwamba, wakati huku tunalia juu ya *capacity charge*, waliopewa wote wametajwa, kule Mtwara hao *ARTUMAS* pamoja na kuzalisha umeme, hawakupewa *capacity charge*, haipo kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninahisi kwamba, matatizo mengi yalitokana na hiyo, kungekuwa na *capacity charge*, kuna wale ambao wangelizungumzia wakawa ndiyo *beneficiaries*, pengine wala tusingefika hapa. Kwa sababu kweli ni matatizo ya ajabu na wao wanasema hawataki *capacity charge* na walituambia sisi Wabunge siku nyingi; wanasema jamani hayo mnayotaka ya *capacity charge* yanayotokea huko ni matatizo na ni kweli kwamba, huo ni mradi tu wa ulaji. Kwa hiyo, wao hawana *capacity charge*. Wanachoomba ni kwamba, waruhusiwe wao wenyewe kusambaza ule umeme na kama mlivyomsikia Mheshimiwa Raynald Mrope asubuhi kwamba, bahati njema sisi wenyewe tumeshiriki. Mkoa wa Lindi yupo Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir na Mkoa wa Mtwara yupo Mheshimiwa Raynald Mrope, ndiyo wanaokwenda katika mchakato huo wa mazungumzo juu ya namna gani tufanye juu ya gesi ya Mnazi-Bay na ule umeme uwafikie wananchi kila mahali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Masasi kuna mashine kubwa tu ya umeme, ambayo ndiyo inayozalisha umeme karibu Mkoa mzima wa Mtwara na sehemu chache katika Mkoa wa Lindi na hao hawajaunganishwa. Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika Mikoa hiyo, kwa miaka mingi sana wamekuwa wakipiga kelele wanaomba waunganishiwe umeme, *TANESCO* ilikuwa haina uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati mwingine nilipokuwa ninasikia watu wanaisemea *TANESCO*, nikasema *toba lillahi*, kumbe hawatujui sisi wenzao tabu inayotupata; sisi hatuna mapenzi na *TANESCO* kule Kusini, kwa sababu mambo yaliyotupata ni makubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi na hao *ARTUMAS*, tuna mazungumzo kila wakati. Waheshimiwa Wabunge wote, wakati mwingine kwenye *RCC*, hao jamaa wana mpango wa kuhakikisha kwamba, hata zile nyumba za nyasi pindi watakapopewa kibali na Sheria hii kupita, nyumba za nyasi zinaweza zikapata umeme. Kuna utaalam unaitwa *Ready Boards*, ambapo wenzetu wa Msumbiji wanautumia na Nigeria wanautumia huko walikobeba kwa *capacity charge*, lakini wanapeleka umeme kwenye nyumba za nyasi. Sisi kule Kusini nyaya zote za umeme zinapita juu ya nyumba za nyasi. Hao jamaa wamekwishafanya utafiti na kujua ni vijiji vingapi katika miaka hii ya mwanzo watapeleka umeme. Wao wenyewe hata kabla ya Sheria hii kuwalazimisha kwamba lazima wapeleke umeme, walituhakikishia kwamba, vijiji vinavyovipitiwa na nyaya za umeme, wanavijiji watapata umeme. Kwa hiyo, la kwanza ni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati *TANESCO* wana masharti magumu sana ya nyumba gani ipate umeme, hawa jamaa wanasema jamani sisi tuna huo utaalam wa kupeleka umeme katika nyumba za nyasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, manufaa tutakayoyapata kule ni kwamba, wataunganisha umeme Mkoa wote wa Mtwara pale ambapo *TANESCO* ilikuwa imepeleka nyaya, lakini wao wataziweka vizuri zaidi, kwa sababu hazitoshelezi kabisa kwa umeme wa gesi unaozalishwa kule; wataunganisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulipozungumza nao tumewaambia umeme huo pindi watakapopata ruksa waufikishe mpaka Tunduru. Tunduru sasa hivi ilivyo katikati ya nchi, bila hawa hawatapata umeme wale, hata kama majogoo yangewika namna gani! Tunduru pamoja na kule kwa Mheshimiwa Vita Kawawa, upite huko umeme uende mpaka Songea na ukifika Songea utafika mpaka Peramiko, halafu wauingize katika Gridi ya Taifa. Umeme ukiingizwa katika Gridi ya Taifa, utasambaa katika sehemu nyingi. Umeme wa maji una matatizo. Tumepata mifano mingi sana katika miaka iliyopita ya ukame mpaka tukataka kutengeneza mvua za *artificial* ili mabwawa yajae maji lakini ikashindikana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa gesi ipo, hakuna kitu cha *artificial* cha kuongeza huko; ni kiasi cha kuweka mitambo na hao wawekezaji watengeneze umeme. Haya mabwawa ya maji, tunakokwenda siyo kuzuri, mvua zinakuwa chache, lakini vilevile kwa ajili ya matumizi yanayotokana na vyanzo vya maji tutapata shida ingawa wanasema eti hicho chanzo ni rahisi, sina uhakika kama huko tunakokwenda kitakuwa rahisi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuzungumzia suala la gharama za kuunganisha umeme; sasa hivi gharama za *TANESCO* ni za juu sana. Ninaomba huyo mdhibiti ambaye anaitwa *EWURA*, asije akawashinikiza hao wawekezaji binafsi na hasa ninamsemea *ARTUMAS* kwa kuwa tunamuelewa. Wasije wakamshinikiza akapandisha gharama za umeme ili walingane na *TANESCO* ili waje watuambie kwamba kiko wapi? Wasifanye hivyo, kama hao wapo tayari kutoza gharama za chini, wawakubalie ili watu waweze kuunganisha umeme katika nyumba zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kuna suala malipo ya matumizi ya umeme ya kila mwezi, ambalo tungependa nalo liangaliwe. Hivi hata *TANESCO* tukiwaliza, tunajua walikuwa wanafanya vile kwa kuwa kulikuwa hakuna mpinzani; hivi hayo malipo ya umeme ya kila mwezi ni kwa ajili ya nani kama siyo wafanyakazi na wafanyakabiashara; ni mkulima gani kijijini; wa pamba, korosho, tumbaku, kahawa au mkulima wa karafuu, anayeweza kulipa ankara ya umeme ya kila mwezi; kwa sababu hao wanapata malipo mara moja kwa mwaka wakati wa msimu wa mavuno?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni sisi kule Mtwara katika utaratibu wetu wa uuzaaji wa korosho, basi mtu anapata malipo ya kwanza, atapata malipo ya pili na akijaliwa atapata malipo ya tatu. Kwa kawaida akishapata hayo malipo mara moja, tena kwa kunyonywa, mkulima hana mapato tena, ingawa wakati ule wa kuuza anakuwa na mapato mengi. Kwa hiyo, mkulima atakapopata fedha, lazima kuwepo na utaratibu wa kumfanya ama alipie umeme wamkadirie hasa ule anaotumia kwa taa, kujua anatumia kiasi gani wakati atakapopata fedha wamwambie alipe mpaka hapo watakapoona kwamba anatumia umeme zaidi ili aongezee fedha. Vinginevyo, huo umeme utakuwa ni wa wafanyakazi wanaopata mshahara kila mwezi, wafanyakabiashara wanaopata visenti sijui; maana wao wanapata kila siku, ndiyo watakaoweza kulipia umeme wa kila mwezi. Mkulima ambaye tunasema lazima apelekewe umeme huko kijijini, tufikirie utaratibu mzuri wa kumfanya alipie wakati anapopata mapato kutoka kwenye mazao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, wale ambaeo wanapata umeme wa *TANESCO*, hata mimi kule Dar es Salaam kwenye kibanda

changu ninapata umeme wa *TANESCO*, lakini hata hivi tunavyosema, pamoja na mvua hizi, sijui wengine; tena ni Oysterbay, kila siku umeme unakatika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine ukipenda sana mtoto atafanya mambo tu, atavunja vioo, atavunja glasi, unamtazama kwa kuwa unampenda. *TANESCO* tumeipenda mno; inapandisha ghamama za umeme inavyotaka na inakukatia umeme inavyotaka. Halafu angalia wanapunguza watumishi lakini wapi, nendeni mkaone kule wanakozalisha umeme Mtwara, mkaangalie kuna watu wangapi? *TANESCO* wanaajiri watu wengi kupita kiasi, halafu wanasema wana matumizi makubwa; matumizi makubwa ni pamoja na kuwa na watu wengi wanaokula hayo mapato madogo na wizi humo humo ndani yake, hakuna utendaji wala ushindani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru katika kelele zetu *TANESCO* itapona, lakini iache kudeka; wakati mwingine hata hizo *capacity charge* nao walikubali, hakuna mahali walipowahi kusema walikataa, walikubali wanayajua hayo. Kwa hiyo, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wezangu kabisa kwamba waukubali Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kwa sababu nilipata kusikia Mbunge wenzetu mmoja alisema kwamba, wasiuze umeme nje hao wazalishaji wa umeme; ninafikiri hili ni zao sawa na korosho tunalouza nje na ni sawa na mahindi wakati mwingine tunayouza nje, pia ni sawa na kahawa tunayouza nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali wawape hao, kama kuna mahali wanapaita maeneo maalum ya uzalishaji kwa ajili ya *export*, ambapo panaweza kutengenza umeme, wapeni watengeneze umeme ambao tutautumia ndani, lakini wanawenza wakauza nje. Hili ni zao tu la biashara, tutapata fedha za kigeni waruhusuni pia kwa mfano, kule Mtwara wakifikisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii, lakini wapewe ruksa wauze umeme nje. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anna Abdallah, ninakushukuru sana, lakini pia ninakushukuru kwa sababu umesemea na Jimbo langu la Peramiho.

Waheshimiwa Wabunge, anayefuata sasa ni Mheshimiwa *Tatu Ntimizi*, lakini kwa kuwa simwoni nitamwita Mheshimiwa *Job Ndugai* na Mheshimiwa *Vita Kawawa ajiandae*.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kuhusiana na Muswada uliopo mbele yetu.

Nianze kwa kutoa pongezi nyingi sana kwa *Waziri*, Mheshimiwa *William Ngeleja* na *Naibu wake*, Mheshimiwa *Adam Malima* kwa usikivu wao katika mchakato mzima

uliopitia Sheria hii na kwa jinsi ambavyo wamewasikiliza Waheshimiwa Wabunge na kuzingatia yale ambayo tulikuwa tumeyapendekeza mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Kongwa, nitoe pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mbunge mpya wa Kiteto, ambaye kwetu ni majirani na wananchi wangu wengi sana wanalima kule kwake. Tunaomba ushirikiano ambao tumekuwa nao uendelee kuwepo na tunaahidi kabisa, tutaendelea kushirikiana naye katika shughuli za kuwaleta maendeleo wananchi wetu na Soko letu la Kibaigwa linategemea mahindi mengi sana kutoka katika Wilaya yake. Ninasema karibu sana Bungeni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumzia jambo muhimu sana, nalo ni kufikia mahali ambapo sekta hii ya umeme sasa inafunguliwa milango kiasi fulani ili pawe na ushindani. Ameeleza ndugu yangu mchana hapa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha kwamba, sekta hizi kubwa wenye we wanaziita zinazotoa *utilities*. Sekta kama ya umeme na maji, katika Mataifa mengi ni sekta ambazo zinashikwa na dola yenye. Sasa huo ndiyo umekuwa utaratibu wa kawaida, lakini dunia inabadilika na mambo yanabadilika na sisi kama nchi sasa tunaingia katika uwanja amba ni tofauti kidogo, kwa sababu uwanja huu unahitaji uwekezaji mkubwa sana. Uwekezaji amba si rahisi sana kuupata katika sekta binafsi, isipokuwa katika Mashirika makubwa ndiyo yanayoweza kuingia katika uwekezaji wa sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika ambalo limekuwa likitoa huduma kwa kiwango kikubwa katika nchi yetu ni *TANESCO*, ambayo kwa miaka yote hii hajafikia hata asilimia kumi ya mahitaji ya Watanzania kwa suala zima la umeme. Kwa hiyio ni vigumu sana, mtu mzima ukasimama leo ukaisemea *TANESCO*, kwa sababu *TANESCO* ya sasa ni kama *RTC* ya zamani, iliyokwisha ile. Mtu akiwa anajenga nyumba yake kule Kongwa pale Mjini, ambako huduma hii ipo, akitaka kuunganisha umeme ataanza kuweka msingi, atajenga nyumba na kadhalika na *TANESCO* hawajaja hata kumtembelea. Wakati hapo nchi jirani, ukichimba msingi tu, *Kenya Power Light Company* wanakuwa wamekwishafika; mzee tukikuwekea nguzo hapa unajua wakati huu tuna bei ambayo kidogo unaweza ukaimudu. Wakitoka watu wa umeme, wanakuja watu wa maji; mzee unajua hapa tukikuvutia bomba la maji tunaweza tukakupa kidogo ahueni fulani. Sisi hapa wao ni mabosi, wamekaa huko kama *RTC* ya zamani; ukishamaliza kujenga nyumba sasa uanze kuwafuata na watakuja wanapotaka wao. Wakija wana orodha; nguzo zinatakiwa tatu utoe hela wewe, vikombe utoe hela wewe, nyaya sijui zinatakiwa mita ngapi utoe hela wewe, mpaka posho ya vibarua utoe wewe; tunakwenda wapi? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyovvye vile, hatuwezi kuendelea na mzigo mzito kiasi hiki? Ujumbe ni kwamba, *TANESCO* lazima ibadilike. Huo ubosi haiwezekani; hatuwezi kwenda hivyo na bei zao wala siyo za soko ni bei za mtu aliyelelewa vibaya. Anaweka tu kuunganisha umeme ni shilingi 400,000, bila shilingi 500,000 hapa wewe umeme hupati, akitaka lipa hutaki shauri yako! Umeme ukiunganisha kwa mteja ni kitu ambacho matumizi yake, wewe umekwishakuwa mteja wa miaka mingi. *TANESCO* yenye sisi ukichelewa wiki moja wamekwishakuja kukukatia umeme, hata hawajali

kwamba huyo mteja wetu, wakitazama kwenye kompyuta malipo yake huwa yanakwenda namna gani, mteja huyu huwa analipa vizuri tu, ameugua au yukoje. Wakorofi kweli kweli! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme kukatika hilo ndilo suala ambalo halina muda, yaani ni saa yoyote umeme hakuna. Kama sisi *line* ya kwenda Kongwa – Mpwapwa, siku mbili kuwa hakuna umeme ni jambo la kawaida; mvua ikinyesha kidogo tu umeme hakuna. Kwa hiyo, kwa ujumla nikisimama kama Mbunge wa Kongwa hapa, nianze kusema *TANESCO*, kwa kweli huko sidhani kama watanirudisha, watasema huyu bwana ana matatizo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* ina matatizo kweli kweli, tunaiomba Serikali iiangalie kwa maana ya kufanya *restructuring* kubwa kabisa ili kurekebisha Shirika hili kabisa, liweze kutoa huduma inayotakiwa na kwa bei ambazo zinawezekana kwa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu huu wa kufanya kazi kama *RTC* ya zamani, hatuwezi kwenda. Jukumu letu kama Bunge ni kutunga sera, kwa maana ya Sera ya Nishati, sasa tunaitafsiri katika Sheria ili iendane na wakati, tukitarajia kwamba, tunachokifanya leo kitakuza uchumi na kwa maana hiyo kupunguza umaskini wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa sasa nilipokuwa ninazungumzia habari ya Mheshimiwa Aggrey Mwanri; uwekezaji huu kwa kawaida ni wa Kiserikali na ni wa Dola; leo tunaruhusu na watu binafsi. Kwa kawaida katika uchumi wa namna hiyo, lazima pawe na *balance* kati ya uwekezaji wa Kiserikali na uwekezaji wa watu binafsi. Kusipokuwa na *balance* nzuri, hao watu binafsi waka-*dominate*, tutapata tatizo kubwa na hapa niseme hata wenzetu wa Kusini, tunategemea tuwe na *supplier* mmoja anayeitwa *ARTUMAS*. Unapokuwa na mtu mmoja tu kwenye soko anayetoa huduma ni kitu cha hatari kweli, kwa sababu huyo anakuwa na *monopoly*. Lazima uwe na taratibu nzuri kweli za kuhakikisha kwamba, leo anakuja hivi; kesho akiamua kupandisha bei zake hamtaki anakata umeme mnafanya namna gani maana tatizo letu ni huo ukiritimba? Sasa Mheshimiwa Aggrey Mwanri ni mjamaa, alikuwa anazungumzia habari ya ukiritimba wa ujamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwajulishe leo hivi mnajua ule ujamaa na ukomunisti haujafa. Ule ujamaa wa ukomunisiti hivi sasa umehamia kwenye *Multi National Corporations*, Mashirika makubwa ya Kimataifa, Mashirika kama hayo yatakayowekeza kwenye umeme. Sasa hivi hayo Mashirika makubwa yanakaa pamoja, yanapanga mipango ya kupandisha bei za vitu na mipango ya kibiashara ili yafanye faida kubwa zaidi kuititia vitu vinaiviyotwa *joint ventures, acquisitions, mergers* na kadhalika na kadhalika; wanatengeneza *cartels*.

Mheshimiwa Aggrey Mwanri, ametaja mtu anayeitwa Adam Smith; mtaalam mkubwa wa uchumi. Alisema, ukiona watu wanaofanya biashara moja kwa kawaida

huwa hawakai pamoja, lakini ukiona wanakaa pamoja, basi ujue watazungumza wataishia kufanya njama za kupandisha bei dhidi ya walaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwahi kukaa mahali Fulani, wakati wa *crisis* ya umeme iliyopita ikaleta maamuzi ya ajabu, tukaambiwa mkubwa mmoja wa Serikali aliwahi kuwaita kwenye mkutano, wawekezaji wa Sekta ya Umeme kuona tunafanyaje? Akashangaa kwamba, katika waliohudhuria karibu wote ni Wazungu wa pale Dar es Saalam. Kwa hiyo, lazima tuwe makini tunakokwenda, kwa kawaida ule ujamaa niliokuwa ninasema umehama toka kwenye ujamaa tunaoujua sasa umeshikwa na Mashirika makubwa. Kwa maana kwamba, sasa yenye ndiyo yanafanya ile *monopoly*, yanatumia *principles* zile zile za ukomunisiti kwa *ku-merge*, yanakuwa sasa hayana washindani wa kushindana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika kuitisha Sheria hii, tuwe makini sana. Huyo *EWURA* ana uwezo wa kuwapiga *break* hao jamaa watakapoanza kukaa pamoja kisirisiri na vigumu kufahamu kwamba, hao wamekaa pamoja; tutujuaje ni kazi kubwa sana? Ndiyo maana katika nchi za wenzetu zilizoendelea, wanazo sheria kali sana zinazoitwa *Anti-trust laws* na sheria nyingine ambazo zinazuia *Anti Competition*. Je, sisi hapa tumejiandaa namna gani tunaporuhusu wawakezaji binafsi kuingia katika sekta muhimu kama hii ya umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejiandaa namna gani kuhakikisha kwamba, hao hawali njama; tumejiandaa namna gani kuhakikisha kwamba huko Kusini hata kwa *ARTUMAS* peke yake; miaka miwili, mitatu, mitano, kumi inayokuja patakuwepo na Kampuni nyingine ili pawe na ushindani wa haki ili mwananchi apate bei nzuri zaidi; tunahakikisha namna gani kwamba kweli hao wawakezaji binafsi wanaokuja watakuwa na nia na msukumo wa kuwekeza vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana hayo yaangaliwe kwa sababu mashirika makubwa hayaji hapa kufanya *charity*, yanakuja hapa kufanya biashara na katika kufanya biashara, wanachoangalia wao ni faida wakati sisi tunaopitisha Sheria hii tunachokiangalia sisi ni huduma. Lengo letu ni huduma kwamba, huduma itapanuka na itawafikia watu wetu, lakini hao tunaowaalika wanachoangalia hapa ni faida yao; hawaii hapa kufanya kazi ya Kanisa wala Msikiti. Kitachowafanya waende kwa taratibu zinazotakiwa ni *regulations* zetu, tuzitazame zimekaa kama sawasawa. Sheria zetu na taratibu zetu za kuhifadhi mazingira ili hao watu wasiharibu mazingira zimekaa sawasawa. Niliwahi kusikia kuna baadhi ya watu wanawaza kwa mfano, *Stigler's Gorge*. Wawekezaji binafsi, Mheshimiwa Waziri hilo tusilikubali hata kidogo, ikiwezekana tuwekeze sisi wenye. *After all Stigler's Gorge* iko ndani ya *Selous Game Reserve*, ambayo ni *World Hunting Site*.

Mahali ambapo kama tutaweka mgodi wa kuzalisha umeme, lazima pawe na uangalifu wa hali ya juu wa hifadhi ya mazingira. Tayari eneo lile ni la kidunia, hatuwezi kumpa mtu binafsi hivi hivi tu; atatuhakikishiaje mazingira pale yatatunzwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niseme tu kwamba, *TANESCO* kutokuweza kusambaza umeme sawa sawa, sisi Kongwa baadhi ya sehemu zina umeme lakini ni

chache sana. Nikumbushe kwa ajili ya rekodi kwamba, vijiji vingi sana bado havina umeme, ambavyo vinafaa kabisa viwe na umeme. Wananchi wa Kongwa wanafahamu, nimekaa kwa miaka mingi nikisemea habari hii ya umeme, lakini bado hatujafanikiwa kupata. Tunaomba vijiji hivi vitazamwe; umeme wa kuelekea Mkoka, Matongoro, Norini, Hogoro, Chamahe, Tubugwe, kule Ibwaga, Sagala, Idulo, Ngumbi na kadhalika, sehemu kubwa kabisa ya Wilaya haina umeme. Tunaomba Wizara ilitazame jambo hili la umeme vijijini na kwa hiyo fursa hii inayokuja, kwa namna yoyote ile, *tu-tune* kwa namna ambayo itawezesha huduma hii kuwafikia wananchi walio wengi. Tukifika hapo tutakuwa tumefanya jambo la haki kabisa kwa wananchi wetu. Nina hakika nia na madhumuni ya sheria hii, pamoja na mambo mengine ni hiyo, ndiyo maana tangu mwanzo nilisema kwamba, ninaunga mkono sheria hii kwa asilimia mia moja ili iende ikafanye kazi ya kuwaendeleza Watanzania. Ninashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia Muswada huu muhimu sana katika uchumi wetu. Nianze kwa kuwapongeza Waziri na Naibu wake, wenyе dhamana ya Nishati na Madini, Watendaji wote wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hii na Kamati yetu ya Bunge, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Kabla sijasahau, nami niseme ninaunga mkono Muswada huu, pamoja na maelezo ambayo nitaendelea kuyatoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Shirika letu la *TANESCO*; Shirila letu la *TANESCO* liliwekwa chini ya *PSRC* kwa ajili ya kubinafsishwa kwa takribani miaka mitano. Lilipokuwa kule *PSRC* kwa miaka mitano yote au zaidi, kulikuwa hakuna uwezekezaji wowote uliokuwa unaendelea; hakuna mfadhili kutoka nje, wala si Serikali ilikuwa inawekeza kwenye *TANESCO*. Kwa hiyo, matokeo yake Serikali ilipokuja kuamua kuliondoa Shirika hili kule *PSRC* na kulirudisha katika mkondo wa kawaida ili liendeshwe kama kawaida na liendelee kuwa mali ya Serikali, tukajikuta miundombinu yake ilikuwa imechoka sana na kwa kweli liko hoi bin taabani.

Sasa hili ndilo Shirika tulilolizoea na ndio Shirika pekee lililokuwa linatoa huduma ya umeme hapa nchini. Hapa mbele yetu, tuna Muswada wa kuifungua Sekta ya Umeme ili Sekta Binafsi nayo ichangie katika uzalishaji, usambazaji na usafirishaji wa umeme. Lakini ni ukweli usiofichika kwamba, katika mambo haya matatu; kufua umeme, kuusafirisha na kuuza kwa walaji wa mwisho, eneo la uzalishaji ndilo lenye maslahi makubwa na ndio rahisi kuliingia. Sasa eneo hili tusije kushangaa kwamba, ndilo hilo litakalowavutia wawekezaji wengi kutoka nje au Sekta Binafsi kwa maana hiyo. Kwa kuelewa hivyo, nilikuwa ninataka niishauri Serikali ifanye haraka, ilirekebishe Shirika letu hili la *TANESCO* ili liwe na hizi sehemu tatu kila moja peke yake; kuzalisha umeme, kuusafirisha na kuuza kwa walaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseje nikasahau kwamba, dhamira yangu hasa ni kuhakikisha kwamba, Serikali sasa inawekeza katika Shirika lake hili la *TANESCO*, ambalo kwa vyovyyote vile tusiliachie likafa. Tuna kila sababu ya kulifanya liendelee kuwepo, hata kama sekta hii sasa tunaifungua kwa wawekezaji binafsi, kazi kubwa bado itafanywa na Shirika letu la *TANESCO*. Kwa mustakabali huo, ninashauri kwamba, *TANESCO* ya sasa kama ilivyo, iko hoi bin taabani kifedha, mwenye mali ni Serikali na

kwa maana hiyo ni sisi Watanzania wote. Ninasisitiza kuwa, kuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba, *TANESCO* inasimama na inafanya kazi zake kama tulivyoitarajia. Kinachotakiwa kama nilivyosema, tuwekeze kwenye *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na mahesabu ya hivi karibuni ya *TANESCO* katika kipindi cha mwaka 2005/2006, walipata hasara ya takriban shilingi bilioni 130. Kwa maana hiyo, kusema kweli kama ingelikuwa Kampuni ya mtu tu hivi hivi, hii Kampuni haipo kwa maana ya kifedha ni *insolvent* au *bankrupt*. Ipo tu kwa sababu ni Kampuni ya Serikali. Sasa Serikali iendelee kuhakikisha inakuwepo kwa kuwekeza zaidi kmtaji. Kwenye mahesabu ya *TANESCO*, kuna hesabu zinaonekana kama mkopo kutoka Serikalini kwenda *TANESCO*. Hiyo lugha ya mkopo kutoka Serikalini kwenda *TANESCO* iondoke na hiyo mikopo yote iwe ni mtaji wa Serikali ndani ya *TANESCO*. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanya hivyo, Serikali kama ambavyo sasa hivi imekwishafanya, isafishe mizania ya *TANESCO* kwa kuiondolea madeni yote iyabebi na kila deni libadilike liwe mtaji. Ukiashafanya hivyo, vunja *TANESCO* katika mafungu matatu au mawili, moja *generation*, lingine liwe la *transmission* na mwisho *distribution*. Hili la *generation*, Serikali ifungue liwe la watu wote, litolewe kwa watu wanunue hisa kule kwa sababu ndiko kunakotengenezwa fedha. Ndiyo maana haya Makampuni ya nje ya *DOWANS*, *RICHMOND*, *AGGREKO*, yakija tunapata matatizo kwa sababu ndio kwenye fedha huko. Kwa hiyo, tunataka *TANESCO* yetu na sisi ifunguliwe, tununue hisa huko kwenye eneo la uzalishaji. Tukishanunua hisa huko kwa sababu tutakuwemo humo, tutasaidiana kuliendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyotevyote vile, *transmission* ibaki chini ya Serikali. Hizi ni njia kuu na nyeti zinazosafirisha umeme kutoka Kidatu, Mtera, Hale na kadhalika, kutoka Iringa, Dodoma, Shinyanga, Mwanza, Nzega, Tabora na Dar es Salaam. Hizi si njia za kumwachia mwekezaji binafsi, ziendelee kuwa chini ya Serikali. Aidha, kuna haja ya kuongeza uwekezaji kwenye *transmission*; sasa hivi *transmission line (National Grid)* yetu imeelemewa. Mwaka huu hivi tunaposema, *transmission* yetu imeelemewa kwa kiasi cha asilimia kumi. Mzigo unaopita kwenye *transmission line/National Grid* imezidiwa ule mzigo umezidi kwa asilimia kumi. Mwaka kesho tukienda kwa hatua hii tunavyokwenda, kwa *demand* kuendelea kuongezeka. Mzigo utaielemea *transmission line* iliyopo kwa asilimia 33.7. Kwa hiyo, kuna haja ya kufanya uamuzi wa haraka sana kuwekeza kwenye *transmission*. Simwoni mwekezaji kutoka nje, ambaye atakuja hapa aseme anataka kuwekeza kwenye *transmission line (National Grid)*, kama yupo nitamsifu sana, lakini kazi hii ni ya Serikali. Serikali iwekeze kwenye *transmission line (National Grid)* na tutatengeneza pesa kwa wale wanaokuja kuwekeza kwenye uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, swali la msingi hapa ni kwamba, Serikali isafishe mizania ya *TANESCO*, iondoe madeni iwekeze kwa njia ya *equity* na kwenye upande wa *transmission* ibaki chini ya Serikali. Ukiangalia kwa ujumla, umeme unaozalishwa nchini sasa hivi, pamoja na *emergency power supply* ni megawati hazizidi 1,000. Matumizi ya hapa nyumbani ambayo ni ya kujibabanana,

maana yake tunaambiwa ni asilimia kumi tu ya Watanzania ndio wanapata umeme. Kwa maana hiyo, kama tunataka kila Mtanzania au sehemu kubwa ya Watanzania tufanye asilimia 50 ya Watanzania wapate umeme, maana yake hizi megawati 1,000 zinazozalishwa sasa hivi, zipande mpaka angalau megawati 5,000 na ndio sababu tunasema, tunahitaji wawekezaji katika Sekta Binafsi kuisaidia Serikali. Bila Sekta Binafsi kuja kuwekeza, Serikali peke yake haiwezi kwa mara moja kukidhi mahitaji hayo, ambayo kila aliyesimama anasema kijijini kwake hakuna umeme na mimi sasa hivi ninasema hivyo hivyo kwamba, katika Mji wa Tabora umezunguuukwa na kata tisa ambazo ziko nje ya mji na hazina umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata hizo ni Tumbi, Kakola, Itaga, Misha, Nderelwa, Intonjanda, Itetemia, Kalunde, wote hawa hawana umeme pamoja na kwamba, wanauzunguka Mji wa Tabora. Kwa maana hiyo, tunahitaji uwekezaji mkubwa katika kuzalisha umeme. Ndiyo maana ninakubaliana na rai ya kuruhusu Sekta Binafsi iingie iisaidie Serikali, kwa maana hiyo *TANESCO*, katika kuzalisha umeme. *Transmission line (National Grid)* ibaki mali ya Serikali, *generation* ya *TANESCO* iondoke kwenye lile Shirika kubwa. Kwanza ni kazi kubwa kui-manage *TANESCO* katika hali yake ya sasa ilivyo, ndiyo maana ninasisitiza sana kuivunjavunja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule upande wa Kusini, tayari ameshapatikana mwekezaji ambaye ameonyesha dalili za kuwa radhi kuwekeza katika uzalishaji na usambazaji naye si mwininge isipokuwa ni *ARTUMAS*. Ninakubali Serikali iendelee kuzungumza na huyu, kwa sababu yeye tayari Serikali kwa kupitia Shirika la Holland linalojulikana kwa jina la Oriet, wamekwishapata asilimia 50 ya gharama za mradi huo kwa njia ya msaada kutoka Netherlands. Asilimia 20 watawekeza kwa njia ya hisa wenyewe *ARTUMAS* na asilimia 30 watawekeza kwa njia ya mkopo. Tayari hizi *financial line up* zipo.

Kwa hiyo, hawa waruhusiwe waendelee lakini hawawezu kuruhusiwa kama sheria hii haitopita. Kwa kuanzia, sasa hivi wanazalisha megawati sita, lakini wana mashine za kuzalisha mpaka megawati 18, lakini wanatarajia kuzalisha mpaka megawati 300 ikiwa wataruhusiwa kuendelea kuzalisha. Ikiwa hizi tunaziona nyangi, ninaungana na Mheshimiwa Anna Abdallah aliposema na kweli kabisa nchi yetu lazima ibadilishe sura ya *exports* zetu. Sio lazima tu-*export* mahindi, pamba au tumbaku peke yake. Tunaweza tuka-*export* umeme vile vile. Masoko ya jirani yapo, kwa hiyo, kama tunadhani umeme huu ni mwinci sana, tutafanya *cross border trade* na wenzetu ambaa wanahitaji umeme huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe mahitaji ya umeme nchi hii bado ni makubwa sana. Kwa mfano, tunaweza vile vile tukiwa na umeme mwinci, tukafanya hata njia zetu za reli zikatumia umeme badala ya mafuta. Ukipshaweka umeme kwenye *railways*, maana yake ume-*improve* ile *efficiency* ya mwenendo mzima wa treni zetu na tutaondokana na utaratibu wa sasa wa treni zetu kwenda taratibu kwa sababu zinakwenda kwa injini za kizamani. Kwa hiyo, mahitaji haya ya umeme, viwanda vinakua, migodi ndiyo hiyo inakua, sasa suala la kusema kwamba, umeme utakuwa mwinci sana utatushinda halipo. Ukweli ni kwamba, hatujaweza kuzalisha umeme kwa kiasi ambacho uchumi huu

unahitaji. Migodi yetu karibu yote inatumia mitambo ya dizeli na hao ndio wanaoitwa *hanker tenants*. Ukishawaona hawa *anchor tenants*. Ukishawapata hawa *anchor tenants* - Bulyankulu, Buzwagi na Geita, hakuna wasiwasi kwamba watalipa bili zako. Leo hatujayafikishia umeme haya makampuni kwa sababu *transmission line* zetu hazijafika huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ninahimiza Serikali iwekeze kwenye eneo hili la *transmission*. Kuna haja ya kuongeza *transmission line* nyingine kutoka Iringa, Dodoma, Shinyanga mpaka Mwanza, ilekee Geita, iende mpaka ifike Kigoma kwa jamaa zangu kule, iteremke mpaka Rukwa ije kuungana huku na *Mbeya National Grid*. Hizo ndio *infrastructure* ambazo tunazizungumza siku zote; tunapozungumza *infrastructure* kwa ajili ya maendeleo ya uchumi sio barabara peke yake, tatizo ni kwamba, sisi tunaposema *infrastructure* wengine wanadhani ni barabara tu; sio barabara peke yake ni pamoja na umeme, reli na bandari, lakini leo somo letu hapa ni umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninakubali Sekta hii ya Umeme ifunguliwe kwa watu binafsi. Yapo mengi ya kusema kwenye vifungu, sasa bahati mbaya muda ni mfupi, ninadhani nitasimama wakati wa vifungu kuchangia ni vifungu gani ninahitaji vibadilike. Ahsante sana.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie katika Muswada huu wa Umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, niwapongeze Wizara ikiongozwa na Waziri, pamoja na Naibu wake. Pamoja na kwamba, Muswada huu uliletwa na tukaukimbia kama Mwenge na pia Wabunge wakakimbizana nao kama Mwenge mpaka tukaweza kurekebisha vifungu 20; Muswada huu tunaweza kusema umetayarishwa kati ya Wizara na Wabunge. Kwa hiyo, ninawapongeza wote kwa kazi nzuri. (*Makofii*)

Ninaipongeza sana Kamati ya Nishati na Madini, kwa kushirikiana na Wizara vizuri sana mpaka tukafikia hapa. Kwa hiyo, kwa sasa ninabadilika ninaunga mkono hoja, maana mimi ndiye niliyosema kwamba, Wizara ilikwishapoteza sifa za kuzungumza na Wabunge, sasa ninaona inakuja vizuri kwa hiyo, ninaipongeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatofautiana kidogo na hii dhana ya kufanya uzalishaji wa umeme uwe huria. Sawa tukubali uwe huria, lakini Serikali iisimamie vizuri *TANESCO*. Serikali i-*empower TANESCO*. *TANESCO* ndiyo Serikali itakuja kurudia huko. Lazima Serikali iwe na chombo chake cha kuzalisha, kusambaza na kuuza umeme ambacho ni *TANESCO*. Hatuwezi hata kidogo kuwaachia watu binafsi na ninataka kuitahadharisha Serikali, hawa wanaokuja hawawezi kupeleka umeme vijijini, wanataka kuja kuuza umeme mjini, hawatakenda vijijini. Mpaka sasa hivi tumeweza kusambaza umeme kwa mujibu wa *TANESCO*, kwa wateja 670,000 tu. Hawa wateja 670,000 ndio wanatuuhangaisha, ndio wanatupeleka kuhangaika kuleta Makampuni ya kuzalisha umeme wa dharura na kulipa fedha nyangi za walipa kodi kwa Makampuni haya bila ya sababu yoyote. Pesa tunazolipa kwa hawa wanaozalisha umeme wa dharura, *capacity charges* ni za wakulima wa Tanzania; wakulima wa pamba, wakulima wa

korosho na tumbaku; kwa mikataba hii ambayo sio sahihi, tunawalipa kila mwezi hawa wanaojiita wafuaji umeme wa dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono *TANESCO* ipewe fedha, tuwe na uzalishaji wa umeme ambao unasimamiwa na Serikali. *TANESCO* waende RUHUDJI wanaweza kuzalisha umeme kule kwa mujibu wa taarifa zao, megawati 350. Waende Rumakari kuna megawati 222, waende *Stigler's Gorge* ambapo wawekezaji Wazungu wanalenga pale, tusiwaruhusu hawa wawekezaji binafsi waende *Stigler's Gorge* ambapo kuna megawati 1,200. *TANESCO* waende Mnazi Bay, kwa sababu tukiwaachia *ARTUMAS* peke yake, hatuwezi kuwapangia bei, lazima kuwe na ushindani. Kwa hiyo, kama *ARTUMAS* watashusha na *TANESCO* pia watashusha, tuwapeleke kule vile vile. Waende pia Mchuchuma na kule Malagarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie hawa watu wa *capacity charge* ili na Watanzania waweze kuona ni jinsi gani sisi tunapoteza pesa. *IPTL* tunawalipa kila siku shilingi za Kitanzania milioni 114 kama *capacity charge*. *SONGAS* wanalipwa shilingi 243,600,000 kila siku kama *capacity charge*. Hawa *SONGAS* hawajaleta hata *equity*, hawajaingiza hata senti tano hapa Tanzania, wamekuja kwa ujanja ujanja kwa kutumia pesa ya Serikali yetu sasa tunawalipa kila siku shilini 243 milioni. *AGGREKO* tunawalipa shilingi 57,600,000. *SONGAS* tuna mkataba na wao wa miaka 20, wataendelea kulipa pesa hizo za Watanzania. Hawa *DOWANS* ambao tumepiga kelele hapa, bado wanaendelea kulipwa; Mheshimiwa Waziri hatujapata taarifa kama zile fedha wanazolipwa shilingi milioni 146 zimesimamishwa au hazijasimamishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hii Kampuni inaitwa *Kiwira Coal Mine Limited*, ilikuwa ni Kampuni ya Umma ya Watanzania. Wachina wali-invest bilioni nne pale. Mwaka 2004 aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Daniel Yona, akaanzisha Kampuni pamoja na mwenzi wake, Rais Mstaafu, inayoitwa *Tan Power Resources Company Limited*. Mwaka 2005 Juni, wakauziwa bila utaratibu wowote, bila hata kutangaza Kampuni hii ya Umma ya *Kiwira Coal Mines* kwa shilingi 700 milioni, wakalipa *downpayments* shilingi milioni 70 tu. Mwaka 2006, bila ya utaratibu unaoeleweka, wakaingia mkataba na *TANESCO* wa kufua umeme kule Kiwira; sasa kuna *capacity charge* kwenye mkataba wa 2006 ya kulipwa milioni 146 kila siku. Mimi ninataka njiulize hivi huu ni uadilifu; huku si kukiuka maadili ya uongozi? Hawa Mawaziri vijana tunaowaweka watapata mfano gani kutokana na hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Naibu Waziri kule Mkuranga kuna gesi, basi na ye ye aunde Kampuni achukue ile gesi. Lazima tufike mahali tuseme inatosha. Mheshimiwa Rais alisema ye ye Urais wake hauna ubia, Watanzania walimpa kura, walimpa ye ye na anajua anataka kuipeleka wapi Tanzania. Sasa hawa wanaomvuta shati na koti asiweze kuelewa, asahau yale malengo aliyopanga ya kuwapeleka Watanzania kwenye maisha bora lazima aseme sasa mwisho. Tupange sasa maendeleo ya Watanzania, hawa wanaotuhujumu wanaturudisha nyuma, tuwaambie basi sasa mwisho na waendelee kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nitalahirisha mpaka wakati wa bajeti, Mheshimiwa Waziri aje na majibu kama haji na majibu asilete bajeti yake hapa. Kwa sababu kikao hiki ni cha kutunga sheria na mimi katika sheria hii, ninaomba niongezee hapo neno; *Clause 41 subsection 7* wamesema kwamba, haya Makampuni ambayo yana capacity charge, yasiruhusiwe kuingia kwenye kuuza umeme mpaka wakae miaka mitano, sawa lakini tuongezee hapo je, kama wakiiza au wakiwapa watoto wao maana yake watoto wao ataruhusiwa kuendelea; sasa tuwafunge kwa kipengele hiki pale mwisho *subsection 7*, tutunge sheria sasa tuongeze kifungu hiki kwa Kiingereza: “*This provision will apply mutatis mutandis to any entity acquiring the assets through ownership thereof.*”

Ninaomba kifungu hicho kiwekwe, kisipowekwa nitakuja mwishoni na *schedule of amendments*. Kwa hiyo, ninakuombeni ili tuweze kwenda vizuri, tukubaliane na haya Wabunge wanayoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu wa Umeme, ultaka kutugawa hapa. Wabunge wengine walisema sisi wa Kusini mnatuonea, wengine sisi wa Kigoma, wengine wanasema sisi wa Tabora, wengine wanasema huko Kilimanjaro umeme upo mpaka kwenye migomba si kweli? Umeme Kilimanjaro hakuna, upo kama ulivyo mijini; kwenye vijiji ni vijiji vichache vina umeme na vyenye umeme huo sasa hivi ni kama kibiriti hauwaki na hautoshi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, ninakuomba hapa tuzungumzie mambo ya utaifa, hatuzungumzii mambo ya Kilimanjaro, Mtwara, Tabora, Kigoma. Tunataka kila mtu apate umeme na ili kila mtu aweze kupata umeme, lazima uweze ku-*impower TANESCO*. Tumebinafsisha *ATC* tumeirudisha, tumebinafsisha *DAWASA* tumerudisha na mimi ninakwambieni haya makampuni ya *utility* ni makampuni ambayo lazima Serikali isaidie. Pesa tunazokusanya lazima ziende kuwasaidia Watanzania, lazima zipeleke umeme vijijini. Kwa hiyo, sikubaliani hata kidogo na hao wanaosema *TANESCO*, ndiyo kweli ipo hoi, lakini ifufuke. Kama haiwezi kufufuka tutaiwajibisha, wapo watu waadilifu tu ambao wanaweza kufanya kazi za *TANESCO* na zikaenda. Kwa hiyo, tutawapeleka huko na Serikali ipeleke pesa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vita hii ya uchumi, lazima tuangalie ni watu gani wanakaa *front line*. Wapo wengine wanapiga kelele tu hapa, lakini mguu wao mmoja upo Tanzania mwininge upo Canada na mwininge upo Uingereza. Kwenye vita hii ya uchumi hatuwezi tukawapeleka mbele, hao lazima tuwaache Kambini wakipika na kusafisha mestini kwa Sababu hatutashinda. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria muda  
wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kimaro ni kengele ya pili.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ninaunga mkono hoja na ninaomba Waziri azingatie yale niliyoyasema.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu katika hoja ambayo tunaijadili hivi sasa. Awali ya yote, bado sijashawishiha kuiunga mkono hoja hii, labda pale nitakapopata maelezo ya ziada kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Ninasema hivyo kwa sababu nilikuwa ninapitia hiki kitabu kidogo, ambacho kimetolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu kinasema ni mwelekeo wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, kipindi cha 2005 hadi 2010 na Ahadi za Mgombea Urais 2005. Kimetolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu si kitabu cha CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema kwamba sishawishiki kuunga mkono hoja hii kwa sababu ya ukurasa wa tano pale panaposema kwamba, ninaomba ninukuu kwa ruhusa yako: "Serikali itaunganisha Mikoa ya Ruvuma na Kigoma kwenye Gridi ya umeme wa Taifa." Rukwa haipo, nitataka maelezo kwa nini Rukwa haimo katika mpango wa kuingizwa katika Gridi ya Taifa. Ni kweli kabisa katika nchi yetu Ruvuma, Kigoma hata Kagera hazimo katika Gridi ya Taifa. Hivi ni kweli kwamba, *ARTUMAS* ataondoa matatizo ya Rukwa na Kigoma? Tusiipeleke nchi hii katika maeneo, tunazo kila sababu za kukubaliana na kuwepo kwa kampuni hiyo katika Mikoa ya Kusini, lakini bado si ufumbuzi wa umeme katika nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tukubali kabisa kwamba, hakuna mjomba atakayekuja katika nchi hii kutusaidia na kutuondolea matatizo ni sisi wenye Watanzania. Bila sisi wenye kujipanga vizuri, matatizo haya hatuwezi kuyamaliza. Sheria na maelezo aliyojatoa Mheshimiwa Waziri hapa ta kututoa hofu ya kwamba, *TANESCO* haibinafsishwi, mimi nimefarijika sana. Mheshimiwa Waziri, utaiingizaje *TANESCO* kwenye ushindani wa biashara huru, ya haki na ya usawa wakati ipo katika hali hii? Haiwezekani ni lazima kwanza ingejengwa *TANESCO*, ikaandaliwa ili iweze kuingia katika ushindani wa biashara ndipo mkafungua milango. Hamuwezi kufungua milango katika Sekta hii ya Umeme wakati *TANESCO* ipo katika hali hii. Mimi siwezi kugeuka jiwe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuitengenezee mazingira ili *TANESCO* iweze kuingia katika ushindani. Tusidanganyane, leo *TANESCO* si kampuni ya biashara, pamoja na kwamba, inafanya biashara ni kampuni inayotoa huduma na inavishwa majukumu ya kisiasa. Leo tunaambiwa kwamba, haya makapuni tutakayoyaleta yataapeleka umeme vijijini. Wakati inavunjwa *NBC* na kuanzishwa kwa *NMB*, tuliamiwa maneno hayo hayo. Tuliamiwa *NMB* itakuwa ni Benki ya wanyonge itakayopeleka huduma zake vijijini. Juzi hapa Mheshimiwa Simbachawene aliomba Benki Kibakwe akaungwa mkono na Mheshimiwa Killimbah na Mheshimiwa Mpina, wote wanahitaji Benki katika miji yao inayofanana na Mji wa Kibakwe. Walijibiwa nini humu ndani ya Bunge?

Walijibiwa kwamba, *NMB* sasa inafanya biashara ina vigezo, kama Kibakwe itatimiza vigezo hivyo, ndiyo itafunguliwa Benki; kinyume na matarajio na maelezo

yaliyotolewa ndani ya Bunge kwamba, Benki hii itakwenda vijijini, leo tunaambiwa kwamba, kuna vigezo na hawa ambao sasa mnasema watafika vijijini wataweka vigezo, kwa sababu ni wafanyabishara. Hawawezi kupeleka umeme, leo hii ukisema *TANESCO* sasa hivi ni kampuni ya biashara, ukamwachia Dr. Rashid kwamba endesha kampuni hii kibashara, jambo la kwanza atakalofanya ni kufunga umeme Mpanda. Ndiyo hatua ya kwanza, atakayochukua Dr. Rashid, kuzima umeme Mpanda kwa sababu gharama za kuzalisha umeme na mapato wanayopata *TANESCO* kule Mpanda hazina uwiano, lakini watu wa Mpanda wanahitaji umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kilo moja ya mchele Mpanda ni shilingi 2,000; tatizo umeme. Mashine zimesimama hazizalishi umeme, vinu vya umeme vimesimama hakuna mchele, bei imepanda maradufu. Ni wazi kabisa kwamba, *TANESCO* leo kama mnasema sasa inafanya biashara, maeneo yote ambayo yanatia hasara kwenye *TANESCO* watazima umeme, mtasema nini na mtawaambia ni hawa Watanzania ambao mnataka kwenda kuwanyang'anya umeme? Hatua ya kwanza ilikuwa ni kuirekebisha *TANESCO*. Imefikishwa hapo ilipofika, kuna watu wamesoma wana elimu na ujuzi, wangeweza kuiendesha, lakini imefikishwa hapo moja ni maamuzi ya kisiasa. Labda siasa itoke katika *TANESCO*. La pili ni ufisadi. Watanzania wanalipia ufisadi, kwa hiyo, ninamtahadharisha mdogo wangu, Mheshimiwa Ngeleja ni lazima awe makini katika mikataba itakayofuatia baada ya kutunga Sheria. Ninajua itapita, pamoja na sisi wawili, watatu, tunaosema hatukubaliani nayo, lakini itapita. Lazima waangalie mikataba watakayoingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii inahitaji mtaji mkubwa, ili watu waweze kuwekeza katika sekta hii wanahitaji misamaha ya kodi. Mnasemaje, tumejiandaa namna gani kuhusu eneo hili la misamaha? Tumepoteza mabilioni na mabilioni ya fedha kwenye misamaha ya kodi kwenye Sekta ya Madini, sasa mnahamisha kutoka kwenye madini mnapeleka kwenye umeme kwamba, misamaha itaendelea kutolewa, tutaendele kupoteza. Watapewa mafuta, wataingiza magari, wataingiza mitambo kwa misamaha ya Mawaziri. Misamaha iwe na kikomo katika mikataba watakayokuwa wanaingia na makampuni yatakayokuwa yanakuja kuwekeza hapa nchini. Hivi tumefumbwa macho, hatuwezi kujifunza kutokana na yaliyopita?

Japo lipo darasa la kutosha kabisa katika kuelekea katika masuala haya ambayo tunayafanya hivi sasa. Ukiangalia nguvu inayotumika sasa hivi kwa Muswada huu si ya kawaida; zimeendeshwa semina, kuna wataalam ambao wapo hapa Dodoma unakuwa na maswali mengi kuliko majibu; kwa nini Serikali itumie nguvu kubwa kiasi hiki kwa ajili ya Muswada huu; hivi kweli Muswada huu ni wa kuwasaidia Watanzania?

Mimi ninapata hofu, ninaona nguvu inatumika ni kubwa sana kwa ajili ya kuusukuma huu Muswada, tofauti na Miswada mingine ambayo nimeshiriki kuipitisha katika Bunge hili. Kama kweli Muswada huu unalenga kuwaondoa Watanzania katika matatizo, basi Mheshimiwa Waziri unastahili kupongezwa sana tena sana. Ninachojua, pamoja na Sheria inasema kwamba, *transmission line* zitakapojengwa na alijaribu sana kutushawishi katika maelezo yake kwamba, kila mahali katika kijiji ambapo *transmission line* mpya itakapopita, basi ni lazima wateremshe umeme katika kijiji hicho, ni jambo

zuri. Sheria inasema nini katika vijiji ambavyo tayari *transmissions line* zinapita na umeme haujateremka? (*Makofi*)

Niungane na Mheshimiwa Kaboyonga, kuhusu *transmission line* kwamba, zibakie kuwa mali na jukumu la Serikali. Sasa hivi Serikali inajaribu kujitoa katika kila kitu hata vile ambavyo ni wajibu wake kuvisimamia, huwezi kuiacha *transmission line* katika mikono ya watu binafsi, lazima ibaki katika mikono ya Serikali. Hata pale ambapo makampuni ambayo ninajua hayawezi kufanya, hata huyo *ARTUMAS* ukimwambia ajenge *transmission line* mpaka Peramiho hajengi na akijenga wewe wa Peramiho huwezi kuununua huo umeme ni lazima arudishe *investment* yake. Tunafanyaje? Hapa ni lazima kuwepo na *PPP*. Lazima Serikali isaidiane na makampuni hayo katika kujenga hizo *transmission lines* na hatimaye iweke bayana katika mikataba hiyo kwamba, baada ya muda fulani, *investment* ikirudi, *line* hizo zinabakia kuwa mali ya Serikali. Tunasema tu, lakini ukiangalia gharama watakazoweka za kusambaza na kujenga njia za kusafirisha umeme; umeme hauwezi kununulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimalizie kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, nitaunga mkono hoja hii iwapo atanieleza *TANESCO* iko katika nafasi gani; ni kampuni ya kibiashara au ni kampuni ya huduma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii ili niungane na Wabunge wenzangu, kutoa mchango wangu kwenye Muswada uliopo mbele yetu. Nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, maana hapa amepata uzoefu wa kutosha. Mikiki mikiki iliyokuwepo, bahati nzuri mdogo wangu umejitahidi mmefika pazuri, hongera sana mdogo wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia Muswada huu na kubaini kuwa, umeandalishi kwa lengo la kuondokana na tatizo la siku nyingi la Sekta ya Umeme nchini, kwa sababu hiyo ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Umeme ni moja kati ya sekta zinazochochea maendeleo na uchumi wa nchi yetu na hivyo ikiratibiwa vizuri na baadae Muswada huu kuwa Sheria, tutapiga hatua kubwa sana. Ninaamini viwanda vitakuwa miundombinu na kwa ujumla uchumi utasogea mbele. Moja ya mambo yanayonipa msukumo zaidi niunge mkono Muswada huu ni Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, kifungu cha 43(a)(3) na (c), ninaomba ninukuu: "Kupanua wigo wa aina za vyanzo vyaa umeme na nishati nyingine, kwa lengo la kuwezesha umeme wa kutosha kukidhi mahitaji ya uzalishaji viwandani na matumizi ya nyumbani; umeme wa gesi ya Mnazi Bay kwa ajili ya Mikoa ya Mtwara na Lindi; na kuongeza kasi ya kupeleka umeme vijijini kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini, utakaoshirikisha Sekta Binafsi na Wahisani. Hii ndiyo safari ya utekelezaji kwa yale tuliyowaahidi Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipewa kura za kutosha kwa kutumia Ilani hii. Kwa hiyo, leo hapa ninapowasilisha, ninaona ni safari ya utekelezaji ndiyo maana nimeridhika

kuunga mkono hoja. Ninatambua kule kwangu ambako hakuna umeme karibu katika Kata zote, safari hii ni nzuri hii, kwa hiyo, nirudie tena kusema ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuitahadharisha Wizara ya Nishati na Madini katika maeneo yafuatayo kama ushauri tu: Kwanza, nimeridhishwa na suala zima la *Rural Electrification* kama lilivyo katika *section 38 – 39* na *section 6(1)(b)* ambavyo vinaeleza dhahiri kwamba, umeme utapelekwa vijijini na kwa sababu Watanzania wengi wanaishi kule, hii ni safari nzuri. Ninamtahadharisha, ipo tabia imejengeka tumeona Songsongo kule chini ya utaratibu wa *Songas*, panapozalishwa umeme hawahudumiwi watu pale badala yake unakwenda kwenye maeneo mengine ya miji kama Dar es Salaam. Kwa hiyo, wakati tunapitisha huu Muswada na baadae kuwa Sheria, ninaomba hilo lizingatiwe. Pale ambapo ndiyo chanzo cha umeme, watu wanaozunguka maeneo yale waanze kunufaika na rasilimali iliyopo, badala ya kukimbiza maeneo mengine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetarajia ndugu yangu, Mheshimiwa Hawa Ghasia kule Mnazi Bay basi watu wake wa Namnyamba, Milongodi na kadhalika wanufaika. Katika hali hiyo, Kata zangu zile za Kitama, Mahuta, Luagala, Mnyawa, Namikupa na Tandahimba, zinufaika maana ndiyo kule unakotoka badala ya kuukimbiza kwenye miji mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ninataka niitahadharishe hii Wizara pia, liko tatizo la Taasisi, pamoja na Watendaji wa Wizara hii ya Nishati ya Madini wana *procedures* ambazo ni *complicated* na ninaweza kutoa mfano hapa; wakati *ARTUMAS* wanaruhusiwa kuanza kuweka mchakato wa kuweka miundombinu ya umeme kwa ajili ya Mtwara na Lindi ile inayoitwa *National Negotiation Team*, ilichukua mwaka mmoja hawajafikia makubaliano yoyote. Lakini ilipofika Mheshimiwa Mrope na Mheshimiwa Mudhihir kuingizwa kwanza, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Dr. Msabaha maana amefanya kazi kubwa sana walikuja na ikachukua mwezi mmoja tu kujulikana safari ya kukamilisha kwa mindombinu hii ya *ARTUMAS*. Sasa unaweza ukaona, hawa watendaji wengi walioko kule wana matatizo makubwa, sijui tuseme urasimu au ndiyo vijisenti au nini? Nilitaka nitoe tahadhari kwamba, tunakuja sasa kwenye mazingira haya, jamani tuache hayo mambo, nia hapa ni kujenga nchi yetu. Tukiendlea na *complicated procedures* hizi hatutafika. Tutaanza kulalamika na kuzalisha mambo mengi ambayo hayana msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpendezwa na Kifungu cha 8(4) kinachopendekeza ushindani wa huduma. Hii ni safi kabisa, lakini ninaomba wakati wa kutengeneza *regulations*, tuweke angalau kila mkoa makampuni mawili au zaidi, isiwe kampuni moja tu. Kukitokea tatizo wakileta *complications* na wao wataacha gizani na ile miundombinu iliyowekwa inaweza tena isitusaidie, tukatafuta mambo mengine baadae ambayo ni kujirudisha nyuma. Kifungu cha sita cha Muswada, kifungu kidogo cha tatu, lipo suala la mapendekezo ya adhabu. Ninapenda kushauri adhabu iliyotolewa pale ambayo inasema si zaidi ya milioni tatu kwa mtu atakaye-violet set procedure, ninaomba iongezwe kwanza kwa makampuni yanayokuja kuwekeza umeme ni matajiri haya; unayapaje adhabu ndogo ya milioni 300; si atatoa tu atafanya madudu yake atalipa hataonekana? Tuanze na isiwe chini ya zaidi ya milioni mia moja, ninaomba hilo pia lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kifungu cha 18 cha huu Muswada, kifungu kidogo cha tatu na cha nne, ambapo kuna *ecemption* za leseni. Ninaomba watu hawa kila mmoja apewe lesini bila kujari anazalisha umeme mdogo kiasi gani. Tusipoliangalia hili, watakuja kututapeli na kutuibia hapa. Hata kama anazalisha megawati moja, kama unaweza kuitisha kijijini zaidi ya watu 200 apewe *fee* inayolingana na umeme anaozalisha na sio kuwapa *loophole* ya wao *ku-capitalize gap* lililopo; hilo pia nilikuwa ninaomba Mheshimiwa Waziri, utililie *consideration* ya juu. Pia kifungu cha nne, sina hakika na *schedule of amendments* kama zipo sawasawa, lakini *section 23 - 25* inaongelea mambo ya *tarrif and charges*.

Ninaomba tu-set standards isije ikatokea eneo au kampuni fulani ikawa na bei tofauti na maeneo mengine. Tutaanza kulalamikiana hapa na kusumbuana kama umeme Mtwara ni shilingi tano Kagera uwe shilingi tano, Zanzibar uwe shilingi tano na mahali pengine ni shilingi tano. Tofauti hii haina haja kuwepo. Nilitaka hilo pia lichukue nafasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* sina matatizo nayo, lakini Mheshimiwa Kaboyonga alitangulia kusema, Gridi ya Taifa inayoendeshwa na *TANESCO* imezidiwa, kama nimemsikia sawasawa alisema, kwa asilimia kumi na itakapofika 2009 itazidiwa kwa asilimia 33.7. Kwa hiyo, kuletwa Sheria hii ni wakati muafaka, maana ndiyo sasa italeta nafasi ya ushindani na maadam *TANESCO* haiondolewi kwenye soko inaimarishwa, ninadhani kuna jambo muhimu tu hapa. Tuwakubalie na tuwaendeleze *TANESCO*, lakini makampuni haya tusiwe na wasiwasi ndiyo ushindani wenyewe huo; makampuni mangapi yameshindanishwa na sasa yanafanya vizuri? Kwa hiyo, tusiwe na wasiwasi, niwaombe Wabunge wenzangu tuukubali huu Muswada na niseme nina *interest*. Maana wadau wa kwanza watakaonufaika na Sheria hii ikipita ni pamoja na mimi. *ARTUMAS* ipo kwangu kule na wamejiandaa.

Leo ndugu zangu ninawaambia nchi ya Kenya inataka *gas under composed natural gas* ya *ARTUMAS*, maana yake hapa tunafanya *exportation* kujenga uchumi imara na wa kisasa wa nchi. Kwa hiyo, ndugu zangu tusiwe na wasi wasi, mimi niungane na watu waliotangulia kuunga mkono hoja, sikuwa na mengi kwa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nami nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ninaomba niseme kwamba, Muswada huu ni chimbuko la sera tuliojiwekea sisi wenyewe (*National Energy Policy*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila sheria zitakazowezesha *ku-implement* sera hiyo, hatutajitendea haki sisi wenyewe hivyo, ninaomba kuunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama habari za kitaalam zinazovyyotuambia kwamba, Gridi yetu ya Taifa imezidiwa kwa asilimia kumi na tukiiacha hivyo hivyo mpaka mwakani itazidiwa kwa asilimia 33.7 hivyo, tutakuwa na tatizo kubwa na la ukosefu wa umeme. Kwa hiyo, hatuna budi kuruhusu Muswada huu ili Makampuni haya binafsi yaje

kusaidia kuongeza nguvu ya Gridi yetu ya Taifa. Kwa hiyo, sisi ambao hatuna umeme kama Namtumbo, tunaukaribisha kwa asilimia 100 Muswada huu kwanza, kwa kuongeza uwezo wa *grid* na pili, kwa kutufikia sisi tusio na umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, suala hili la umeme wa gridi kuzidiwa kwake, uwezekano wa huduma ya umeme kufika vijiji ni itakuwa ni ndoto. Ninaomba Wabunge wenzangu akina Mheshimiwa Said Arfi, wabadilishe mawazo yao, tuunge mkono huu Muswada. Ninaomba Waziri awe na uwezo wa moja kwa moja wa kisheria wa kutunga Kanuni ya kulazimisha wanaoomba leseni, kama hawatafuata ifungu cha 39(4) na (5), kufanya hivyo kwa mujibu wa yifungu hivyo. Kifungu cha 39(6) katika *schedule of amendments* kinasema kwamba: “*The Minister may make regulations prescribing the manner in which sub-section (4) and (5) may be implemented.*”

Ninaomba kisomeke namna hii ili kumwongeza nguvu Mheshimiwa Waziri kwamba: “*The Minister shall make the regulations prescribing the manner in which sub-section (4) and (5) may not be implemented.*”

Hii ninaamini itaongeza nguvu, itasukuma zaidi na kuwa na uhakika wa *rural electrification* toka asilimia moja ya sasa na *ku-speed up* kazi hiyo kwenda vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii pia kutoa ombi la Wana-Namtumbo, wakati wanashubiri umeme huu wa gridi wanasema kwa kuwa Mtwara na Lindi watapata tukishapitisha Muswada huu, watapata umeme ule wa gesi. Kwa hiyo, wanakumbushia ombi lao lile kwa Mheshimiwa Waziri kwamba, tupate lile jenereta linalotumika kule ili tuanze kuzoea kuwa na umeme mpaka hapo umeme wa gridi utakapofika ili tusije tukauogopa ukifika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la sisi kukosa umeme, nilishalitaarifu Bunge lako Tukufu wakati ule kwamba, lilisababisha mpaka kifo cha Afisa wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo. Alikwenda kununua mafuta katika kituo cha mafuta na wakati anaenda kulipa ilikuwa ni usiku wanatumia chemli, kwenda kuhesabiwa kupewa risiti yake, mafuta yale yakalipuka kwa sababu ya ile chemli, hii yote ni sababu ya kukosa umeme. Kwa hiyo, tunaomba sana Muswada huu upite na ninarudia tena kwamba, Wana-Namtumbo wanaomba yale majenereta yatakayoachwa Masasi, basi yaje Namtumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina ya kuongea zaidi, ninawaomba sana wenzangu wasifikirie tofauti; Muswada huu ni kwa ajili ya *National Interest*; kwa hiyo, tunawaomba sana sote kwa pamoja, tuunge mkono ili uje kuisaidia Gridi yetu ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie huu Muswada wa Umeme. Kabla sijaendelea, ninaomba nitangaze maslahi; mimi ni Mjumbe wa Bodi ya *TANESCO* lakini vile vile katika kuchangia ninajikuta nina mgongano wa maslahi vile vile. Kwa mgongano huo ili kumwondoa mdogo wangu mashaka, nitamke kwamba, ninaunga mkono hoja, lakini

pamoja na kuunga, yapo mambo ambayo itabidi niyaeleze na niiombe Wizara iyatilie maanani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, nimesikiliza kwa makini sana wachangiaji walipokuwa wanazungumza, wanaishambulia sana *TANESCO* na ndipo hapo ninaposema ninatangaza maslahi. Kama sikosei ilikuwa mwaka 2001 au 2002, ililetwa Kampuni ya *NetGroup* na Serikali iliileta kampuni hii kwa dhana ya kuja kuifufua *TANESCO*. Kilichotokea ni nini? Ilikuja kuiua *TANESCO* kwa hili nitakalolisema. Inaitwa *NetGroup Solution*, sasa ilichofanya kampuni ile na niseme kwa Kiingereza pengine inasikika vizuri zaidi, *they came, they grouped us, they netted us and there was no solution!* Ninarudia; *they came, they grouped us, they netted us and there was no solution!* *NetGroup Solution* ni moja ya vyanzo vya matatizo ya *TANESCO* ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msambya, kwa manufaa ya Watanzania, ninadhani ingekuwa vizuri hicho ulichokisema ukirudie kwa Kiswahili.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa! Kiswahili chake ni kwamba, hawa *NetGroup* walikuja, wakatukusanya, halafu baadaye wakatuzingira na hawakuwa na ufumbuzi wowote wa matatizo yetu ya umeme Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili siyo la *NetGroup Solution* ni la Serikali. Serikali ndio imeifikisha *TANESCO* pale ilipofika. Kwa kuifikisha, sasa ninafikiri pengine Serikali inatafuta njia ya kuisaidia *TANESCO* kuiondolea sehemu ya mzigo ili wapatikane wawekezaji binafsi ambaa na mimi ninaunga mkono, waweze kuondoa matatizo ambayo yamesababishwa na Serikali yenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza, mimi ni Mjumbe wa Bodi ya *TANESCO*; *TANESCO* wameomba mkopo kwenye benki binafsi na wakapewa ili wapunguze baadhi ya matatizo ya kiuendeshaji yaliyoko *TANESCO*. Bahati mbaya siwaoni watu wa Hazina hapa, lakini mkopo umeombwa na ambaa una riba. Imechukua zaidi ya miezi minane tangu mkopo kuthibitishwa na Benki mpaka kupata kibali cha Serikali. Kwa hiyo, hapo unajua na *TANESCO* inashindwa kufanya mambo yake kwa mujibu wa mahitaji ya nchi. Sasa, ningemba basi wakati tunapitisha sheria hii, Serikali ijitazame upya, ione kwa dhati kabisa, namna ambavyo wataisaidia *TANESCO* na siyo kwa dana dana, hapana. Waisaidie kwa dhati ili *TANESCO* iweze kutoa huduma stahiki kwa Watanzania. Mheshimiwa Kaboyonga, ametoa takwimu nzuri na ndio za ukweli. Takwimu hizo ndizo tulizokuwa tunazijadili kwenye Kikao cha Bodi cha mwisho mwezi uliopita. Sasa, kama Serikali itafuata ushauri wa Mheshimiwa Kaboyonga na Wabunge wengine waliosema kuhusu *TANESCO*, ninaamini kabisa, *TANESCO* itaingia kwenye ushindani ikiwa na nguvu na wala haiwezi kuogopa kwamba anakuja mwekezaji binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ieleteke tunawaita wawekezaji hawa binafsi waje wasaidiane na *TANESCO* katika kuzalisha umeme nchini. Vilevile ni vizuri ifahamike kwamba, nilidhani ingekuwa vizuri akija mwekezaji binafsi, tufanye kama wanavyofanya wenzetu Kenya; haendi mtu kuwekeza katoka London, New York, katoka Japan, akafika akawekeza kama yeche na lazima awe na ubia na Mkenya. Hii itaondoa mchezo kama uliotokea kwenye Hoteli moja ya kitalii; imebadilisha mikono mara tatu kwa ujanja

ujanja tu. Hii yote ni namna ya kukwepa kodi na gharama nyingine ambazo wanetakiwa wailipe Serikali ya Tanzania. Kwa hiyo, nilikuwa ninafikiri kwa hili na nimesoma kwenye Muswada huu, kuna mahala ambapo hawa wawekezaji pale watakapoweka mitambo yao, watatakiwa kumiliki ardhi. Hivi, ardhi yetu ina mahala kuna sheria inaruhusu mwekezaji binafsi apewe ardhi? Ardhi kwa mujibu wa Sheria ni mali ya Watanzania. Sasa huyu mgeni ili apate uhalali wa kumiliki ardhi ni vizuri angeshirikiana na Mtanzania na kwa bahati nzuri Watanzania wenye vijisenti wapo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipokuwa anazungumza Mbunge wa Mpanda, Mheshimiwa Arfi, hapa watu walibea. Hapana, nimepitia kijitabu hiki alichokuwa anasoma, ambacho kimetoka Ofisi ya Waziri Mkuu. Ukiiruka Mpanda bila kuiweka kwenye umeme wa Gridi, maana yake unauruka na Mkoa wa Kigoma na hasa kwenye kata ambazo ziko kwenye Jimbo la Kigoma Kusini ambako mimi ni Mwakilishi. Ukiishaunganisha Mpanda, ukapeleka mpaka Kigoma kwenye umeme wa Gridi ambao utatoka Ruvuma au Mtwara, unanipa nafuu na mimi kwenye Kata za Kalya, Buhingu, Sigunga, Sunuka na Ilagala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze wazi kwamba, kwa sisi Mkoa wa Kigoma, hawa wawekezaji binafsi watatusaidia sana. Mimi huwa ninashangaa; nikiwa Dar es Salaam, umeme unakatika dakika tano watu wanapata homa. Sisi tuko kwenye mgawo tangu hatujapata uhuru. Maana sisi umeme siku ukikatika na usipokatika, *the difference is just the same*, hakuna tofauti.

Niishukuru Serikali ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa juhudini walizofanya kwa kushirikiana na *MCC*, wanatuwekea *Mini-Hydro* pale Igamba – Uvinza. Bahati mbaya, kwa hujuma zilizotokea Wizarani, tunawekewa *Megawatt* 9 na pale mahala pana uwezo wa kuzalisha *Megawatt* 45. Sasa viongozi waliokuwepo Wizarani, *MCC* walitaka kushirikiana na *African Development Bank (ADB)*; mtu kwa maslahi yake binafsi anasema, hakuna haja ya kuwaweka hawa watu wawili wakazalisha umeme. Umeme ambao ungezalishwa kwa *Megawatt* 45, ungetosha hata kumaliza tatizo la Mheshimiwa Arfi; ungekwenda Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Kigoma. Hivi leo huo utakaozalishwa na *MCC*, Wilaya ya Kibondo haiwezi kupata na Wilaya ya Kibondo ni sehemu ya Kigoma. Kwa hiyo, Wizara inafanya makusudi kutugawa watu wa Kigoma ili watu wa Kigoma wachukiwe na watu wa Kibondo, watu wa Kasulu wachukiwe na watu wa Kibondo kwa sababu umeme utakuwa hauwezi kwenda Kibondo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa ni ushauri wangu vilevile wakati tunakaribisha hawa watu, Wizara itazame upya, huu mradi ambao unasihamiwa na *MCC* chini ya uongozi wa Serikali, kama wanaweza wakaingia kwenye mazungumzo mapya, mimi ninasema ni vizuri hata wakachelewa kwa mwaka, lakini tukiwaingiza na *ADB* ili upatikane umeme wa kutosha, itakuwa ni vizuri zaidi kuliko katika Mkoa huo huo, sehemu moja ya Mkoa inatengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wale wamesema kwamba, umeme utakaozalishwa pale Igamba, utakwenda kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya Kasulu na

Kigoma, lakini vilevile utapita kwenye maeneo ya vijijini. Niombe Wizara isimamie kweli, maana kama walivyosema wachangiaji wengi hapa, hao wazalishaji binafsi, dhana ya kwamba kijijini kunahitajika umeme, haipo akilini mwao. Sasa ni vizuri tukaangalia umeme huu upelekwe kwenye viji kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nieleze kwamba, kama nilivyosema, ninaunga mkono hoja hii, lakini katika kuunga leo kwenye hiki kitabu zipo Wilaya kama nane na kwa bahati nzuri nimewahi kuwepo Wizarani pale, ninashukuru Wilaya hizi ambazo zinatakiwa zipate umeme, sasa zimepungua. Wilaya hizi nane, huko nyuma uliwekwa utaratibu, kulikuwepo na *Escrow Account*, ambayo ilikuwa inatakiwa iondoe tatizo la umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya zote ambazo zilikuwa hazina umeme na vilevile isaidie kupeleka umeme vijijini. Leo hii akaunti na ninasema ni kwa hujuma za Serikali, ilipelekwa kwa matumizi mengine na kwa maana hiyo, kama alivyosema Mbunge mmoja hapa, kila Mbunge analalamika kwa kutokuwa na umeme kwenye viji vyake. Sasa tunailamu *TANESCO*, lakini tunaacha tulipojikwaa, tunatazama tulipoangukia. Tulipojikwaa ni Serikalini siyo *TANESCO*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie, ninasema nina masilahi kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Bodi ya *TANESCO*. Siku ya Ijumaa nilimsikia Mheshimiwa Mbunge mmoja anazungumzia kwamba, watumishi wa *TANESCO* wanalipiwa umeme na *TANESCO*, lakini gharama zinapandishwa kwa watumiaji wengine. Ndugu zangu, kila mtu pale anapofanya kazi anakuwa na marupurupu yake. Sisi Wabunge hapa, ninafikiri hilo tungesema, kwa sababu mwananchi wa kawaida aliyeko kule kijijini hawezi kwenda Benki akapewa mkopo bila kuwa na *collateral*; Mbunge gani anakwenda *CRDB* kuchukua mkopo kwa *collateral*; mbona hili hatulisemei? Tunapata mikopo sisi kwenye mabenki haya kwa barua ya kutoka kwa Katibu wa Benki, ndiyo *collateral* yetu. Nani anapata barua kutoka kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji, kwenda kuchukua mkopo benki? Sasa tusione tabu kwa mtumishi wa *TANESCO* kupata nafuu ya kulipiwa umeme, ndiyo marupurupu anayoyapata kazini kwake na kila mtu kwenye sehemu yake ya kazi anayo marupurupu yanayompa motisha ya kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika Muswada huu wa umeme. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wengine wote, kwa maandalizi mazuri sana ya Muswada huu ambao umechukua muda mrefu, lakini wameuleta ukiwa umeboreshwa vizuri sana. Pia pongezi nyingine ziende kwa wanasheria wetu, ambao wamekuwa wanatusaidia katika Kamati zetu. Wamekuwa makini sana, wamekuwa wakirudia rudia mara kwa mara kutoa fasili, imefika mahala tumeuelewa vizuri zaidi Muswada huu, wameturahisishia sana. Kwa hiyo, ndugu zetu wanasheria mnaotusaidia, tunawapongeza sana kwa juhudhi hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Ngeleja na Mheshimiwa Malima, walivyoanza wanaenda vizuri. Hii kazi ilikuwa ni nzito sana, lakini jinsi walivyoshikamana na kwa baraka zake, Mheshimiwa Rais, akawapa nafasi kuchukua Wizara hiyo, wanaenda vizuri mno. Ninaomba waendelee kushikamana, watatufikisha mbali. Ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, niunge mkono kwa asilimia mia moja Muswada huu. Ninasema ninauunga mkono kwa asilimia mia moja. Sheria hii inaelekea kupita na tuna imani kabisa itapita. Ningependa nizungumzie machache kuhusu hali halisi ilivyo kwa Shirika letu la *TANESCO*. Hali ya *TANESCO*, kila mmoja anaifahamu, tumehangaika nayo muda mrefu na hali yake ilivyo sasa hivi tunaifahamu kila mmoja, *TANESCO* ina matatizo yake. Leo hii tunapitisha sheria hii tukiruhusu kuwe na soko huria kwa maana ya kwamba na watu binafsi watakuwa wanazalisha umeme na kuuza. Hali ya hii *TANESCO* ni mbaya sana na ili tuweze kuilewa ubaya wake, nilipata fursa ya kupitia kitabu hiki cha Mkaguzi Mkuu wa Serikali, ukurasa wa 69 ameelezea tu mashirika ya umma na taasisi nyingine zenye matatizo ya kuijendesha kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukursa wa 70 akalenga zaidi kwenye Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*). Nitanukuu baadhi ya maneno ili baadae tuendane na yale niyotaka kuyazungumza. Amesema: “Hali ya kifedha ya shirika inaendelea kuwa mbaya, kutokana na gharama kubwa ya umeme unaonunuliwa toka kwa wazalishaji umeme binafsi; hasa toka kwa *Independent Power Tanzania Limited* na *Songas Limited*. Hali hiyo imetokana na ukame wa muda mrefu nchini.” Hiyo ni picha ambayo ameieleza Mkaguzi hapa, lakini akaendelea kusema: “Katika mwaka wa fedha wa 2006, gharama ya kununua umeme ilizidi mapato yake kwa shilingi 445,000,000. Athari ya hali hii ni kwamba, shirika limejiendesha kwa hasara ya shilingi 137,959,000, *gross loss* katika mwaka 2006 ukilinganisha na hasara ya shilingi 54,563,000,000 mwaka uliopita, yaani mwaka 2005. Hadi kufikia Desemba 2006, madeni ya shirika yalifika shilingi 87 bilioni.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishaelezwa mpaka kufika hapo, leo hii *TANESCO* unataka uiruhusu iende kushindana na hali hii hawataweza! Niombe Serikali, ijithidi sana kuiweka *TANESCO* katika hali nzuri, madeni yote yanayosomeka hapa yabebwe na Serikali na ipewe mtaji, itafanya kazi nzuri zaidi. Tusimpeleke tu *TANESCO* kwenda kushindana akiwa na hali hii; hali ya soko huria tunaifahamu, wakulima wameteswa na soko huria, imekuwa ni soko holela, watu wanateseka. Leo hii kwenye zao la pamba na mazao mengine, watu wanateseka, bei haieleweki. Kwa hiyo, *TANESCO* ni tegemeo la Watanzania maskini, tuiwezeshe iweze kutuokoa Wananchi wa Tanzania, isiachwe kiholela ikaingia kwenye mashindano ambayo yako mbele yao ikiwa na hali hiyo.

Tuna imani na Dr. Idris Rashid, ni mtalaam wa uchumi, atatuvusha iwapo tutamwondolea mizigo ya madeni haya, itafika mahala *TANESCO* itaonekana kwamba, ndiye mkombozi wa Watanzania katika hali ngumu hii waliyonayo. Niombe sana Serikali ilizingatie hilo, pamoja na kwamba tumesharuhusu soko huria, wale wengine tunawakaribisha, lakini tegemeo letu ni kwenye *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EWURA* ndiye msimamizi wa hizi shughuli zote, atailinda *TANESCO* na washindani wengine. Tunaomba awe imara, asicheze kwa kuegemea upande mmoja. Asimamie, hali ni mbaya mno! Sasa hivi mwananchi wa kawaida kuingiza umeme kwa shilingi 600,000 hawez. Tupate msaada wa hali ya juu ili angalau tuweze kufika huko tunakoeleke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumzia mambo mengi sana, wametaja namna nguzo zinavyopita. Baadhi ya vijiji vimepitiwa na *line* ya umeme huo lakini havina umeme. Zipo Wilaya nyingi ambazo hazijapata, tuombe kabisa *TANESCO* wajaribu kuangalia uwezekano wa vijiji hivyo ambavyo vimepitiwa na *line* ya umeme. Nitoe tu mfano; katika Jimbo langu la Misungwi, kuna umeme uliotokea Kiesesa – Mwanza kuja Sumve, umepita katika Kijiji cha Bujingwa, Kanyerere, Kolomije na baadaye Sumve. Sumve sasa hivi tayari wana umeme, Kolomije nguzo zimepita hapo hapo; kuna sekondari, kituo cha afya, *centre* kubwa na mashine za kusaga.

Vivyo hivyo Kanyerere kuna sekondari, zahanati na vitu vingi viro pale. Hali kadhalika, Bujingwa kuna sekondari inayojengwa. Sasa hapo ni kuweka transfoma na kusambaza umeme ukaanza kuvuna. Niombe sana hilo, wafikiwe wananchi ambao wanapitiwa na *line* za umeme, transfoma zipatikane uteremshwe umeme na baadaye wananchi wa maeneo hayo waweze kufaidika na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka wakati nikichangia kwenye bajeti iliyopita, nilizungumzia maeneo ambayo Mheshimiwa Waziri anayafahamu. Kulikuwa na mradi fulani wa kupeleka umeme kwenye chanzo cha Kahama na Shinyanga; nguzo zilisimikwa na nyaya zikaletwa, transfoma imewekwa ipo kwangu, lakini baadaye ilibadilika ikabidi umeme uchukuliwe *line* ya pili kuja kwenye chanzo cha maji. Ilitakiwa zile nguzo zing'olewe, baadhi ya vijiji viligoma, nguzo bado zipo na nyaya bado zipo. Sasa ningelipenda Waziri anihakikishie au anieleze; hivi kuna ugumu gani wa kuruhusu wananchi wa maeneo hayo, wawekewe umeme ambao nguzo zipo na nyaya zipo; tatizo liko wapi?

Ninajua Mheshimiwa Waziri ana shughuli nyingi, aliniahidi kwamba, angelitembelea eneo hilo mpaka Kijiji cha Seeke na Buhingo na baadaye kuongea na wananchi wa maeneo hayo, lakini hajapata nafasi. Ninapenda tu labda nimsaidie kwa njia moja, mitaomba waandishi wa habari ambao ni figa letu la nne ambalo tunalitegemea sana, twende nao kwangu, wakayaone na watoe kwenye Tv, waone nyaya zilivyorundikana na vitu vyote ambavyo vinawenza kabisa kuunganishwa wananchi wakapata umeme. Hali ni mbaya, wataona kwenye Tv jinsi nyaya zilivyo.

Watu wengine wanalilia nyaya na nguzo, mimi kila kitu kipo, kinachotakiwa ni Serikali kufika pale na kuunganisha wananchi wapate huduma hiyo. Mazao yalivurugwa, hawakupata *compensation* kwa kutegemea umeme. Vijiji vya Buhingo, Seeke, Nyamayinza, Mbalama, Isesa mpaka Ihelele, wana matatizo makubwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina masikitiko makubwa, iwapo hatutatendewa haki wananchi wa maeneo hayo na Ilani ya Chama cha Mapinduzi inaelekeza kwamba, umeme utafika vijijini, itatupa shida sana siku za usoni. Kwa hiyo, ninaiamini Serikali ya

Chama cha Mapinduzi, kwa kuwa ni sikuvi, hilo basi watalichukulia maanani na kulipa heshima ya pekee ili angalau tuweze kumaliza kero hiyo, ambayo inatusumbua sana katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamezungumzwa na wenzangu, lakini ninataka niulize moja; sijui kuna utaratibu upi kwa mfano; kuna sehemu nyingine nguzo za umeme zimepita, lakini labda kuna mwekezaji mwingine au tuseme ni mkodishaji kama atakuwa tayari kuweka transfoma yake akashusha umeme wake, mkaelewana naye ninyi watu wa *TANESCO* inakuwaje; maana yake wewe unaweza kuona hakuna faida, lakini yule mwingine anaona akiteremsha pale, faida itapatikana; kwa nini asiruhusiwe kufanya hivyo, wakaelewana na watu wa *TANESCO* na wengine? Ninajua ni biashara, lakini kama wataweza kuwasiliana wanaweza wakalifanyia kazi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni zetu zinatuzuia kurudia kurudia, labada kuna hili moja ambalo Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani aliwahi kuniahidi akiwa Naibu Waziri wa Nishati; kuna kijiji changu kimoja cha Nyan'ghomango pale karibu na Usagara, tayari pale kuna umeme kwenye viwanda vingine; Kuna kiwanda cha nondo kinajengwa pale Nyan'ghomango, wana umeme wao tayari, kile kijiji kinahitaji nguzo chache tu; Kijiji cha Nyangomango na baadaye tuwfakirie watu wa Fela. Aliniahidi kwamba, atalifanyia kazi. Leo hii Mheshimiwa Waziri yupo, Nyan'ghomango anaifahamu vizuri sana, hebu tuwfakirie Wananchi wa Nyan'ghomango waweze kufaidika badala ya kumwangalia mwekezaji yule anayetutengenezea nondo pale nao waweze angalau kupata umeme waendelee na shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelzo hayo, nikushukuru sana lakini kwa msisitizo kwamba, wakati wanawahudumia Wananchi wa Misungwi, Peramiho nao wana matatizo kama ya Misungwi; wafikiriwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Kicheko/Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Shibili. Peramiho wamekusikia, ninashukuru na kule Nyan'ghomango wamekusikia. Kwa hiyo, kwa kweli tuko pamoja.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kupata nafasi ili na mimi nichangie machache kuhusu Muswada huu wa Umeme uliopo mbele yetu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu, tuna Mradi mkubwa ambaa uko pale Somanga – Fungu. Mpaka leo ule Mradi unasuasua, uko nyuma kwa miezi 16 hadi leo. Ninataka niliseme hilo kwa sababu wakati tumeanza kuomba kura, tulikuwa tumetoa ahadi kwamba tutakuwa na umeme wa kutosha Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilwa ni wazalishaji wakubwa wa gesi ambayo inakwenda Dar es salaam, lakini Wilaya yenye haina umeme. Ni aibu kubwa sana kuwa na nishati ya gesi halafu unakosekana umeme. Tuko gizani, tunaambulia

vikorboi tu. Pale Wilayani Kikwa Masoko, tuna jenereta bovu tangu wakati wa mkoloni. Umeme ni wa kusua sua na tunaupata kwa mgawo kutwa mara tatu kama dawa za Panadol! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Mradi wa Somanga - Fungu unatuletea aibu kubwa sana; unategemewa na majirani zetu wa Rufiji, Kibiti na Bungu, mpaka leo imekuwa kitendawili tu. Amepatikana mkandarasi mmoja mbovu hafai kabisa kila siku anatoa tarehe tu; *civil* yetu bado, huo mtambo wenyewe *testing* bado, siku zinakwenda tunakaa na vikorboi hatuna umeme. Mheshimiwa Waziri, analijua hili na Mheshimiwa Rais, alikuja pale analijua lakini mpaka leo bado ule mtambo unasuasua na hatuna umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linanitia uchungu sana kwa sababu ninazalisha gesi kwa wingi sana Songosongo inakwenda Dar es Salaam, wanaofaidi ni watu wa Dar es Salaam, lakini mimi niko gizani sawasawa na mtu ana mwembe lakini anashindwa kula zile embe, kuna jamaa anakuja kuzichukua usiku. Kweli nina mwembe, lakini tunda lile silifaidi, jambo hili linanitia huzuni sana na wenzangu majirani vilevile wana matatizo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, pesa za fidia kwa wananchi wangu shilingi milioni 400 zimepatikana zinakwenda kwa wananchi wa Bungu, Kibiti, Ikwiriri, Somanga, Miteja, Nangurukuru, Singino na Mikwajule, watapata hizo pesa za fidia. Mheshimiwa Waziri, ameshanihakikishia kwamba, cheki ya shilingi milioni 400 ameshakabidhiwa *DC*, kwa hiyo sina matatizo na hilo. Nina matatizo makubwa kuhusu umeme, ukizingatia Kilwa kama Mji Mkongwe na wa kitalii, hatuna umeme; jamani tunakwenda wapi? Tunataka ku-*promote* utalii hatuna umeme.

Baada ya kusema hayo, ninataka niseme machache kuhusu *Songas; capacity charge* tunazolipa za milioni 200 na zaidi, pale gesi inapotoka hatuna huduma ya aina yoyote. Kijiji cha Songosongo hakuna huduma wala ajira; wananchi wangu hawapati chochote kutokana na *Songas* na *Pan African Energy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Pan African Energy* sijui kwa nini tunawaweka pale, wanazidisha hizo *capacity charge*, bei inaongezeka ndiyo inaleta mzigo mkubwa kwa *TANESCO*. *Songas* inawashinda milioni mbili kuchangia sekondari, mradi ambao unaingiza milioni 200 na zaidi kwa siku moja, mikataba yote ni bomu, ndiyo inayoleta *TANESCO* iwe mufilisi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matatizo sana, ndugu yangu, Mheshimiwa Msambya hapa amesema kwamba, marupurupu Kilwa hatuna, Kijiji cha Songosongo kinatozwa umeme sawa na *tariff* ya Taifa, uhariifu mkubwa unafanyika pale Songosongo na ule mradi. Zao moja tu la mwani ndio linaloota pale na sasa hivi umeathirika hauzai. Wanakijiji walikuwa wanapata tani hamsini za mwani, sasa hivi tunazalisha tani saba au nane kwa mwezi. Wanakijiji wa Songosongo hali zao ni duni, ule ni mwamba hakioti kitu, walikuwa wanautegemea mwani na sasa hauzai kwa sababu ya *effects* za ule mradi, mwanakijiji atafanya nini; umeme alipie bei ya kawaida, hakuna marupurupu, mradi kuchangia sekondari ni matatizo, ukiwaambia wanasema *We will do*

*it; when are they going to do?* Michezo vijana wangu Songsongo inawashinda, mipira na jezi hawana! Hii Mikataba ya Songsongo ni bomu na hatumtaki *Pan African Agency*, tunaongeza gharama bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la mwisho ni kuhusu mrabaha kutokana na gesi yetu ya Songsongo; Wilaya yangu ya Kilwa ifaidike, haina kipato, wananchi wangu hawazalishi kwa sababu ya *splitting* ya mafuta na kuharibu mazingira, hatuna mrabaha wowote unaotokana na Mradi wa Songsongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikikwambia mimi kwa sababu kinanihusu na kinanikera, mrabaha kama wa Mwanza, Geita huko wanapata kutokana na dhahabu ambayo inatoka chini ya ardhi ya Mwenyezi Mungu, gesi pia inatoka huko huko chini; nimekosa nini na wananchi wangu wamekosa nini, huu mrabaha hauingii mfukoni kwangu? Inabidi Halmashauri yangu tukae, tuufanyie kazi Mradi huu ulete maendeleo Kilwa. Sijapata mrabaha, matatizo moja kwa moja; niko gizani, umeme sijapata; basi wafaidi huko Dar es Saalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema ninaunga mkono hoja hii iliyopo mbele yetu, lakini nina uchungu sana na mwembe ambao sifaidi tunda lake. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Dewji na pole sana kwa kutunza mwembe halafu maembe huyafaidi. Ninaomba nimwite Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na mMuda wetu ukiruhusu zaidim tutamsikiliza Mheshimiwa Blandes.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kupata fursa hii ili niweze kuchangia huu Muswada wa Umeme wa 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, pamoja na Wataalam wao, kwa jinsi walivyoleta marekebisho yanayohusu Muswada huu, baada ya vuta nikuvute. Watanzania wanabubiri kwa hamu ni jinsi gani Muswada huu utakapokuwa sheria, watapata manufaa kutokana na Muswada huu au itakuwa ni sawasawa na Miswada mingine yote ambayo imekuwa ikipita hapa halafu Watanzania wanaingia katika dimbwi la matatizo wala hawaelewii ni kitu gani kinachofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavutiwa sana na ukurasa wa tisa, aya ya (6), juu ya kazi za chombo hiki kinachoitwa *EWURA*, kuwalinda watumiaji wa umeme katika nchi hii. Mambo yameandikwa vizuri sana kutoka (a) - (h). Mfano, ninanukuu kifungu (b) kinasema: “*Kazi itakuwa ni ku-promote access to and affordability of electricity services particularly in the rural areas.*” Suala la umeme tunaouzungumzia leo hapa ni ule utakaokwenda vijijini zaidi, kwa sababu tumetunga na kuitisha sheria juu ya umeme lakini ndugu zangu *TANESCO*, wameshindwa kabisa kupeleka huo umeme vijijini, kwa sababu umeme wanaousambaza nchini toka tumpatwa uhuru ni asilimia kumi tu ya Watanzania ndiyo wanaoupata huko mijini.

Umeme uliosambazwa katika vijiji vya Tanzania ni asilimia moja tu na asilimia moja hiyo ni katika mikoa fulani fulani tu, sehemu kubwa bado iko gizani. *TANESCO* wameshindwa kwa sababu ambazo wenzangu walotangulia wamezitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hali ni hiyo; tatizo ni nini? Tatizo ni mikataba mibovu, ambayo imetajwa hapa sina sababu ya kuirudia; *RICHMOND, IPTL, DOWANS, AGGREKO* na mingine. Kila siku ninajiuliza; vyombo vinavyohusu gesi, mara zote huweka kitu kinachoitwa *safety valve* ni *valve* ya usalama kwamba, likitokea jambo, hapo ndipo unaweza kubonyeza ili gesi ile iliyojaa sana kupindukia, iweze kutoka na watu wakabaki salama, lakini usipofanya hivyo ni dhahiri gesi ile italipuka au mtungi ule utalipuka na watu waliopo pale wataumia.

Katika mikataba yote inayoingiwa hapa Tanzania, haina *safety valve*, kwa sababu inapofika wananchi au Bunge linaiuliza Serikali; huu mkataba mliingiaje tunataka muuvunje, wanasema hapana kwa sababu kuuvunja mkataba huu tutapata hasara sana, tutashtakiwa na tutalipa fedha nyingi! Hivi wanasheria hawana *safety valve* ya kuwasaidia Watanzania wasibebe mzigo usiohitajika katika nchi hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba yote inayowekwa na Serikali, inamkandamiza Mtanzania ili aweze kulipa zaidi na zaidi. Hiyo haiwezekani, mikataba isiyokuwa na *safety valve* kwamba tukishindana, wewe usipotimiza hivi, basi sisi tutafuta mkataba huu kwa sababu hujatimiza hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mbunge mmoja ananiambia kwamba, *safety valve* hakuna kwa sababu kuna *ten percent*, kumbe wakikamata *ten percent* na *safety valve* hakuna! Watanzania waendelee kuumia, hii haiwezi ikakubalika katika Tanzania hii ya utandawazi. Usipokubali kuwasaidia Watanzania waepukane na migogoro na wawekezaji ambao wataibana nchi na kuendelea kulipa hata kama hawapati huduma nzuri, unawaleta makampuni ambayo yatakuja kupata fedha yakaondoka na sisi tukabaki na matatizo na wewe ukabaki pale ukidhani umebak salama; kwa kweli Watanzania hawatavumilia mambo hayo. Mnapokwenda kusoma mikataba hii, hakikisheni lazima mnaangalia juu ya *safety valve*, mahali ambapo Watanzania wakichoka na mikataba hii wanasema tunatumia kifungu hiki ili tuweze kusema ondoka na tuangalie ni jinsi gani tunaweza kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Mikataba ya Ndege ni hivyo hivyo, Mikataba ya Reli ni hivyo hivyo na mingine. Hatuna *safety valve*, kwa sababu ya *ten percent*, hii ni aibu kubwa sana kwa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoolewa, hakuna mtu yejote ambaye atawekeza kiwanda mahali popote halafu aanze kusubiri umeme. Mtu yejote mwenye busara anapojenga kiwanda, anahakikisha kwamba, umeme upo wa kutosheleza ili kiwanda kile kifanye kazi, lakini fikra ambayo ipo kwa wataalam wanaofikiria kwamba, mfano, Mkao wa Rukwa mpaka viwanda viongezeke ndiyo walete umeme, hii ni fikra potofu. Umeme upatikane baada ya kiwanda kujengwa, hiyo haipo mahali popote duniani. Kwanza, miundombinu ijengwe na umeme ufile kule ili watu waweze kushawishika kuwekeza katika viwanda, hiyo ndiyo *principle* inayotumika duniani kote. *TANESCO* wakati wote

imekuwa ikisubiri ulalamike waseme hata tukipeleka umeme kule kwani kuna kiwanda? Anachofikiria kwanza ni kujengwa kiwanda halafu ndiyo asukumwe kujenga miundombinu ya umeme kupeleka kule. Anasahau kwamba, wapo Watanzania wanaohitaji umeme ule kwa kuendesha mitambo midogo midogo, ambayo itazalisha labda kwa kusaga unga au kufanya kazi nyingine kama vile kusindika matunda na vyakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusifanye kazi kwa mazoea, tusifanye kazi kizamani kwa sababu dunia hii ya utandawazi, haiwezi hata kidogo ikatuvumilia. Tutaendela kuumbuka kila siku, kwa sababu hatufuati *principles* ambazo zinakubalika mahali pengine duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Arfi amesema, hataunga mkono hoja kwa sababu ya mambo ambayo hayako wazi, lakini mimi ninaunga mkono Muswada huu ili waje watu binafsi, wanaoweza kuamua kuwekeza katika kanda. Ukanda wa Magharibi hauna kitu na kile kilichopo ni danganya toto, umeme unaokatika mara elfu kama alivyoeleza Mheshimiwa Kimiti katika Bunge lako Tukufu ni aibu tupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi ukawekeza kitu cha maana katika Ukanda wa Magharibi wa Tanzania, kwa sababu miundombinu ya umeme haipo, hilo ni jukumu ambalo tunapozungumzia Muswada huu, kama *TANESCO* wameshindwa, sisi tumeingizwa katika Gridi ya *ZESCO*, ambayo nayo imeshindwa kutupatia umeme wa kuweza kukidhi matakwa ya Tanzania. Wawekezaji wapo, *Upendo Group*, wanafikiria kujenga mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Namwele, lakini hawawezi kuwekeza katika mitambo hiyo, kwa sababu haijapitishwa Sheria hiyo. Ndiyo maana ninaunga mkono Sheria hii ipitishwe ili makampuni binafsi, yaweze kuwekeza pale mnapoona kwamba, hakuna faida wengine wakiwekeza watapata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku tumesikia Serikali imetoa fedha, umeme unasambazwa vijijini. Toka umeme wa Zambia umeingia Mkao wa Rukwa ni zaidi ya miaka minane, lakini hakuna hata kijiji kimoja kilichopatiwa umeme; ni mwaka gani umeme huo utasambazwa katika vijiji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba umeme katika Jimbo langu la Kalambo, uteremshwe katika Vijiji vyangu vya Matai, Sopa, Katuka, Msanzi, Singiwe na Kasesya mpakani kwa miaka saba, ambapo unapita kutoka Zambia unakwenda katika Mji wa Sumbawanga, ili watu waweze kufanya shughuli zao kama wengine waliopata maendeleo, lakini hakuna chochote mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme ule ukiweza kuteremshwa Matai upelekwe Kasanga katika bandari iliyoko katika Ziwa Tanganyika, ambayo nayo inajengwa, hakuna lolote mpaka kesho, maendeleo ya Mkao huu yatapatikana wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nkansi haina umeme mpaka kesho, Mpanda umeme unasuasua, lakini mpango thabiti ni kuunganisha katika gridi halafu umeme ukija

kwa wingi, ndiyo uweze kusambazwa katika Vijiji vya Mkoa wa Rukwa na katika Mkoa wa Kigoma, lakini ni mpango gani umeandaliwa? Ndiyo maana tunapitisha Muswada huu ili tuweze na sisi kupata wawekezaji, watakaokuwa tayari kuwekeza katika Mikoa yetu kama ilivyofanyika katika Mikoa ya Mtwara na Lindi. Tunahitaji na sisi tuweze kupata hata umeme wa makaa ya mawe na kusambazwa katika vijiji vyetu ili watu wetu nao waweze kupata manufaa ya umeme wa nchi hii. Suala la kutafuta Gridi ya Taifa ifike katika maeneo haya ili haki itendeke katika nchi hii, tunaomba Serikali iwe makini katika suala hili, hatuwezi kuendelea kusema bila Serikali kuchukua hatua ya kuyatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ninashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mwananzila na sasa ninaomba nimwite Mheshimiwa Blandes.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti nichukue nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwisho kwa siku ya leo. Kama wenzangu walivyofanya, ninaomba nichukue nafasi ya pekee, kumshukuru Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu wake, Mheshimiwa Adam Malima, Katibu Mkuu wao na kikosi kizima cha Wizara, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Sote ni mashahidi kwamba, Muswada huu mpaka umefika hapa, kwa kweli cha moto wamekipata, ninawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue nafasi hii kupitia Bunge lako, kutoa taarifa kuwa, jana kwenye Jimbo langu la Karagwe, kilitokea kitendo cha kihistoria, kwa mara ya kwanza, Timu ya *Simba Sports Club* ya Dar es Salaam, ilicheza Wilayani kwangu Karagwe na wachezaji wa Simba, kwa mara ya kwanza walijionea wenyewe mpira wa Karagwe jinsi unavyofanana, kwa sababu hadi mpira unaisha golikipa wa Simba; Juma Kaseja alishafungwa goli moja ingawa na wao walitufunga mawili. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza sana vijana wangu na nimeahidi nitaenda kuwapongeza. Ninapongeza pia mfadhibili wa timu hiyo, Bwana Karim Amri, kwa kuwapeleka Simba Karagwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba nigusie Muswada kama ulivyo, nitaenda kwa *substantive sections*, nitaanza na kifungu cha 25(1) na 25(3), ambacho kinazungumzia juu ya Mikataba ya Ununuzi wa Umeme. Sheria hii inalenga kuitambua mikataba ya kuuziana umeme na katika kifungu hiki namba 25(1), kinaongelea juu ya mikataba ya ununuzi wa umeme kwa maana ya kwamba, watakuwepo wauzaji na wanunuzi wa umeme huu, baada ya kuwekeana makubaliano. Katika sheria hiyo hiyo, mikataba hii itakapokuwa imefungwa, sheria itatambua kwamba, lazima pande zote mbili zikubaliane na hili jambo ni zuri sana. Ukiangalia kifungu hiki cha 25(3), kinaeleza kwamba, mikataba yote itakayofungwa katika kifungu 25(1) ni lazima isimamiwe na chombo maalumu na utaona kwamba hapa ndani ugomvi mkubwa umekuwa ni namna ya ufungaji wa mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nikatangulia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Sheria imeweka wazi mikataba yote, lazima itakuwa *approved* na mamlaka yetu ya *EWURA*. Mikataba itakapofungwa ni lazima ipelekwe *EWURA* waweze kui-*approve short of that*, zaidi ya hapo huo mikataba hautambuliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna upungufu kidogo kwenye kifungu hiki ambacho ningemwomba Mheshimiwa Waziri, baadaye akirekebishe kikae vizuri. Kifungu hiki kinasema kwamba, mikataba yote kama haitapita *EWURA*, *shall be void* kwamba haitatambulika kisheria ila wakaweka *proviso*, kuna maneno hapa yanaendelea ambayo sikuyapenda, yanasema *unless such agreements relate to (a) the cross border trade of electricity, the selling of electricity to eligible customers*, yaani kama mikataba uta *relate* na hayo mambo mawili; umeme unaouzwa nje ya nchi, *EWURA* hawataangalia mikataba hiyo. Umeme ambaa utauzwa kwa wateja ambaa ni *eligible EWURA* hawatapa nafasi ya kuangalia hiyo mikataba, sasa huu mwanya ningependa tuuzibe mapema usiwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza kwamba, yale maneno kuanzia kifungu (a) na (b) katika kifungu cha 25(1) yaondolewe moja kwa moja, tubakie na maneno yanaoanzia kipengele cha (c) na (b) zibadilike ziwe (a), (b), nina imani Mheshimiwa Ngeleja ananielewa kwa sababu ni Mwanasheria mwenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho hicho, nilikuwa ninajaribu kuangalia *schedule of amendments*, kwenye kifungu cha 25(3) mstari wa pili kati ya neno of na *authority ina-miss article (the)*, ambayo ni *very important*, ningemwomba Mheshimiwa Waziri aiweke vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti katika kifungu hiki cha 25(3) (a) na (b), utaona kikiachwa bila kufanyiwa marekebisho hayo, kinakuja kuleta mgongano na kifungu kilichotangulia cha 22(2) na 22(3), kwa sababu kifungu cha 22(2) chenyewe kinaeleza kuwa, maombi yote ya kuuza umeme nje ya nchi ni lazima yaambatane na mikataba ambayo ndiyo itakuwa kigezo muhimu cha kuweza kutoa leseni.

Kifungu cha 22(3) kinazungumzia kwamba, inapotoka mabadiliko katika mikataba wowote, labda wale waliokubaliana wanafanya *amendments* ya mikataba au wanaleta mikataba mpya, sheria inaeleza kwamba, lazima mikataba hiyo ipelekwe *EWURA* ili ipate nafasi ya kuihakiki. Jambo hili ni zuri isipokuwa ugomvi wangu hapa neno ambalo limetumika siyo zuri kisheria na litakuwa haliwabani hawa waombaji ipasavyo. Neno lililotumika ni *verification*, ningeshauri Mheshimiwa Waziri, abadilishe liwe neno *approval* hilo litakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu namba 17(7), kinahusu utoaji wa habari yanapotoka majanga ya umeme, pamoja na ajali. Kifungu cha 4(1)(h) kinazungumzia jambo hilo hilo.

(*Hapa umeme ulikatika*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, ninaomba uendelee kwa kuwa tunakusikia na ninadhani watu wetu watashughulika kuturudishia umeme muda si mrefu.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Inapendeza unapojadili Muswada wa Umeme na umeme unakatika. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninasema kuna kifungu hapa cha 15(7) na 4(1), ambacho lazima taarifa za ajali ya umeme zipelekwe kwenye vyombo vyetu vya Serikali. Sasa 4(1) inazungumza kupeleka taarifa kwa Mheshimiwa Waziri na 17(7) inazungumza kupeleka taarifa *EWURA*.

Ningependekeza kwamba, vifungu hivi viangaliwe kwa umakini ili angalau tujue ni wapi taarifa zinastahili kwenda; kwa Mheshimiwa Waziri au kwa chombo chetu cha *EWURA* ili kuondoa *confusion* na kuweza kuongeza uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye *TANESCO*; yamesemwa mengi sana. Watu wamezungumzia hali yake, hakuna ubishi na chanzo chake mpaka imefikia hapo. Mimi nilitaka nijiulize kabla ya kuzungumzia *TANESCO*; nini madhumuni ya Muswada huu; hivi ni kwa nini huu Muswada unakuja hapa Bungeni; maana yake ni nini?

Madhumuni ya Muswada huu yalizungumzwa kwamba ni kupendekeza masharti bora ya usimamizi wa Sekta Ndogo ya Umeme nchini, kutokana na mfumo wa biashara huria na changamoto zilizojitokeza hivi karibuni katika kuisimamia sekta hiyo. Maana yake ni kwamba, tunataka umeme wetu uwe wa soko huria.

Sasa Waheshimiwa Wabunge wengi ambao wamesimama hapa, ninaomba nitofautiane nao kidogo; tunalia *TANESCO* na ukiangalia katika kifungu 41(6), *TANESCO* wamebebwa kupita kiasi, wanasema kwamba, watapewa *right to first refusal* maana yake ni kwamba, ile miradi yote mizuri kwanza *TANESCO* waichambue ile mizuri halafu ile mibaya, sehemu ya mifupa fupa sasa ndiyo wapelekewe wawekezaji wengine; hivi ni mwekezaji gani atakayekubali sheria ya namna hii na kuja kuwekeza hapa nchini? Mimi simwoni, kwa sababu hata mimi kama ninataka kuwekeza, lazima niwekeze sehemu ambayo ninajua nitapata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitoe ushauri, tuna mifano mingi sana, Benki ya *CRDB* ilishakufa kabisa, lakini baada ya kuifutia madeni, kuuza hisa kwa wananchi na kumkaribisha mwekezaji, Benki ya *CRDB* imeendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Blandes. Waheshimiwa Wabunge, kwa dakika chache zilizobakia, Mheshimiwa Mollel amesema kwamba, anaweza akazitumia vizuri tu kufikishia ujumbe wake.

Kwa hiyo, ninaomba nimwite Mheshimiwa Mollel na ndiyo atakuwa msemaji wetu wa mwisho kwa siku hii ya leo.

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, ambayo ni ya mwisho kwa jioni hii na mimi nitakuwa mchangiaji wa mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake, kwa kuandaa na kuwasilisha Muswada huu wa Umeme wa mwaka 2007.

Aidha, niipongeze Serikali kwa kukubali kufayanya kazi maoni na ushauri uliotolewa na wadau mbalimbali katika semina mbalimbali, kwa mfano, Kamati ya Nishati na Madini na Waheshimiwa Wabunge. Serikali kwa kukubali kuchukua ushauri huo, imeboresha sana Muswada huu ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umekuja katika wakati muafaka; wakati kuna kilio kikubwa sana na kero nyingi sana katika jamii kuhusu nishati ya umeme, kuunganishiwa umeme wa gharama kubwa; kutozwa gharama kubwa ya matumizi ya umeme kila mwezi na kucheleweshewa kupewa huduma ya kuunganishiwa umeme. Hivi tunavyozungumza, kuna zaidi ya wateja 10,000 ambaao wameshalipia huduma ya kuunganishiwa umeme, lakini mpaka leo wako bado wanasubiri kuunganishiwa umeme huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio ya wananchi ni kwamba, tukipitisha Muswada huu watakuwa na faida mbili kubwa; moja kupata umeme kwa bei nafuu na mbili nchi nzima itakuwa ina umeme itatoka kwenye giza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie kidogo juu ya *TANESCO*. Wengi wetu tumeilaumu *TANESCO* na kwa sababu za msingi kabisa, lakini ninaomba niseme kwamba, matatizo yote ya *TANESCO* yametokana na Sera ya Serikali yetu.

Matatizo ya *TANESCO* yametokana na *under capitalization*; imepewa majukumu makubwa ya kuzalisha na kusambaza umeme nchi nzima mijini na vijijini, lakini hawakupewa mtaji unaotosha kuendesha shughuli hizi na hata pale walipopewa, umekuwa mdogo na siyo endelevu.

Kwa hiyo, ninaomba niseme kwamba, pamoja na matatizo yote tulyonayo ya uzalishaji na usambazaji wa umeme, hayatokani na matatizo ya *TANESCO* bali yanatokana na matatizo ya Serikali yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiacha mitaji ambayo *TANESCO* imekosa kwa muda mrefu, nizungumzie juu ya mikataba mibovu ambayo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamezungumzia. Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi na Waheshimiwa Wabunge, wengi hapa ni mashahidi; mwaka 2002 tulikataa Serikali isiwaajiri *NetGroup Solution* kuja kufanya kazi ya utendaji na kuendesha shirika letu.

Serikali haikutusikia, waliletwa na wamepewa vipindi viwili vya kufanya kazi ya kuongoza *TANESCO*; nini kimetokea? Kwanza, katika kipindi chote cha miaka minne walichoongoza, yafuatayo yametokea: Kwanza, hadidu zile za rejea ambazo wamesaini hazijatekelezwa kwa asilimia 75, ninayo ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kazi waliyofanya hawa wataalam ni kukusanya madeni *on a selective basis*, madeni yale ya Serikali na asasi zake zile ambazo ni *easily collectable*. Zile ambazo ni za akina yahe zimeachwa, kiasi kwamba mpaka walipoondoka mwaka 2006, *TANESCO* ilikuwa inadai shilingi bilioni 201 kwa wateja mbalimbali. Fedha hizi ni mapato ya *TANESCO* karibu kwa mwaka mzima kutoka kwa watumiaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ni kwamba, hawakushughulika kabisa na *ku-repair* ama *continuous maintenance* ya mitambo ya *TANESCO*, kiasi ambacho mpaka walipoondoka, asilimia 80 ya mitambo ya *TANESCO* haikuwa inazalisha umeme ilikuwa imefungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nikueleze kwamba, tatizo lingine kubwa kabisa ni hili ambalo wenzangu walilisema la kwamba, sasa hivi *lines* za umeme zimeshaelemewa. Sasa hivi tunapoteza umeme mwingi sana unaozalishwa na hawa *private power producers*. Asilimia 33 ya umeme unaozalishwa hapa nchini, unapotea kabla haujapokelewa na *TANESCO*, hiyo ni *cost* ya shilingi bilioni 13 kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuupitishe Muswada huu. Tukiupitisha ndiyo itakuwa ukombozi wetu sisi kupata umeme vijijini vinginevyo, tazama miaka 50 ya uhuru wetu, asilimia kumi ya wananchi wa mijini ndiyo wenye umeme na asilimia moja ya wananchi vijijini ndiyo wenye umeme. Hata hii

asilimia moja ya wananchi wa vijijini, walio na umeme ni wale wananchi ambao wako kwenye *periphery* ya *urban areas*. Maana yake, hakuna miundombinu ya kuzalisha umeme kule vijijini. Tunahemea na kuibia umeme unaotoka kwenye miji. Vijiji vyatani kabisa hatuna umeme, tukiupitisha Muswada huu, tutaweza kupata umeme wa kuridhisha katika vijiji vyetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia niseme maneno mawili, matatu; utendaji wa *TANESCO* umeingiliwa sana na Serikali. Hapa kwenye taarifa ya *Controller and Auditor General*, kuna mifano mingi ambayo Mikataba imesainiwa na Serikali badala ya kusainiwa na *TANESCO*. Miswada kama *IPTL* na *Songas*, imekuwa *quoted humu* kuwa ni mikataba mibovu hii ambayo ina mamilioni ya fedha. Kwa mfano, hii ya *capacity charge* ndiyo inayouimiza *TANESCO* na uchumi wetu. Hapa kwenye *report* ya *Controller and Auditor General*, kwa sababu ya Mkataba wa *IPTL*, *Songas* na *Richmond* wamesema kwamba, kuna dola milioni 12 zinalipwa kila mwezi kwa *capacity charge*. Dola 144 milioni kwa mwaka ni fedha nyingi sana, ndiyo zinazofanya umeme uwe *very expensive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme kwamba, nimeona katika Muswada huu wa 2007, *capacity charge* haitakuwa *applicable* kwa wawekezaji wapya, hii ni hatua nzuri lakini swalii hapa ni kwamba; je, hizi *capacity charges* ambazo bado hawa *private power producers* wanalipwa kwa mikataba ambayo ipo sasa tunafanya nini, maana tusipojihidi kuondoa hizo basi hali itakuwa ni ile ile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaomba niseme kwamba, katika jedwali la marekebisho, kifungu cha 41(6) kinasema kwamba, *TANESCO* watapewa uwezo wa kifedha ili waweze ku-*compete* na vilevile wawekezaji binafsi watakaopewa leseni za kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni sawa lakini *section one* ya Muswada huu, inasema kwamba, Mheshimiwa Waziri atatangaza wakati muafaka wa kuruhusu sheria hii kuanza kutumika. Ninaomba niseme kwamba, ningetaka wakati wa majumuisho, Mheshimiwa Waziri atuhakikishie kwamba ni ipi inatangulia, maana kama Sheria hii ikija *into operation* kabla hali ya *TANESCO* haijarekebishwa, basi hakuna *fair ground* ya *competition*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mollel, kwa kutumia vizuri muda wetu na kutusaidia kumaliza ratiba yetu ya leo kwa kukuruhusu wewe uzungumze. Waheshimiwa Wabunge, kama kesho tutaendelea tena na mada hii, labda wachangiaji wa mwanzo ningewasoma kabisa ili waweze kujiandaa. Tutaanza na Mheshimiwa Magalle Shibuda, Mheshimiwa Anastazia Wambura na Mheshimiwa Juma Killimbah, atakuwa msemaji wetu wa tatu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge niliowataja, basi wangkuwa tayari kuanza kuchangia hoja yetu kwa siku hiyo ya kesho.

Ninaomba nichukue nafasi hii, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge. Ninaona kwa kuwa muda ambao umebaki umeshatutupa mkono na shughuli zetu za leo basi itatupasa tuishie hapa. Kwa hiyo, baada ya shughuli hizi zote za jioni, ninaomba niahirishe Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.39 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,  
Tarehe 22 Aprili, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*